
# ILANI YA UCHAGUZI YA ASASI ZA KIRAIA TANZANIA



## UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA 2019 NA UCHAGUZI MKUU WA 2020

"Tanzania Tuitakayo"

# ILANI YA UCHAGUZI YA ASASI ZA KIRAIA TANZANIA



## *“Tanzania Tuitakayo”*

**UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA 2019 & UCHAGUZI MKUU WA 2020**


AZAKI TANZANIA, SEPTEMBA 2019

# MAONI YA AZAKI MBALIMBALI KWA URATIBU WA:

**MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA,**
S.L.P 105926, DAR ES SALAAM,
TANZANIA

BARUA PEPE: info@thrd.co.tz
SEPTEMBA, 2019 Tanzania
© MUUNGANO WA AZAKI, 2019

# YALIYOMO




ORODHA YA VIFUPISHO VYA MANENO ..... viii

SHUKRANI ..... ix

DIBAJI ..... x

VIPAUMBELE VIKUU VYA AZAKI ..... xi

**SURA YA KWANZA: MAELEZO YA JUMLA ..... 1**

1.1 UTANGULIZI ..... 1

1.1.1 Asili na Mantiki ya Ilani ya Azaki ..... 1

1.1.2 Lengo la Ilani ya Uchaguzi ya Azaki ..... 2

1.2 UHALALI WA AZAKI KUTOA ILANI YA UCHAGUZI ..... 2

1.3 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA ILANI ..... 2

1.4 MUUNDO WA ILANI ..... 3

1.5 SIFA ZA KIONGOZI ANAYEFAA KWA MUJIBU WA ILANI ..... 4

1.6 TUNU ZA TAIFA ..... 4

**SURA YA PILI: ULINZI, USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA HAKI ZA BINAADAM NA UTAWALA BORA ..... 5**

2.1 UTANGULIZI ..... 5

2.2 TATHMINI FUPI YA ILANI ILIYOPITA KUHUSU ULINZI NA USALAMA ..... 5

2.2.1 Mafanikio ..... 5

2.2.2 Mapungufu ..... 5

2.3 TAMKO LA ILANI KUHUSU ULINZI NA USALAMA ..... 6

2.4 UFAFANUZI ZAIDI WA ILANI KUHUSU ULINZI NA USALAMA ..... 6

2.4.1 Uhuru wa Kujieleza ..... 6

2.4.2 Uhuru wa Kukutana na Kujieleza ..... 7

2.4.3 Ushirikishwaji wa Wananchi Katika Mipango na Maamuzi ..... 7

2.4.4 Haki za Makundi Maalum ..... 8

2.4.5 Haki za Kisiasa ..... 9

2.4.6 Utawala wa Kitaasisi ..... 9

**SURA YA TATU: UKATIBA NA UTAWALA WA SHERIA ........................................ 11**

3.1 UTANGULIZI ........ 11
3.2 TATHMINI FUPI YA ILANI ILIYOPITA KUHUSU UKATIBA NA SHERIA ........ 11
3.2.1 Mafanikio ........ 11
3.2.2 Mapungufu ........ 11
3.3 HALI YA USIMAMiZI NA ULINZI WA KATIBA YA SASA ........ 12
3.4 TAMKO LA ILANI KUHUSU UTEKELEZAJI WA KATIBA ........ 12
3.5 UFAFANUZI ZAIDI WA ILANI KUHUSU UTEKELEZAJI WA KATIBA ........ 12
3.5.1 Utawala Washeria ........ 12
3.5.2 Mgawanyo wa Madaraka ........ 13

**SURA YA NNE: UCHUMI JUMUISHI NA ENDELEVU ........................................ 15**

4.1 UTANGULIZI ........ 15
4.2 MAANA NA MANTIKI YA UCHUMI JUMUISHI ........ 15
4.3 TATHMINI FUPI YA ILANI ILIYOPITA KUHUSU UCHUMI JUMUISHI ........ 16
4.3.1 Mafanikio ........ 16
4.3.2 Mapungufu ........ 16
4.4 TAMKO LA ILANI KUHUSU UCHUMI JUMUISHI ........ 16
4.5 UFAFANUZI ZAIDI WA ILANI KUHUSU UCHUMI ........ 17
4.5.1 Uchumi Endelevu – Hali Ilivyo Kwa Sasa ........ 17
4.5.2 Dira na Mpango wa Maendeleo yaTaifa na Uchumi wa Tanzania ........ 19
4.5.3 Ajira na Ustawi wa Jamii ........ 20
4.5.4 Usalama wa Mali ........ 21

**SURA YA TANO: ULINZI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA ............... 22**

5.1 UTANGULIZI ........ 22
5.2 TATHMINI YA HALI HALISI NA UTEKELEZAJI WA ILANI YA AWALI ........ 22
5.3 MADAI YA ILANI YA AZAKI ........ 23
5.4 UFAFANUZI ZAIDI KUHUSU USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA ........ 23
5.4.1 Usimamizi wa Rasilimali ........ 23
5.4.2 Ushiriki wa Raia ........ 24
5.4.3 Uwajibikaji wa Makampuni Kwa Jamii ........ 25
5.4.4 Usimamizi wa Mapato Maliasili na Rasilimali za Nchi ........ 25
5.4.5 Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi ........ 26

**SURA YA SITA: USAWA WA KIJINSIA NA MAKUNDI MAALUM........................ 28**

6.1 UTANGULIZI ....28
6.2 JITIHADA ZA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA KIJINSIA ....28
6.3 TAMKO LA ILANI KUHUSU USAWA WA KIJINSIA....28
6.4 HAKI ZA MAKUNDI MAALUM....29
6.4.1 Ufafanuzi – Hali Halisi ya Makundi Maalumu....29
6.4.2 Watu Wenye Ulemavu....30
6.4.3 Uwezeshaji wa Wanawake ....30
6.4.4 Maendeleo ya Vijana ....31
6.4.5 Ulinzi na Ustawi wa Wazee....32
6.4.6 Ulinzi na Ustawi wa Watoto ....33
6.4.7 Maendeleo ya Wakulima, Wafugaji wa Asili na Waokota Matunda....33

**SURA YA SABA: UPATIKANAJI NA UNAFUU WA HUDUMA ZA MSINGI ZA KIJAMII.................................................................................................... 35**

7.1 UTANGULIZI ....35
7.2 TATHMINI FUPI KUHUSU UPATIKANAJI NA UNAFUU WA HUDUMA....35
7.3 UFAFANUZI WA ILANI KUHUSU UPATIKANAJI NA UNAFUU WA HUDUMA....36
7.3.1 Upatikanaji wa Huduma ya Elimu....36
7.3.2 Upatikanaji na Unafuu wa Huduma za Afya....37
7.3.3 Upatikanaji na Unafuu wa Huduma za Maji Safi na Salama ....39

**SURA YA NANE: AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO WA TAIFA ... 41**

8.1 UTANGULIZI ....41
8.2 MWENENDO WA AMANI, USALAMA NA UMOJA WA KITAIFA ....41
8.3 UFAFANUZI ZAIDI KUHUSU AMANI, USALAMA NA UMOJA....42
8.3.1 Amani Katika Taifa ....42
8.3.2 Usalama Katika Taifa ....42
8.3.3 Tamko la Ilani Kuhusu Amani, Usalama, Umoja na Mshikamano....43

**SURA YA TISA: TANZANIA NA DIPLOMASIA YA KIKANDA NA KIMATAIFA .... 44**

9.1 UTANGULIZI ....44
9.2 SERA MPYA YA MAMBO YA NJE YA TANZANIA ....44
9.3 MUELEKEO WA KUNUFAIKA KUPITIA DIPLOMASIA YA UCHUMI ....45
9.4 UWAKILISHI WA NCHI KATIKA MIKUTANO YA KIKANDA NA KIMATAIFA....45
9.5 UTEKELEZAJI WA MAKUBALIANO NA MIKATABA YA KIMATAIFA ....46
9.6 TAMKO LA ILANI KUHUSU DIPLOMASIA....46

**SURA YA KUMI: UHURU WA KUJIELEZA, KUJUMUIKA NA KUKUTANA .......... 47**

10.1 UTANGULIZI ........ 47
10.2 UHURU WA KUTETEA, KUDAI NA KULINDA HAKI ZA BINADAMU ........ 47
10.2.1 Hali ilivyo kwa sasa kuhusu Uhuru wa Azaki ........ 47
10.2.2 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kudai Haki, Kutetea na Kulinda Haki za Binadamu ........ 48
10.3 UHURU WA KUTOA MAONI NA KUSHAURI ........ 48
10.3.1 Hali ya Uhuru wa Kutoa Maoni na Kushauri ........ 48
10.3.2 Jitihada Zilizochukuliwa Kumaliza Tatizo Hili ........ 49
10.3.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kutoa Maoni Mbalimbali ........ 49
10.4 UHURU WA KUJUMUIKA NA KUFANYA SHUGHULI ZA KIRAIA NA KISIASA ........ 50
10.4.1 Hali ya Uhuru wa Kujumuika na Kufanya Shughuli za Kiraia na Kisiasa ........ 50
10.4.2 Jitihada Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto Hizo ........ 50
10.4.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kujumuika ........ 51
10.5 UHURU WA KUFANYA TAFITI NA KUTOA TAARIFA MBADALA ........ 51
10.5.1 Hali ya Uhuru wa Kufanya Tafiti na Kutoa Taarifa Mbadala ........ 51
10.5.2 Jitihada Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto Hii ........ 51
10.5.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kufanya Tafiti na Kutoa Taarifa Mbadala ........ 51
10.6 MASUALA MENGINE KIUJUMLA ........ 52

**SURA YA KUMI NA MOJA: UWEKEZAJI NA ULINZI WA MATUMIZI YA TEHAMA...53**


11.1 UTANGULIZI ........ 53
11.2 BAADHI YA FAIDA YA TEHAMA KWA JAMII ........ 53
11.3 TAMKO LA ILANI KUHUSU TEHAMA KIUJUMLA ........ 54
11.4 UHURU NA ULINZI WA MATUMIZI YA TEHAMA ........ 54
11.4.1 Hali Ilivyo Sasa ........ 54
11.4.2 Tamko la Ilani Kuhusu Ulinzi na Matumizi ya TEHAMA ........ 54
11.5 UPATIKANAJI NA UNAFUU WA GHARAMA ZA MATUMIZI YA TEHAMA ........ 55
11.5.1 Hali Ilivyo kwa Sasa Kuhusu Unafuu wa Gharama ........ 55
11.5.2 Tamko la Ilani Kuhusu Unafuu wa Gharama ........ 55

**SURA YA KUMI NA MBILI: WITO KWA WADAU KIUJUMLA .............................. 56**

12.1 UTANGULIZI ........................................................................ 56
12.2 WITO KWA WADAU MBALIMBALI ................................................ 56
12.2.1 Kwa Wananchi ........................................................................ 56
12.2.2 Kwa Vyama vya Siasa ............................................................ 56
12.2.3 Kwa Wagombea ........................................................................ 56
12.2.4 Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi (Tume za Uchaguzi (NEC na ZEC) na TAMISEMI ........ 57
12.2.5 Vyombo vya Ulinzi na Usalama ................................................ 58
12.2.6 Wadau wa Kimataifa ................................................................ 58
12.2.7 Watumishi wa Umma ................................................................ 58
12.2.8 Vyombo vya Habari .................................................................. 58
12.2.9 Viongozi wa Dini ...................................................................... 59
12.2.10 Asasi za Kiraia (AZAKI) ........................................................ 59
12.2.11 Serikali ya JMT na SMZ ........................................................ 59
12.2.12 Msajili wa Vyama Vya Siasa: .................................................. 59


**SURA YA KUMI NA TATU: HITIMISHO ................................................ 60**

# ORODHA YA VIFUPISHO VYA MANENO



| | |
|---|---|
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| AZISE | Asasi Zisizo za Kiserikali |
| COMESA | Jumuiya ya Soko la Pamoja Kusini mwa Afrika |
| CORDS | Shirika la Utafiti wa Jamii na Huduma za Kimaendeleo |
| Dkt | Usomi wa Shahada ya Uzamivu |
| EAC | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| EIA | Tathmini ya Athari za Kimazingira |
| GePG | Mfumo wa  Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali |
| IRCPT | Baraza la Dini Mbalimbali kwa ujenzi wa Amani Tanzania |
| JMT | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| LEAT | Shirika la Wanasheria wa Mazingira Tanzania |
| LHRC | Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu |
| MCH | Huduma ya Afya kwa Mama na Mtoto |
| MTAKUWA | Mpango wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto |
| NBS | Idara ya Taifa ya Takwimu |
| NEEC | Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| NEMC | Baraza la Usimamizi wa Mazingira |
| OJADACT | Chama cha Waandishi wa Habari Wa Kupiga Vita Matumizi Ya Dawa Za Kulevya Na Uhalifu Tanzania |
| PLAJC | Kituo cha Amani, Msaada wa Kisheria na Haki Tanzania |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |
| SAHRiNGON | Mtandao wa Asasi za Haki za Binadamu Kusini mwa Afrika |
| SDGs | Malengo ya Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa |
| SHIVYAWATA | Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania |
| SIDA | Shirika la Msaada la Swideni |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| TACCEO | Mtandao wa Asasi za Kiraia wa Uangalizi wa Uchaguzi |
| TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANLAP | Mtandao wa Mashirika ya Msaada wa Kisheria Tanzania |
| TASAF | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEITI | Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Madini Tanzania |
| TGNP | Mtandao wa Kijinsia Tanzania |
| THRDC | Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu |
| TIB | Benki ya Uwekezaji |
| TRA | Mamlaka ya Mapato ya Tanzania |
| UCSAF | Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote |
| WAHAMAZA | Chama cha Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar |
| WiLDAF | Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika |
| YPC | Ushirikiano wa Vijana Nchini |
| ZAFAYCO | Shirika linalopambana dhidi ya Changamoto za Vijana Zanzibar |
| ZLSC | Kituo cha Msaada wa Sheria Zanzibar |

# SHUKRANI



Kwa namna ya kipekee, tunapenda kutoa shukrani zetu kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kwa kukubali kuratibu shughuli nzima ya upatikanaji wa ilani hii katika hatua zake zote. Tunawashukuru wawakilishi kutoka AZAKI zaidi ya 90 nchi nzima waliyojitokeza katika mkutano wa kwanza uliofanyika tarehe 4 Julai 2019 jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mapitio ya ilani ya Uchaguzi ya AZAKI ya mwaka 2015 na kupendekeza wajumbe kutoka mashirika 15 walioandika ilani hii. Pia shukrani zetu ziwaendee wajumbe wa timu maalum ya wanaAZAKI kutoka asasi zifuatazo ANGOZA, TCIB, TACCEO, SHIVYAWATA, TGNP, THRDC, HAKIRASILIMALI, LEAT, SAHRiNGON, MWANAMKE NA UONGOZI, RESTLESS DEVELOPMENT, PLAJC, DOOR OF HOPE TANZANIA, YPC na WAHAMAZA, walioshiriki katika uandishi wa Ilani hii.


Aidha, tunawashukuru wote waliojitoa kuweza kupitia na kuhariri kazi hii. Kwa namna ya kipekee tunawashukuru Dr. Helen Kijo-Bisimba (Mkurugenzi mstaafu wa LHRC); Prof. Prosper Ngowi (Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Mzumbe); Wakili Clarence Kipobota (Mshauri, Ledeco Consultants); na, Mr. Nazar Nicolas kutoka shirika la Internet Society kwa kufanya uhariri wa Ilani hii.

Pia tunayashukuru mashirika ya ZLSC, TANLAP, HAKIMADINI, WILDAF, CORDS, HAKIELIMU, IRCPT, ZAFAYCO na OJADACT kwa kushiriki katika kuiboresha kazi hii.

Vile vile, wapo waliowezesha gharama za kuendesha mikutano ya wana AZAKI tangu mwanzo hadi kupatikana kwa ilani hii. Pamoja nao, tunapenda kuwashukuru SIDA na OXFAM TANZANIA ambao walichangia gharama za awali katika kufanikisha kazi hii.

Tunatoa shukrani zetu pia kwa FREEDOM HOUSE na PACT TANZANIA kwa kujitolea kubeba gharama zote zilizobaki ili kuhakikisha malengo ya Ilani hii yanafika kwa wadau wote na kwa wakati.

# DIBAJI



Asasi za Kiraia (AZAKI) zilianzishwa nchini miaka mingi iliyopita. Kwa mfano, historia inaonyesha kuwa, AZAKI zilihusika kwa kiasi kikubwa katika harakati za kupigania uhuru wa taifa letu la Tanzania. Baada ya uhuru, AZAKI ziliendelea kusaidia katika mambo muhimu yenye maslahi ya taifa hasa kuanzia miaka ya 1990.

Kwa muktadha wa Ilani hii, AZAKI maana yake ni asasi zote zisizo za kiserikali (AZISE); jumuiya za kijamii; taasisi za kidini; vyama mbalimbali visivyo vya kisiasa ikiwa ni pamoja na vyama vya wafanyakazi, taasisi za kitaaluma na vyombo vya habari.

Kwa muda wote, takribani miaka 30 tangu 1990, asasi zimekuwa zikitoa mchango muhimu katika upatikanaji na utetezi wa haki za kijamii; utoaji wa huduma za kijamii kama vile elimu na afya; na, maendeleo ya nchi kwa ujumla. Mafanikio haya yametokana na kuimarika kwa uhusiano baina ya asasi hizi pamoja na vyombo vya maamuzi kama Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Bunge.

AZAKI zimekuwa muhimili muhimu kwenye kuhimiza maendeleo ya jamii, kupitia miradi mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha vijana na wanawake kiuchumi na kutoa huduma za maendeleo ya jamii kwa kutumia gharama nafuu na hata muda mwingine kwa kutumia rasilimali za wanaojitolea. Pia, utoaji wa elimu bure ya afya, mapambano ya magonjwa ambukizi, mila na desturi zenye madhara kwa vijana na watoto. Kuna asasi zinazowezesha vijana kuwekeza kiuchumi katika miradi midogomidogo ya uzalishaji mali.

AZAKI zilizohusika na uandaaji wa Ilani hii zote zimesajiliwa chini ya sheria za Tanzania na zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria mbalimbali. Aidha, asasi hizi zina haki na zinatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Moja ya majukumu makuu ya AZAKI yamekuwa ni kusimamia utekelezaji wa haki za kikatiba; utawala wa sheria; utetezi wa haki za binadamu; na, masuala yote ya kimaendeleo ili kuhakikisha, kati ya mambo mengine, maisha ya mtanzania yanakuwa bora katika nyanja zote na taifa la Tanzania linaendelea kwa manufaa ya watu wake.

Kwa kuwa nchi yetu inaelekea katika vipindi vya uchaguzi wa Serikali za Mitaa (SM) mwaka huu 2019 na uchaguzi mkuu mwaka 2020, AZAKI, kwa umoja huu, zimeonelea ni busara kuchangia katika mchakato wa chaguzi hizo zote mbili kwa kukuza uelewa wa haki za kiraia, kidemokrasia na upigaji kura; na pia, kubainisha masuala yenye tija kwa taifa ambayo ni muhimu kuakisiwa na kutiliwa maanani wakati wa mchakato wa chaguzi hizo na vilevile viongozi watakaochaguliwa katika nafasi mbalimbali.


Ubainishaji wa masuala haya kama vipaumbele vya kuzingatiwa umefanyika kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na (i) uzoefu wa AZAKI katika kuhudumia jamii nchi nzima; (ii) tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya AZAKI ya 2015; na, (iii) hali halisi ya sasa ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na mambo mengine kama hayo.

Serikali kupitia sera, sheria na matamko ya viongozi mbalimbali imekiri kutambua na kuthamini juhudi na mchango wa AZAKI kwa maendeleo ya nyanja mbalimbali. Hili ni jambo jema na kuwa AZAKI inaahidi kushirikiana na serikali na wadau wengine kwa upana zaidi, ikiwa ni pamoja na kutumia njia ya kutoa mawazo juu ya masuala ya msingi ya kuzingatia wakati wa uchaguzi na katika mipango ya mbeleni.

Ilani hii ya AZAKI inanuwiwa kuwa mwongozo kwa wadau mbalimbali wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na Serikali, vyama vya siasa, wangombea nafasi mbalimbali za uchaguzi na hata wapiga kura au wananchi wengine katika kupanga, kusimamia, kutekeleza na kutathmini mipango na vipaumbele vya kitaifa. Hivyo, wadau wote wanashauriwa kuitumia Ilani hii kwa mantiki hiyo.

**AZAKI za Tanzania**
Septemba 2019
Tanzania

# VIPAUMBELE VIKUU VYA AZAKI



**(i) Ulinzi, Usimamizi wa Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Jukumu la ulinzi na usalama wa raia na mali ni jukumu la Serikali kupitia vyombo vyake mbali mbali vya usalama. Halikadhalika, usimamizi wa haki za binadamu na utawala bora ni jukumu la serikali. AZAKI huwa zinatekeleza jukumu hili kuisaidia serikali husika. Hivyo basi, sisi kwa niaba ya taifa letu tunahitaji kuona viongozi watakaosimamia kipaumbele hiki haswa katika kipindi hiki ambacho suala la usalama wa watu na mali zao ni tatizo. Pia kumekuwa na uvunjifu mkubwa wa haki za binadamu. Tunataka viongozi watakaosimamia misingi ya haki za binadamu kulingana na mikataba mbali mbali ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu Tanzania imeridhia.

**(ii) Ukatiba na Utawala wa Sheria**

Katiba ndiyo sheria mama ya nchi. Sheria zingine zote zinatokana na Katiba ya nchi. Tunataka kiongozi atakayeweza kuilinda, kuitetea na kuiheshimu Katiba ya nchi. Kiongozi huyo ni lazima awe tayari kufwata sheria kama zilivyo na sio kuwa juu ya sheria. Tunataka kiongozi anayeamini kwamba Sheria kwa misingi yake hazina macho na hivyo yeyote anayekwenda kinyume na sheria zetu ni lazima awajibishwe kwa mujibu wa sheria.

**(iii) Uchumi Jumuishi na Endelevu**

Dhana ya uchumi jumuishi na endelevu inatekelezeka pale ambapo shughuli za kiuchumi zinamlenga kila mtu kwa nafasi yake katika jamii. Tunataka kiongozi atakayesimamia uchumi ambao utamnufaisha kila mtanzania kwa namna moja ama nyingine.

**(iv) Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Umma**

Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizobarikiwa kuwa na rasilimali ambazo ni ardhi, madini, gesi asilia, mafuta, bahari, maziwa, mito, wanyama pori na misitu asilia. Katika miaka ya hivi karibuni ulinzi thabiti wa rasilimali za nchi hususani kwa mamlaka husika umeonekana kuongezeka ukilinganisha na miaka 10 ya nyuma. Upotevu na ubadhirifu wa rasilimali za nchi umedhibitiwa. Aidha, bado tunaendelea kuona viongozi wakiingia mikataba ya uwekezaji na uvunaji wa rasilimali isiyo na tija kwa taifa. Tunawataka viongozi wote wenye kuwania nafasi za uongozi kutamka bila kificho namna watakavyoendeleza usimamizi mzuri na ulinzi thabiti wa rasilimali za nchi ili ziendelee kutumika kwa manufaa ya Taifa na watu wake.

**(v) Usawa wa Kijinsia na Makundi maalum**

Katiba yetu inatambua kuwa raia wote ni sawa. Maamuzi yeyote yanayomlenga au kumuathiri mwananchi ni lazima mwananchi huyo ashirikishwe bila kujali tofauti ya jinsia, hali, na kadhalika. Makundi maalumu yana nafasi na mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa letu. Hivyo ni lazima viongozi watakaochaguliwa wabebe dhana ya kwamba hakuna maamuzi yanayoweza kupitishwa juu ya wananchi bila kuwashirikisha wananchi. Pia tunawataka viongozi waatakaohakikisha nafasi za maamuzi zinakuwa na usawa wa kijinsia ili kufikia lengo la 50/50.





**(vi) Upatikanaji na Unafuu wa Huduma za kijamii**

Changamoto kubwa tuliyonayo kama taifa ni upatikanaji na unafuu wa huduma za kijamii kama vile umeme, maji, huduma za dawa/afya, elimu, miundombinu nk. Tunataka viongozi watakaoweza kusimama kwa dhati na kusimamia kero za huduma za jamii bila ubaguzi. Hili litawezekana endapo rushwa, matumizi mabaya ya madaraka, matumizi sahihi ya rasilimali za nchi, utulivu wa wateule katika taasisi, ukabila vitapigwa vita kwa vitendo na sio maneno.

**(vii) Amani, Usalama na Mshikamano wa Kimataifa**

Kamwe maendeleo hayawezi kupatikana katika nchi yenye machafuko. Amani na mshikamano visipotawala, nchi itaharibika kwa machafuko. Tunahitaji viongozi watakaoweza kudumisha amani tuliyonayo na kuendelea kuilinda na kujenga taswira nzuri ya nchi yetu kimataifa.

**(viii) Tanzania na Diplomasia ya Kikanda na Kimataifa**

Ikumbukwe kwamba, uhusiano mzuri baina ya nchi na nchi ni chachu ya maendeleo, ulinzi, heshima, na kuaminiana. Nchi isiyokuwa na mahusiano mazuri na nchi nyingine mara nyingi nchi hiyo huishia kuwekewa vikwazo, na pengine kutengwa kabisa. Tunahitaji kiongozi anayeamini katika diplomasia safi, ujirani mwema, utekelezaji wa mikataba mbali mbali ya kikanda na kimataifa kwa nia njema.

**(ix) Uhuru wa Kujieleza, Kujumuika na Kukutana**

Haki ya uhuru wa kujumuika, kujieleza, na kukutana ni haki zilizopo kikatiba. Kama wana AZAKI tunaamini kwamba haki ya kujieleza ndio haki ya kwanza na ya msingi kuliko haki zingine, kwakuwa endapo mtu hana uhuru wa kujieleza basi ni ngumu kupata haki zingine. Miaka minne iliyopita iligubikwa na ukiukwaji wa haki ya kujieleza huku vyombo vya habari vikifungiwa, sheria kandamizi zimetungwa, mikutano ya kisiasa imepigwa marufuku, AZAKI zimewekewa masharti magumu kisheria, pamoja na changamoto zingine nyingi. Tunataka kiongozi atakayesimamia uhuru wa kujieleza kwanza kwa kufuta sheria kandamizi na zinazominya demokrasia, haki, na utawala bora.

**(x) Uwekezaji na Ulinzi wa Matumizi ya Tehama**

Katika ulimwengu na karne hii ambapo teknolojia inakuwa kwa kasi, taifa linahitaji kuwekeza vilivyo katika uwanda huo. Hata hivyo, ukuaji wa teknolojia unakuja na changamoto zake ambazo zisipowekewa tahadhari na udhibiti zinaweza kuleta madhara makubwa kwa taifa. Tunahitaji kiongozi atayeheshimu na kuwekeza katika teknolojia lakini pia aheshimu uhuru wa mawasiliano ya watu na haki ya faragha kwa kulinda taarifa za watumiaji wa mitandao.



# Sura ya 1

# MAELEZO YA JUMLA

## 1.1 UTANGULIZI

### 1.1.1 Asili na Mantiki ya Ilani ya Azaki

Hii ni Ilani ya pili ya uchaguzi kutolewa na Asasi za Kiraia (AZAKI) ambayo inafuatia Ilani nyingine kama hii toleo la mwaka 2015. Lengo la Ilani ya Uchaguzi ya AZAKI ya 2015 lilikuwa ni kuweka wazi matakwa ya AZAKI juu ya Tanzania Tuitakayo kupitia mchakato wa uchaguzi. Asili yake hasa ni maazimio ya mkutano wa watetezi wa haki za binadamu uliofanyika kwa mara ya kwanza tarehe 24 Julai 2015. Lengo la mkutano ule lilikuwa ni kutathmini nafasi ya AZAKI katika michakato ya kidemokrasia ikiwemo uchaguzi mkuu. Mkutano huo uliazimia pamoja na mambo mengine, kuundwa kwa kikosi kazi kitakachoandaa rasimu ya ilani kwa niaba ya AZAKI mwaka 2015. Ilani ilipatikana na kutumika mwaka huo 2015 na hata baada ya uchaguzi mkuu.

Kama ilivyokuwa katika Ilani ya awali, nia hasa ya Ilani hii ya sasa ya AZAKI ni kutoa mwongozo kuhusu namna mbavyo vyama vya siasa, wagombea wa uchaguzi, Tume za Taifa za Uchaguzi (Zanzibar na Tanzania Bara), vyombo vya usalama, serikali, na wananchi wote kwa ujumla wanatakiwa kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa (SM) wa 2019 na uchaguzi mkuu wa 2020.

Aidha, Ilani hii ya pili ya AZAKI imechagizwa na maazimio ya wawakilishi wa AZAKI kutoka nchi nzima katika mkutano uliofanyika mnamo tarehe 4 Julai 2019. Lengo la mkutano huu wa Julai 2019 ulikuwa ni kufanya tathmini ya Ilani ya AZAKI ya mwaka 2015. Katika mapitio hayo, kuna masuala kadhaa yalijitokeza na kubainishwa kwa mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya AZAKI ya Uchaguzi ya 2015. Masuala hayo yamebainishwa katika Ilani hii. Aidha, kuna changamoto ambazo wana AZAKI walizibaini katika utekelezaji wa Ilani ya awali. Ikaazimiwa ya kwamba, masuala ambayo bado ni changamoto yaingizwe katika Ilani hii kwa kujumuishwa na mengine yaliyojitokeza katika kipindi hiki tokea mwaka 2015.

Kwa kuwa viongozi wa AZAKI za Tanzania wameamua kwa dhati kujenga jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani: wameamua kuandika Ilani hii kwa niaba ya Wananchi, kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu unafanyika kwa kuzingatia sheria na matakwa ya wananchi, na pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia na utawala bora.

### 1.1.2 Lengo la Ilani ya Uchaguzi ya Azaki

Ilani hii ni matakwa ya AZAKI kuelekea na baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2019 na uchaguzi mkuu wa 2020 kuhusu Tanzania Tuitakayo.

Ilani hii imekusudiwa kutoa mwongozo kwa serikali, vyama vya siasa, wagombea wa nafasi mbalimbali za kisiasa wakati wa uchaguzi, wapiga kura na viongozi watakaoshinda chaguzi ili kutambua vipaumbele vya kisheria, kijamii, kidemokrasia na kadhalika katika kutekeleza wajibu wao kwa manufaa ya taifa na watu wake wote.

> *Demokrasia ni mfumo wa serikali ambapo wananchi wote ni sawa mbele ya sheria na wanashiriki katika kufanya maamuzi ya kitaifa juu ya masuala ya umma. Wakati mwingine wananchi hushiriki moja kwa moja. Hii ina maana kwamba, wao hupiga kura moja kwa moja kwenye masuala kama vile sheria na katika chaguzi na pia huwakilishwa na viongozi wao waliowachagua. Ni utawala wa watu na watawala hutawala kwa ridhaa ya watu.*

Aidha, wadau wote wa uchaguzi wanashauriwa watumie Ilani hii kama mwongozo kwa lengo la kufanikisha uchaguzi kuwa huru, haki na wenye kuzingatia sheria na Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

## 1.2 UHALALI WA AZAKI KUTOA ILANI YA UCHAGUZI

AZAKI zote ambazo ni sehemu ya uandaaji wa Ilani hii zimesajiliwa kisheria na zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu mbalimbali za JMT. Aidha, kama taasisi huru kisheria, AZAKI zinawajibu wa kushiriki katika shughuli na maamuzi ya umma kwa mujibu wa Katiba ya JMT ya 1977. Kufanya yote haya pia ni haki ya kidemokrasia kwa AZAKI na wananchi wote.

> *Japo jamii ya kitanzania ina masuala mengi sana ambayo ni vipaumbele kwao, Ilani hii imeakisi yale ambayo ni muhimu na ya kimkakati siyo tu kwa ustawi wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT), bali pia, taifa zima la JMT. Ubainishaji wa mahitaji hayo umefanyika kwa ustadi mkubwa hasa kwa kuzingatia uzoefu wa AZAKI wa ufanyaji kazi na jamii kila sehemu hapa nchini.*

Ibara ya 8 ya Katiba ya JMT ya 1977 inatilia mkazo suala la demokrasia. Ibara hiyo inabainisha ya kwamba (nukuu):

> *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii. Serikali itawajibika kwa wananchi, wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.*

Kwa hivyo, ni muafaka kwa wana AZAKI kushiriki katika mchakato wa uchaguzi kwa njia hii na nyinginezo kama haki na wajibu wetu kwa pamoja.

## 1.3 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA ILANI

Kwa mujibu wa tathmini ya AZAKI, imebainika na kuonekana kuwa, katika kipindi cha miaka minne iliyopita serikali ya JMT kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa na AZAKI, imetekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni pamoja na (baadhi tu kwa hapa):-

(i) Kuendelea kwa hali ya amani na utulivu nchini.

(ii) Uboreshaji wa elimu kwa kuakisi hali ya watu wa kipato kidogo. Mfano utekelezaji wa sera (maagizo) ya elimu bure kwa shule za msingi na sekondari za umma.

(iii) Uboreshaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na kujenga au kupanua vituo vya afya sehemu mbalimbali hapa nchini.

(iv) Ulinzi na usimamizi mzuri wa rasilimali za umma.

(v) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali.

(vi) Kuziba mianya ya ufujaji wa fedha na mapato mengine ya umma.

(vii) Uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya kiuchumi kwa ufanisi wa hali ya kuridhisha (tofauti na miaka mingine). Miradi hii ya kimkakati kiuchumi ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, upanuzi wa uwanja mkubwa wa ndege wa Dar es Salaam na ununuzi wa ndege na kuanzisha safari nje ya nchi.

(viii) Utekelezaji wa mipango mikubwa ya kiutawala na kisheria ikiwa ni pamoja na kuhamishia serikali Dodoma, kurahisisha upatikanaji wa hati miliki za ardhi, kuanzisha Mahakama Kuu kitengo cha Makosa ya rushwa na Uhujumu Uchumi, kuimarisha utendaji kazi wa vyombo vya kisheria na kadhalika.

(ix) Utekelezaji mkubwa wa dhima ya Tanzania ya Viwanda.

Hata hivyo, katika utekelezaji huo, mapungufu kadhaa yameonekana. Mapungufu hayo ni pamoja na utungwaji wa sheria kandamizi dhidi ya baadhi ya haki za msingi za binadamu; na, baadhi ya maamuzi ya kiutawala mfano agizo la kutoruhusu mwanafunzi kurudi shuleni baada ya kujifungua. Aidha, serikali kusitisha na kuamua kutoendelea na mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya ya JMT.

Baadhi ya changamoto nyingine, kama ambavyo imefafanuliwa zaidi katika Ilani hii ni ongezeko kubwa la matukio ya ukikwaji wa haki za binadamu na demokrasia nchini; kupungua kwa uhuru wa kujieleza; kubinywa kwa haki za kisiasa; na, kudhibiti uhuru wa kujumuika na kufanya kazi za utetezi nchini.

### 1.4 MUUNDO WA ILANI

Kimuundo Ilani hii imezingatia sura zilizowekwa kulingana na vipaumbele vya AZAKI. AZAKI zimeazimia ya kwamba, vifuatavyo ndiyo vipaumbele vya masuala ya kuzingatia katika kipindi hiki cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2019 na uchaguzi mkuu wa 2020. Vipaumbele vikuu ni masuala ya:-

(i) Ulinzi, usalama na utekelezaji wa haki za binadamu na utawala bora.
(ii) Ukatiba na utawala wa sheria.
(iii) Uchumi jumuishi na endelevu.
(iv) Ulinzi na usimamizi wa rasilimali za umma.
(v) Usawa wa kijinsia na makundi maalum.
(vi) Upatikanaji na unafuu wa huduma za kijamii.
(vii) Amani, usalama na mshikamano wa kimataifa.
(viii) Tanzania na diplomasia ya kikanda na kimataifa.
(ix) Uhuru wa kujieleza, kujuika na kukutana.
(x) Uwekezaji na ulinzi wa matumizi ya TEHAMA.

Vipaumbele vyote hivyo vimefafanuliwa kwa undani katika sehemu zinazofuata za Ilani hii. Kila kipaumbele kimefafanuliwa na Sura ya Ilani hii. Ukijumuisha na sura ya utangulizi, Ilani hii ina jumla ya sura kumi na tatu. Uchaguzi wa sura hizo umezingatia masuala mbalimbali kama ilivyobainishwa hapo juu. Aidha, aina zote za haki za binadamu na misingi ya utawara bora vimezingatiwa.

### 1.5 SIFA ZA KIONGOZI ANAYEFAA KWA MUJIBU WA ILANI

Ili wapiga kura waweze kuchagua kiongozi atakayeweza kusimamia maendeleo ya nchi na kuhakikisha amani ya nchi inazidi kudumu, haina budi kuwa na vigezo vya kiongozi bora. Vigezo hivyo ndiyo dira inayoongoza asasi zote na wananchi kwa ujumla kuwapigia kura wanaotafuta ridhaa ya kuingia madarakani.

Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu huo na pasipo kuathiri masharti ya kisheria ya jambo hili, inapendekezwa ya kwamba, kiongozi anayefaa kuiongoza Tanzania Tuitakayo ni:-

(i) Mtetezi, mlinzi na msimamizi wa Katiba na haki za binadamu. Hii ni sifa kuu kwa kiongozi yeyote yule kuanzia ngazi za chini za serikali mpaka ngazi za juu.

(ii) Awe na utashi na busara za kiuongozi na asiyekubali kupitisha na kusimamia sheria mbaya ikiwa ni pamoja na zile zenye kukandamiza haki za binadamu.

(iii) Ni muwazi katika utendaji kazi wa serikali na anayethamini ushirikishwaji wa wananchi katika mipango ya umma kwa maendeleo ya taifa.

(iv) Ni muwajibikaji na aliye tayari kufanya maamuzi yenye tija kwa taifa pamoja na kuwawajibisha viongozi wengine wa umma wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao bila kuvunja sheria za nchi.

(v) Ni mwadilifu, asiyetoa wala kupokea rushwa, mzalendo kwa nchi yake na aliye tayari kuondoa mifumo ya rushwa na ubadhirifu nchini.

(vi) Ni mahiri katika kusimamia na kulinda rasilimali za nchi yetu ikiwemo kupinga mikataba ambayo haina tija kwa nchi yetu.

(vii) Kiongozi anaye amini kwa dhati katika misingi ya usawa wa kijinsia kwa mapana yake.

(viii) Ni mbunifu mzuri , asiye kaa na kusubiri maelekezo toka juu na asiye yumbishwa kwa kufuata maelekezo kutoka kwa yeyote yasiyo zingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania.

### 1.6 TUNU ZA TAIFA

Katika uchaguzi wa JMT, kunahitajika viongozi watakaoenzi na kuzingatia tunu nne za taifa, ambazo ni:-

(i) Lugha ya Kiswahili.
(ii) Muungano.
(iii) Utu na udugu.
(iv) Amani na utulivu.



Sura ya 3

# ULINZI, USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA HAKI ZA BINAADAM NA UTAWALA BORA

## 2.1 UTANGULIZI

Jukumu la ulinzi na usalama wa raia na mali ni majukumu ya kisheria ambapo, serikali kupitia vyombo vyake na mifumo yake ya kiutendaji, ina jukumu la awali kabisa kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuendelezwa kwa mujibu wa sheria za nchi (zisizokandamizi) na mikataba au maazimio ya kikanda pamoja nay a kimataifa. Halikadhalika, usimamizi, utekelezaji na uendelezaji wa haki za binadamu na utawala bora ni jukumu la serikali. AZAKI huwa zinatekeleza jukumu hili kama sehemu ya kuisaidia serikali.

## 2.2 TATHMINI FUPI YA ILANI ILIYOPITA KUHUSU ULINZI NA USALAMA

### 2.2.1 Mafanikio

Serikali ya JMT na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zinatambua umuhimu wa kulinda, kusimamia haki na kuimarisha utawala bora na umoja wa kitaifa. Katika kipindi kilichopita, pande zote mbili za JMT zimeweza kusimamia vizuri maendeleo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kifedha na kiutawala kwa lengo la kuweka mazingira ya kuimarisha ukuaji wa uchumi na huduma za jamii. Baadhi ya maendeleo makubwa yanayoshuhudiwa ni pamoja na mabadiliko katika utumishi wa umma (kuimarisha uwajibikaji), SM, usimamizi wa fedha za umma na maboresho ya mifumo ya usiamizi wa sheria mbalimbali. Aidha, hakujawa na hatari yeyote kubwa dhidi ya JMT.

### 2.2.2 Mapungufu

Hatahivyo, pamoja na jitihada zilizocuhukuliwa katika kulinda na kusimamia utawala bora na haki za binadamu bado yapo maeneo ambayo yanalalamikiwa kutokana na mapungufu. Miongoni mwa maeneo hayo ni kuwepo kwa rushwa na uhujumu uchumi; na, kuwepo utaratibu wa kufanya maamuzi yenye usumbufu na kupelekea kuathiri haki za binadamu. Mfano, maamuzi ya bomoabomoa nyumba za watu pasipo kuwapatia fidia eneo la kando ya barabara ya Ubungo-Kimara kwa hoja kuwa, ni wavamizi wa eneo hilo.

Aidha, vyombo vya dola, hasa Polisi, utendaji wake umelalamikiwa na baadhi ya wanasiasa kuwa ni wa kiupendeleo hasa katika kuruhusu na kuzuia mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa. Ongezeko la uhitaji wa kipato na ugumu wa maisha, vimechangia kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu vikijumuisha vijana wadogo na familia masikini mfano utumikaji wa kingono na usafirishaji haramu wa binadamu.

Vilevile, hali inaonyesha kuwa, kuna udhoofu wa usimamizi na kuheshimu misingi ya utawala bora. Kwa mfano, kumekuwa na matumizi mabaya ya madaraka ya kisheria kwa baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya hasa Tanzania Bara. Haki za kupata habari na kutoa maoni nazo zimebinywa kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, kuna hali ya kutia shaka ya kufungiwa kwa vyombo vya habari na kupotea kwa wanahabari. Aidha, kuzuia matangazo ya Bunge kuwa mubashara ni ishara ya kupungua kwa uhuru huo.

Vitendo vya mauaji na utekaji vinavyofanywa na 'watu wasiojulikana' vimeongezeka katika kipindi hili bila ufumbuzi wa kueleweka. Uhuru wa kujumuika na kufanya kazi wa AZAKI umebanwa sana katika kipindi hiki kupitia kutungwa na kusimamiwa kwa sheria na kanuni mbalimbali ndani ya miaka hii minne.

**2.3 TAMKO LA ILANI KUHUSU ULINZI NA USALAMA**

Kwa kuwa masuala ya ulinzi, usalama, haki za binadamu na utawara bora ni nguzo muhimu sana ya maendeleo jamii nzima na taifa, hivyo basi:-

(i) AZAKI kwa niaba ya taifa letu tunahitaji kuona viongozi watakaosimamia kipaumbele hiki haswa katika kipindi hiki ambacho suala la usalama wa watu na mali zao ni tatizo.

(ii) AZAKI tunataka viongozi wajao wawe ni wale watakaosimamia misingi ya haki za binadamu na utawara bora kulingana na mikataba mbali mbali ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu Tanzania imeridhia.

(iii) Aidha, AZAKI tunataka viongozi watakao chaguliwa wahakikishe kwamba masuala ya ulinzi, na usimamizi wa haki za binaadamu, demokrasia na utawala bora yanafanyiwa kazi kwa kufuata misingi ya katiba, na sheria katika serikali zote mbili ya JMT na SMZ ili kukuza uwajibikaji, ufanisi na tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

(iv) Vilevile, suala la umaliziaji wa mchakato wa Katiba mpya litiliwe mkazo na viongozi wote watakaochaguliwa.

**2.4 UFAFANUZI ZAIDI WA ILANI KUHUSU ULINZI NA USALAMA**

**2.4.1 Uhuru wa Kujieleza**

**2.4.1.1 Hali Ilivyo Sasa**

Katika Ilani iliyopita ya mwaka 2015 imependekeza kuona baada ya uchaguzi Tanzania yenye kuzingatia uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari na kupata habari. Hali ilivyo hivi sasa uhuru wa vyombo vya habari umefinywa ambapo baadhi ya vyombo vya habari vilifungiwa na vengine kutozwa faini kwa kuandika habari ambazo kwa madai ya kwamba zinahatarisha usalama wa taifa. Baadhi ya watu wamewekwa ndani kutokana na kutumia haki yao ya kutoa maoni. Kwa mfano, ripoti za miaka ya hivi karibuni kuhusu hali ya Watetezi wa Haki za Binadamu kwa ujumla zilizotolewa na Mtanzano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa pamoja zinaonyesha uwepo wa watu mbalimbali waliokamatwa na kuwekwa kizuizini mara kadhaa kwa kutoa maoni yao bila kukiuka misingi ya Katiba.

**2.4.1.2 Jitihada Zilizochukuliwa**

Jitihada zimechukuliwa na taasisi za kiraia kudai marekebisho ya vifungu mbali mbali vya sheria ambavyo vinakandamizi uhuru wa kujieleza lakini bado madai yao hayajapewa uzito unaosatahiki. Hata hivyo jitihada zinaendelea, AZAKI zimeendelea kujengea taasisi mbali mbali vikiwemo vyombo vya habari na jamii uelewa juu ya haki na wajibu. Hili limefanyika kwa kushirikisha pia vyombo mbalimbali vya serikali ili kuhakikisha haki ya kujieleza inasimamiwa na kukuzwa.

#### 2.4.1.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kujieleza

Katika Ilani hii tunapenda kuona baada ya uchaguzi JMT ikiwemo Zanzibar inazingatia uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari na wananchi kupata habari bila ya pingamizi. Katika kufanikisha hili sheria zinazo athiri uhuru huo zifayiwe marekebisho mfano sheria ya vyombo vya habari ya Tanzania Bara na ya Zanzibar.

### 2.4.2 Uhuru wa Kukutana na Kujieleza

#### 2.4.2.1 Hali Ilivyo Sasa

Haki ya kujumuika pamoja na raia wengine ni mojawapo ya haki za msingi kwa raia wa Taifa lolote lile. Katika kipindi hiki imeonekana maandamano, mikutano ya hadhara hasa kwa vyama vya upinzani imepigwa marufuku kwa madai ya kuhatarisha amani ingawa mikutano ya chama tawala inaruhusiwa. Hali hii inaonesha kuwepo kwa upendeleo kinyume na matakwa ya katiba na sheria.

#### 2.4.2.2 Jitihada Zilizochukuliwa

AZAKI, vyama vya siasa wananchi na wadau wengine wamejitahidi kapigania kuwepo uhuru wa kukutana na kujieleza lakini bado vilio vyao havijapata kushughulikiwa, ila ukandamizi unazidi kujitokeza kutokana na kufanyia marekibisho ambayo yako kinyume na madai yao. Kwa mfano, AZAKi zimefanya kazi kubwa kukutana na viongozi wa serikali, wabunge na wadau mbalimbali katika taasisi za uma ili kushawishi marekebisho ya sheria na sera zinazokandamiza haki ya kujumuika.

#### 2.4.2.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kukutana na Kujieleza

Ilani hii inawataka viongozi wanaohitaji ridhaa ya kuongoza taifa kupitia uchaguzi wa 2020 kuhakikisha haki hii ya kujumuika na kufanya maandamano inalindwa na kuheshimiwa kama ilivyo elezewa katika Katiba na sheria.

### 2.4.3 Ushirikishwaji wa Wananchi Katika Mipango na Maamuzi

#### 2.4.3.1 Hali Ilivyo Sasa

Mpango wa ushirikishwaji wa wananchi kupitia ugatuzi wa madaraka kutoka katika serikali kuu kwenda kwa wananchi umeweza kufanyika katika serikali zote mbili (JMT na SMZ). Mwaka 2014 Baraza la Wawakilishi lilitunga Sheria ya Serikali za Mitaa Zanzibar ambayo utekelezaji wake ulianza mwaka 2016. Ilipofika mwaka 2017, SMZ ilifanya majaribio kwa kufanya ugatuzi wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda SM ambako ndiko wananchi wako wengi. Ugatuzi huo ulifanyika katika sekta tatu ambazo ni sekta ya afya ya msingi, sekta ya elimu kwa upande wa elimu ya msingi na sekta huduma za ugani katika kilimo.

Michakato muhimu kama ya uandaaji wa bajeti ya taifa ya kila mwaka, bado imekua na changamoto mbalimbali. Pamoja na uwepo wa ushiriki wa wadau mbalimbali wakiwemo wabunge katika upitishaji wa bajeti hizo, bado ushiriki wa wananchi katika uandaaji wa bajeti umekua ni mdogo sana hasa katika ngazi ya SM.

#### 2.4.3.2 Jitihada Zilizochukuliwa

Utekelezaji wa Ugatuzi wa madaraka kwa upande wa Zanzibar ulianza kwa majaribio mwaka 2017 ambao ulionesha muelekeo mzuri. Hata hivyo, kuna changamoto mbalimbali zinazokabili utendaji wamamlaka ya serikali za mitaa hadi serikali kuu katika serikali zote mbili. Hadi sasa mamlaka ya wananchi katika vyombo

vilivyoanzishwa yakiwemo baraza la kata na kamati za ushauri za Shehia hayaonekani (Zanzibar). Haieleweki ni kwa namna gani wanashiriki katika maamuzi katika shughuli za maendeleo na ukuaji wa uchumi wa nchi, huduma za jamii na maisha yao kwa ujumla.

#### 2.4.3.3 Tamko la Ilani Kuhusu Ushirikishwa wa Wananchi Katika Mipango na Maamuzi

Viongozi watakao chaguliwa wakiwemo wabunge na wawakilishi (na serikali):-

(i) Wanahitaji kuweka mikakati thabiti ya uendelezwaji wa utekelezaji wa sheria za SM ili kuwa na mipango na mifumo bora ya serikali za mitaa ambayo inalenga kupeleka madaraka kwa wananchi.

(ii) Ihakikishe inaboresha sheria za serikali za mitaa ili ziweze kuwa wajibisha viongozi wa vijiji/ mitaa ambao hawashirikishi wananchi kwenye zoezi la kuibua, kupanga na kusimamia miradi katika maeneo yao.

(iii) Waweke utaratibu utakaweza kuzibana serikali za mitaa/ serikali kuu kuheshimu maamuzi ya vikao halali vya serikali za mitaa/ vijiji vilivyobainisha vipaumbele vya wananchi na hivyo ndivyo vipewe fedha kwa utekelezaji.

(iv) Utaratibu wa matumizi wa kodi zinazokusanywa katika ngazi za Halmashauri zikiwemo maegesho ya magari, mabango ya matangazo na fedha zinzokusanywa kutoka kwa wafanya biashara wadogo ziwe zinabaki katika halmashauri ili kuziimarisha kifedha.

(v) Kuhakikisha wananchi kuanzia ngazi ya vijiji/ mitaa kupitia serikali zao wanashiriki ipasavyo katika kutunga na kuboresha sera zanchi badala ya kuwa watekelezaji tu.

(vi) Iwaelimishe wananchi kuhusu ulipaji kodi na ihakikishe inakusanyakodi nakutumia mapato ya kodi hizo kwa manufaa ya wananchi.

### 2.4.4 Haki za Makundi Maalum

#### 2.4.4.1 Hali Ilivyo Sasa

Haki za makundi maalum ni haki zote za binadamu katika makundi mbalimbali ya watu wanaotakiwa kupewa uangalizi maalum kwa sababu ya hali ya mazingira magumu wanayokutana nayo katika jamii. Makundi haya ni kama vile watoto, vijana, watu wenye ulemavu (WWU), wakimbizi, wazee, wanawake na makundi mengine madogo katika jamii mfano wadzabe (wanaoishi kimila hasa kwa kuotota matunda na kuwinda).

Kwa kuwa haki za watu walio katika makundi haya zimeainishwa katika haki za binadamu kiujumla wake, kumekuwepo na usahaulifu wa mamlaka husika na wananchi kuwa, makundi haya yanahitaji uangalizi maalum kutokana na hali yao ya wepesi wa kuathirika na mazingira wanayokutana nayo katika maisha. Mathalani, mauaji ya watu wenye ualbino nchini, sheria kandamizi dhidi ya wanawake na watoto na pia ukosefu wa hifadhi ya jamii kwa wazee na makundi mengine ya pembezoni.

#### 2.4.4.2 Jitihada Zilizochukuliwa

Jitahada za mkusudi zimechukuliwa kushuhulikia madai ya makundi haya ya kiwemo kutungwa kwa na kupitishwa sheria ya kumlinda mtoto na kuanzishwa kwa pensheni jamii kwa wazee wote (universal pension scheme) waliofikia umri wa miaka 70 mwaka 2017 (Zanzibar). Kuwepo fursa kwa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu, kunazishwa kwa mifuko ya vijana katika halmashauri ambapo asilimia 2 ya bajeti ya Halamshauri inaingizwa katika mfuko wa vijana - ingawa ni vijana wachache ndiyo wameshafikiwa hadi sasa kupitia vikundi vya ujasiliamali. Vilevile, Mamlaka za SM zote (Tanzania Bara) zinatakiwa kutenga asilimia 10 kutoka katika makusanyo yao kwa ajili ya wanawake (4%), vijana (4%) na WWU (2%).

#### 2.4.4.3 Tamko la Ilani Kuhusu ya Makundi Maalum

Ilani hii inawataka viongozi watakaochaguliwa wazingatie na kutoa kipaumbele haki za makundi maalum ili kuleta usawa kwa binadamu wote. Serikali ya JMT ianzishe pensheni jamii kwa wazee wote waliofikia umri wa miaka 70 ili kuwapunguzi ukali wa maisha.

### 2.4.5 Haki za Kisiasa

#### 2.4.5.1 Hali Ilivyo Sasa

Haki za kisiasa ni haki za msingi katika kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika shughuli za umma na utawala wa nchi. Kila raia ana uhuru wa kushiriki ipasavyo katika utawala wa nchi yake moja kwa moja au kupitia wawakilishi wake. Kama ilivyotamkwa hapo awali, Ibara ya 8 na 21 za Katiba zinasisitiza kuwa mamlaka ya nchi yatatoka kwa wananchi na wananchi wanahaki ya kuchagua na kuchaguliwa.

> *Wananchi wana haki ya kushiriki katika mipango na maamuzi yanayohusiana na uendeshaji wanchiyao. Katika kipindi cha uchaguzi wa mwaka 2015 na katika chaguzi ndogo wananchi wachache wameshiriki katika kuweka viongozi waliopo sasa madarakani. Kwa upande wa Zanzibar Uchaguzi wa marudio ulifanyika kwa wananchi wa chache ikilinganisha na walioshiriki katika uchaguzi uliofutwa.*

Kwa upande wa daftari la wapiga kura linapaswa kufanyiwa mapitio mara mbili ndani ya miaka mitano. Hali ilivyo sasa daftari linafanyiwa mapitio mara moja tu tena kwa utaratibu wa haraka sana. Hali hii imepelekea kuathiri dhana ya ushirikishwaji ambayo ni miongoni mwa misingi mikuu ya utawala bora Tanzania.

#### 2.4.5.2 Jitihada Zilizochukuliwa

AZAKI, viongozi na watendaji wa vyama vya siasa wamekuwa wakidai marekebisho ya vifungu vya sheria ambavyo vinaminya uhuru wa kisiasa. Hata hivyo, bado hakujawa na mabadiliko ya sheria hizo na badala yake, baadhi ya viongozi wa umma wamekuwa wakitumia vyombo vya dola kuendelea kukandamizi uhuru wa kisiasa.

#### 2.4.5.3 Tamko la Ilani Kuhusu Haki za Kisiasa

AZAKI tunahitaji:-

(i) Uwepo wa mazingira ya uhuru na ushirikishwaji kwa wananchi katika utawala wanchi ili kuheshimu misingi ya demokrasia na utawala bora Tanzania.

(ii) Kuwepo mfumo wa siasa unaotoa fursa sawa kwa wananchi wote na makundi yote ya kisiasa bila ubaguzi au upendeleo na kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki katika mazingira sawa na wezeshi kwa wananchi kushiriki utawala wanchi yao. Mathalani kuhakikisha nafasi ya mwananchi kugombea kama mgombea binafsi inakuwepo.

### 2.4.6 Utawala wa Kitaasisi

#### 2.4.6.1 Hali Ilivyo Sasa

Msingi ya demokrasia na utawala bora unasisitiza umuhimu wa kufanya maamuzi kwa njia ya vikao halali vya taasisi husika badala ya mtu mmoja kutoa maamuzi. Tanzania inaongozwa na utawala wa kikatiba wa mgawanyo wa madaraka ambao unajumuisha Mahakama, Bunge na Serikali. Kwa upande wa Zanzibar kuna Baraza la Wawakilishi, Mahakama pia na Serikali.

Kumejitokeza changamoto kwa baadhi ya viongozi kuingilia mamlaka ya mihimili mingine ya dola na hasa kutoa mamamuzi bila ya kushirikisha muhimili husika au idara mahususi ndani ya muhimili. Mfano, kuna baadhi ya maamuzi ya Bunge hayajahusisha kamati za kudumu za Bunge. Pia kutengua uteuzi wa baadhi ya watumishi wateule bila ya kushirikisha tume ya maadili ya utumishi wa Umma. Aidha, kauli za baadhi ya viongozi kwa Mahakama zimeonekana kama ni 'maagizo' kwa namna yalivyotolewa.

#### 2.4.6.2 Jitihada Zilizochukuliwa

Jitihada zimechukuliwa kudai Katiba mpya ambayo ingeweza, kati ya mambo mengine, kudhibiti madaraka kwa Rais kwa kuyapunguza kuyapeleka katika mihimili mingine kama njia ya kuboresha teuzi za viongozi wa umma. Mfano, uteuzi wa Majaji na Mawaziri, ungeweza kufanyika kwa kushirikisha Bunge na Baraza la Wawakilishi badala ya kuwa ni matakwa ya mtu au taasisi moja. Hata hivyo, madai ya Katiba mpya hayakufaikiwa na tayari uongozi wa juu wa JMT umeshaweka msimamo wa kutoendeleza mchakato wa Katiba mpya uliosimama toke mwaka 2015.

#### 2.4.6.3 Tamko la Ilani Kuhusu Utawala wa Kitaasisi

AZAKI tunataka viongozi watakaoteuliwa kuzingatia misingi ya utawala bora kwa kushirikisha vyombo husika katika kufanya maauzi yanayohusu utawala na kuzingtia misingi ya kidemokrasia, haki za binaadam na utawala bora.



## Sura ya 3

# UKATIBA NA UTAWALA WA SHERIA

### 3.1 UTANGULIZI

Katika Ilani ya AZAKI ya mwaka 2015, masuala ya katiba mpya, utawala wa sheria na mgawanyo wa madaraka yalikuwa ni mojawapo ya vipaumbele vikubwa vya AZAKI na Watanzania kwa ujumla. Watanzania walitaka kupata viongozi wanaolinda Katiba, wanaoongoza kwa misingi ya utawala bora, kuzingatia na kuweka mifumo ya mgawanyo wa madaraka pamoja na upatikanaji wa Katiba mpya. AZAKI zinaamini kuwa amani, utulivu, ustawi wa jamii na maendeleo endelevu ya taifa hutegemea sana misingi ya kikatiba, mgawanyo wa madaraka na utawala wa kisheria.

### 3.2 TATHMINI FUPI YA ILANI ILIYOPITA KUHUSU UKATIBA NA SHERIA

#### 3.2.1 Mafanikio

Kwa mujibu wa tathmini ya AZAKI, kiujumla takwa hili halikufanyiwa kazi kwa asilimia kubwa katika utawala huu wa awamu ya tano.

Tanzania kwa muda mrefu sasa imekuwa na changamoto kubwa kuhusu utawala wenye kufuata misingi ya sheria na mgawanyo wa madaraka. Utendaji wa viongozi wengi wa serikali hasa wanapotekeleza majukumu yao ya kiutawala umekuwa wa kutokuzingatia Katiba, sheria za nchi na wenye kukiuka haki za binadamu. Hali hii ya kutokutii na kuheshimu sheria za nchi siyo tu imekuwa ikijitokeza kwa viongozi bali hata kwa wananchi wenyewe. Kwa mfano, kuna madai kuwa baadhi ya fedha za umma zimekuwa zikitumika pasipo kufuata bajeti iliyoamriwa na Bunge.

#### 3.2.2 Mapungufu

Changamoto ya mgawanyo wa madaraka imezidi kushamiri. Aidha, utawala wa sheria umekumbwa na changamoto kadhaa na hadi tunapoandaa Ilani hii ya AZAKI ya 2019/2020 hakuna dalili za kupatikana kwa Katiba mpya. Wizara ya Katiba na Sheria haikuwahi kuonyesha dalili ya kumalizia mchakato wa Katiba mpya ulianzishwa na serikali ya awamu ya nne. Hali inatokana na sababu tajwa hapo juu.

Kwa upande mwingine, serikali imekuwa ikiandaa sheria kadhaa ambazo badala ya kuboresha utawala wa sheria , zimekuwa zikiongeza idadi ya sheria kandamizi. Kwa ujumla misingi ya utawala wa sheria, ukatiba na mgawanyo wa madaraka bado ni changamoto kubwa katika taifa hili. Masuala yote haya yanahitaji utashi wa viongozi wenye maono mbadala – hasa viongozi watakaoweza kusimamia na kulinda Katiba, kuleta Katiba mpya, mifumo ya kiutawala inayolinda mgawanyo wa madaraka na utawala wa sheria.

### 3.3 HALI YA USIMAMIZI NA ULINZI WA KATIBA YA SASA

Msingi wa ulinzi na usimamizi wa Katiba ya sasa upo katika Katiba yenyewe. Mfano, Ibara ya 26 ya Katiba ya JMT ya 1977 inabainisha kuwa, kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za nchi. Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 nayo ina masharti kama hayo.

Mbali na kukwama kwa hitaji la kuwa na Katiba mpya, kwa sasa kuna mazingira mengi yanadhirisha kuwa hata Katiba zinazotumika kwa sasa JMT haziheshimiwi na kulindwa ipasavyo na viongozi walioko madarakani. Matukio na maamuzi mengi yamekuwa yakifanyika pasipo kufuata misingi ya kikatiba.

> *Mfano Katiba Zanzibar imeeleza muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ila kwa sasa Zanzibar hakuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Katika marekebisho yaliofanywa 2010 pamoja na mambo mengine imeondosha nafasi ya Waziri Kiongozi na kuweka Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais. Kwa sasa, kuna Makamo mmoja tu wa Rais kinyume cha takwa la Katiba ya Zanzibar.*

Kwa upande wa Tanzania Bara, pia kuna mambo mengi ya ukiukwaji wa Katiba. Kwa mfano, amri ya kuzuia mikutano ya hadhara na maandamano ya vyama vya siasa iliyotolewa na Rais wa JMT. Amri hii inakinzana na masharti ya Katiba. Aidha, kama ilivyosemwa hapo awali, maamuzi ya kuzuia kuona majadaliano ya moja kwa moja ya Bunge la JMT ni kuwanyima wananchi fursa ya kujua hoja za wawakilishi wao. Vilevile, kumetungwa sheria kadhaa zinazovunja misingi ya kikatiba kama vile sheria ya takwimu, sheria ya makosa ya mtandao, marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa, sheria ya vyombo vya habari na kadhalika (zimejadiliwa katika sehemu nyingine za Ilani hii).

Hali kama hiyo pia inatekelezwa kwa upande wa Zanzibar ambayo Jeshi la Polisi limezuia kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya wanasiasa na baadhi ya mijadala na makongamano. Kwa mfano, Kituo cha Katiba cha nchini Uganda kilizuiwa kuzindua utafiti wao walioufanya kuhusiana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa hapa Zanzibar mwezi Agosti 2019.

### 3.4 TAMKO LA ILANI KUHUSU UTEKELEZAJI WA KATIBA

Kwa kwa sasa bado hakuna jitihada za kutosha zinazochukuliwa na Serikali zote mbili kuhakikisha katiba inalindwa na kuheshimiwa hasa na viongozi waliokula kiapo cha kulinda katiba, basi, kuna haja ya kuwa na viongozi wengine wenye nia hiyo. AZAKI tunatambua na kusistiza kuwa, ulinzi na usimamizi wa Katiba ya nchi ndio msingi wa utawala bora na utulivu katika taifa lolote lile. Hivyo basi:-

(i) Tunahitaji kupata viongozi watakaolinda na kuheshimu Katiba zote mbili.
(ii) Watanzania tuwachague viongozi watakaoonekana kujali misingi ya katiba na walio tayari kuongoza nchi kwa mujibu wa Katiba.

### 3.5 UFAFANUZI ZAIDI WA ILANI KUHUSU UTEKELEZAJI WA KATIBA

#### 3.5.1 Utawala Washeria

#### 3.5.1.1 Maana ya Utawala wa Sheria

Utawala wa sheria maana yake ni kuwa raia na viongozi wanatii na kuheshimu sheria. Sheria zote zinapaswa kutekelezwa na kupitishwa kwa uwazi na ushirikishwaji wa wananchi wote wanaoathiriwa na sheria husika na pia kuhakikisha kuna kuwepo na matumizi sahihi ya sheria husika kwa vyombo vyenye jukumu la kutekeleza sheria hizo. Vilevile, utawala wa sheria ni pamoja na kuhakikisha misingi yote ya haki za binadamu na usawa vinaheshimiwa na kulindwa; na pia, sheria zote zinazotungwa ziheshimu misingi ya haki za binadamu na kulinda Katiba.

#### 3.5.1.2 Hali ya Sasa na Jitihada Zilizochukuliwa

Madai ya AZAKI ya uwepo wa utawala wa sheria hayakuzingatiwa kwa kiasi kikubwa katika kipindi hiki cha utawala. Kwa mfano, viongozi wa ngazi mbalimbali wakifanya maamuzi yasiyozingatia utawala wa sheria na hata baada ya kufanya hivyo, viongozi hao hawajachukuliwa hatua za kisheria au kinidhamu.

#### 3.5.1.3 Tamko la Ilani Kuhusu Utawala wa Utawala wa Sheria

Ilituweze kuwa na Tanzania yenye kuheshimu utawala wa sheria, mtu mwenye kuutaka uongozi anapaswa kuwahakikishia watanzania kuwa:-

(i) Kutakuwa na taifa lenye kuzingatia utawala sheria. Tunahitaji taifa ambalo serikali na watendaji wake pamoja na mtu mmoja mmoja na taasisi binafsi wanawajibika na kufanya maamuzi kwa mujibu washeria.

(ii) Kuwepo na sheria nzuri, zinazojulikana na wote, zenye kuzingatia misingi ya haki, usawa na usalama wa watu na mali zao.

(iii) Sheria lazima ziwe wazi vya kutosha kwa sababu watu hawawezi kutii sheria ikiwa hawazielewi sheria hizo.

(iv) Taifa ambalo mchakato wa upatikanaji wa sheria na sera mbalimbali utazingatia uwazi na ushirikishwaji wa jamii na makundi mbalimbali ya raia nchini.

(v) Mfumo wa utoaji haki ambao ni huru, imara na wenye kuzingatia weledi, muda na usawa mbele ya sheria.

### 3.5.2 Mgawanyo wa Madaraka

#### 3.5.2.1 Hali Ilivyo kwa Sasa Kuhusu Mgawanyo wa Madaraka

Utawala wa sheria unahitaji kuwa mihimili mikuu ya nchi, yaani serikali, bunge na mahakama vinatenganishwa na haviingiliani katika utendaji kazi. Kutenganishwa huko kunalenga pia kuzuia watendaji katika chombo kimoja kuwa na majukumu katika chombo kingine.

Hali ya sasa inaonyesha kuwa, Tanzania haina mgawanyo sahihi wa madaraka kama ilivyojadiliwa hapo awali. Mihimili mikuu ya dola (Bunge, Mahakama na Serikali) zimekuwa vikiingiliana katika utendaji wake wa kila siku na wakati mwingine mhimili mmoja kukimbia majukumu yake kwa kisingizio cha kuepusha mgongano na mhimili mwingine.

Changamoto nyingine za kimfumo ni pamoja na wabunge kuwa mawaziri. Kiutawala imekuwa ni vigumu kutenganisha chama na serikali au kutenganisha maamuzi ya bunge na serikali. Bunge limeonekana mara kadhaa kushindwa kutimiza majukumu yake ya kusimamia serikali kutokana na mfumo wa sasa ambayo Rais na mawiziri ni sehemu ya bunge.

#### 3.5.2.2 Tamko la Ilani Kuhusu Mgawanyo wa Madaraka

Ili kuhakikisha taifa linakuwa na maendeleo endelevu kwa ngazi zote na kwa watanzania wote, tunahitaji:

(i) Viongozi watakaohakisha mgawanyo wa madaraka unapatikana na kuheshimiwa. Mathalani, Serikali kutotawala, kuingilia ama kufanya kazi za mhimili mwingine kama Bunge na Mahakama.

(ii) Tanzania ambayo mawaziri hawatokani na wabunge ilikujenga vizuri dhana ya mgawanyo wa madaraka na uwajibikaji.

(iii) Uwepo wa vyombo huru vya utoaji haki hasa Mahakama; Tume ya Hakiza Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG); na, Tume za Uchaguzi. Wasimamizi wa uchaguzi ngazi za wilaya wasitokane na chama chochote au serikali za mitaa bali tume iwe na watumishi wake watakao ajiriwa.

(iv) Tanzania yenye mfumo wa uongozi ambao hautoi mwanya kwa watumishi wa umma kushika nafasi za kisiasa wakiwa na nyadhifa za kiserikali kama ukurugenzi.

(v) Tanzania yenye mfumo wa uongozi ambao hutenganisha shughuli binafsi za kibiashara na uongozi wa umma ili kuepuka mgongano wakimaslahi.

(vi) Serikali inayoingia madarakani ipunguze mrundikano wa madaraka kwa watendaji wake. Endapo mtu atakuwa mbunge asiwe mkuu wa mkoa/ wilaya wala mjumbe kwenye Bodiza Mashirika ya umma.

(vii) Serikali kuu isimamie vizuri dhana ya ugatuzi kwa kupeleka madaraka mikoani na kuacha kuingilia mapato na kazi za serikali za mitaa

### 3.5.2.3 Uhitaji wa Katiba Mpya

Mchakato wa Katiba mpya ulikuwa shirikishi na watanzania wengi walishiriki na kutoa maoni yao miaka ya 2013 hadi 2015. Katiba iliyotokana na Bunge la Katiba na ile ilyotokana Tume ya Katiba mpya (Tume ya Warioba), zote kwa pamoja zilikuwa zimebeba mawazo ya watanzania kwa asilimia kubwa. Watanzania wana amini endapo Tanzania itapata katiba mpya mambo mengi yanayohusu mfumo wa utawala, mgawanyo wa madaraka, utawala wa sheria, haki za binadamu, rasilimali za nchi, rushwa na utawala bora zitakuwa zimetatuliwa kwa asilimia kubwa.



## Sura ya 4

# UCHUMI JUMUISHI NA ENDELEVU

### 4.1 UTANGULIZI

Tanzania ni nchi inayoongozwa na Dira ya Maendeleo Taifa 2025 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (FYDP II) katika juhudi za kufikia maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Taarifa rasmi zinaonesha kuwa uchumi wa Tanzania umekua ukikua kwa wastani wa asilimia 7 katika miaka ya hivi karibuni. Kwa kadiri ya taarifa za Serikali ukuaji unakadiriwa kuongezeka hadi kufika asilimia 7.3 ifikapo mwaka 2019/ 2020. Hata hivyo, taarifa ya Benki ya Dunia ya 2019 imeonyesha kuwa ukuaji utakuwa chini ya kiwango hiki.

Pamoja na kuongezeka kwa tarakimu zinazoashiria ukuaji wa uchumi mkuu, bado ukuaji huo haujawa dhairi kwenye maisha ya walio wengi hasa watu wa kipato kidogo. Haujaleta ajira na vipato vingi na haujapunguza umasikini kwa kiasi kikubwa katika jamii.

Ili kuleta tija kwenye ngazi zote za jamii, nadharia ya uchumi jumuishi; ajira zenye staha na tija; ustawi wa jamii; na, usalama wa mali zao, ni masuala yanayopaswa kutiliwa mkazo na kila mgombea au chama kinachotaka madaraka ya kuongoza umma.

### 4.2 MAANA NA MANTIKI YA UCHUMI JUMUISHI

Uchumi jumuishi ni uchumi unaonufaisha kila mwananchi katika nyanja zote zikiwemo za kisiasa na kijamii. Vilevile, uchumi wa aina hiyo unaweza kulinufaisha taifa moja kwa ujumla au mataifa mengi yaliyokubaliana na kuungana.

Katika mazingiria ya uchumi huria ni wazi kwamba serikali sio muendeshaji pekee wa uchumi bali inatakiwa wadau mbalimbali (wakiwemo watu masikini na walio pembezoni) wachangie katika kujenga uchumi wa taifa lao ambapo wanunuzi na wauzaji wa bidhaa na huduma hufanya kazi kwa uhuru chini ya uangalizi mdogo wa serikali. Serikali inao wajibu wa kuweka mazingira rafiki na ya kuvutia ya kisera, kisheria na kiudhibiti ili sekta binafsi iweze kuwa injini ya ukuaji na uendeshaji wa uchumi.

> *Ifahamike kuwa, katika dhana hii ya kiuchumi, lengo halipaswi tu kuwa ni kukua kwa uchumi bali uchumi ukue na kuwanufaisha wananchi. Unatakiwa kuwa na ukuaji unaoleta ajira zenye staha, unaoleta vipato endelevu, unaopunguza umasikini, ulio shirikishi, ulio endelevu, unaojali mazingira, unaojali haki za binadamu na utawala bora.*

AZAKI tunaamini na kushauri kuwa, kupima kiwango cha ukuaji wa uchumi ni lazima kuhakikisha maeneo yote muhimu yanazingatiwa kwa sababu kama kutakosekana moja wapo linaweza kusababisha udumavu au kutokukua kabisa kwa uchumi. Pamoja na kukuza uchumi wa Taifa ni vyema kupima na kujiridhisha kwamba uchumi wa raia mmoja mmoja unakua pia.

### 4.3 TATHMINI FUPI YA ILANI ILIYOPITA KUHUSU UCHUMI JUMUISHI

#### 4.3.1 Mafanikio

Serikali ya awamu ya tano imefanya kazi kubwa sana katika kukuza uchumi wa kitaifa. Juhudi hizi ni pamoja na:-

(i) Kuboresha miundo mbinu ikiwemo miundombinu ya nishati kama vile umeme wa mto Rufiji, barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari. Lengo ni kurahisisha biashara na shuguli nyingine za kiuchumi kufanyika kwa urahisi na haraka.

(ii) Kuimarisha biashara kwa wafanyabiashara ndogondogo (wamachinga) kwa kuwaongezea unafuu wa kulipa ushuru wa Shilingi elfu 20 kila mwaka. Hali hii imechangia pia kurasimisha biashara hizi na kuongeza usalama wao ukilinganisha na hapo awali walipokuwa hawatambuliki na kunyanyasika sana.

(iii) Kufufua shirika la ndege la serikali (ATCL) kwa kununua ndege mpya kwa hela taslimu. Hii ni hatua muhimu ambayo itatanua wigo kwa Watanzania kufanya biashara nje na ndani ya nchi pamoja na kupanua sekta ya utalii nchini.

(iv) Katika bajeti ya mwaka 2019/ 2020 serikali imejitahidi kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya kiudhibiti katika kuanzisha na kuendesha biashara. Mpango huu ujulikanao kama Blue Print umeanza kutekelezwa rasmi katika mwaka wa fedha 2019/ 2020.

(v) Kudhibiti mianya mingi ya wizi na utoroshwaji wa mali na rasilimali za taifa kama vile madini. Jambo hili limepelekea ongezeko la pato la ndani katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2018/ 2019 (Julai - Novemba), makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) yalifikia TZS 7.37 trlioni sawa na 88.9% ya makadirio ya TZS 8.30 trilioni katika kipindi hicho.

(vi) Kuongezeka kwa mapato yasiyo ya kodi – kutokana na kuimarishwa kwa ufuatiliaji kwenye taasisi, mashirika na kampuni kulikoiwezesha serikali kupata michango na gawio stahiki kutoka kwenye uwekezaji wake.

(vii) Kuimarika kwa matumizi ya technolojia katika ukusanyaji wa maduhuli kwenye wizara na idara zinazojitegemea kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato uitwao 'Government Electronic Payment Gateway' (GePG) ambapo kati ya Julai 2017 hadi Novemba 2018, jumla ya Taasisi za Serikali 325 zinatumia mfumo huu kukusanya maduhuli.

#### 4.3.2 Mapungufu

Pamoja na mambo mazuri yanayofanywa na serikali, kumekuwa na malalamiko kwamba uchumi wa nchi katika ngazi ya taifa unakua vizuri ila haujazingatia ukuaji wa uchumi wa wananchi wenyewe hasa wale masikini. Pia, kuna changamoto ya kutokuongeza mishara kwa watumishi wa umma na kutumia asilimia kubwa ya mapato ya ndani kuwekeza kwenye miundo mbinu moja kwa moja bila kuwa na mlinganyo sawia katika maeneo mengine yanayochangia ukuaji wa uchumi haya yamelalamikiwa kama mambo ambayo yanaondoa dhana ya uchumi jumuishi.

### 4.4 TAMKO LA ILANI KUHUSU UCHUMI JUMUISHI

Kuhusu uchumi jumuishi, AZAKI tunahitaji kuwa na wagombea nafasi za uongozi ambao, kati ya mambo mengine ya msingi viongozi:-

(i) Watakaowezesha na kurahisisha ushiriki na kufaidi kwa kila Raia kwenye ukuaji wa uchumi.

(ii) Watakaoweza kuendeleza na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na kuvutia na kubakiza wawekezaji kutoka nje ambao watashirikiana na wazawa.

(iii) Watakaounda serikali itakayotengeneza mazingira mazuri ya kuhakikisha inajumuisha kila raia katika kukuza uchumi na kufaidi matunda yake ili kuongeza pato la taifa na kuimarisha ustawi wa mtu mmoja mmoja.

(iv) Watakaounda serikali itakayozingatia na kuweka mlinganyo sawa katika maeneo yote ya uchumi, kijiografia, kijinsia na umri ili kupata uchumi jumuishi.

## 4.5 UFAFANUZI ZAIDI WA ILANI KUHUSU UCHUMI

### 4.5.1 Uchumi Endelevu – Hali Ilivyo Kwa Sasa

Uchumi endelevu ni ule unaokua kwa kuongezeka lakini si kwa kurudi nyuma au kuwa na ongezeko lile lile kwa miaka kadhaa wa kadhaa. Uchumi endelevu ni lazima uzingatie uhifadhi wa mazingira. Katika kuangazia masuala ya Uchumi endelevu, mwaka 2015 AZAKI tulitoa madai ya kufufua na kuendeleza kilimo cha kisasa na endelevu kwa kutumia umwagiliaji na nyezo za kiteknolojia za kilimo cha kisasa, mikakati ya kuboresha viwanda vikubwa na vidogo vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kufufua viwanda vilivyokuwa vikizalisha nguo, nyama, minofu ya samaki na kadhalika.

#### 4.5.1.1 Mafanikio

Katika utekelezaji wa madai ya AZAKI, tumeona juhudi mbali mbali za serikali katika kusimamia shuguli za kilimo hata kupelekea kutenguliwa kwa baadhi ya mawaziri ambao hawakufikia ufanisi unaohitajika ili kupata mafanikio katika sekta hii ya kilimo. Katika mazao serikali imejitahidi kutetea haki za wakulima kwa kuhakikisha kuwa inasimamia bei za mazao yao kama vile korosho, pamba, tumbako nk. Mafanikio chanya mengine ni pamoja na:-

(i) Serikali imepunguza na kudhibiti kodi mbali mbali zilizokuwa zinatozwa kwa wakulima haswa wakati wa kusafirisha mazao yao.

(ii) Serikali imefanya juhudi kubwa za kukuza viwanda vikubwa na vidogo vidogo ikiwemo pia ni kubadilisha Mawaziri kadhaa wa kadhaa ili kuleta utendaji wenye tija.

(iii) Serikali imeweka mikakati ya kila mkoa kuwa na angalau viwanda 100 kwa mwaka vinavyofanya kazi na viajiri asilimia kubwa wazawa wa maeneo yale kilipo kiwanda, vitumie maligafi ya nyumbani, viuze katika soko la ndani na kuuza ziada nje.

(iv) Serikali imewasaidia wasindikaji wadogo wadogo kwa namna mbali mbali kama vile kuwawezesha na nyezo, mikopo na ujuzi wa aina mbali mbali.


(v) Serikali imelisimamia suala la ufufuaji wa viwanda haswa vile vya pamba na vya nyama lakini pia imeweza kuhamasisha wawekezaji kufungua viwanda vingine vipya maeneo mengi Nchini wakiongozwa na Mkoa wa Pwani.

#### 4.5.1.2 Changamoto

Pamoja na juhudi hizo zilizofanywa na serikali, bado kunachangamoto katika masoko ya mazao ya wakulima kama vile korosho na mbaazi. Pia gharama ya uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vidogo vidogo ni kubwa ukilinganiasha na maisha halisi ya wananchi walio wengi hali inayopelekea kukosekana muendelezo wa baadhi ya viwanda vidogo vidogo na hata kufikia hatua ya kufungwa kabisa.

Aidha, japokuwa serikali imekua ikifanya jitihada kadhaa katika kukuza uchumi wa taifa letu; na, tayari kumekuwa na mafanikio mbalimbali katika jitihada hizo ikiwa ni pamoja na kuwa na uchumi unaokuwa kwa asilimia 6.8 hadi 7 kila mwaka. Hata hivyo ukuaji huu wa uchumi haujapunguza umaskini na kuleta ajira kwa namna inavyotarajiawa na watanzania.

Kwa mujibu wa takwimu za Trading Economics deni la nje la taifa hadi kufikia aprili 2019 lilikuwa $21587.90 milioni ambayo ni sawa na TZS 50,062,572,000,000. Deni hili la nje la taifa limekua likikua kwa kasi kubwa ambapo, mwezi Julai 2018 lilikuwa $19883.6 milioni, Oktoba 2018 lilikuwa ni $20759.1 milioni, Januari 2019 lilikuwa $21184.2 milioni na mpaka kufikia Aprili 2019 lilifikia $21587.9 milioni. Pamoja na deni hili kukua pia riba yake inaongezeka kila mwaka na hali hii ni dhahiri kwamba linatishia hali ya kuwa na uchumi endelevu.




*Takwimu za Ukuaji wa Deni la Nje la Taifa 2018 – 2019.*

Katika deni la taifa, Serikali imesema mara kadhaa kuwa pamoja na ukuaji huu wa deni, bado deni ni himilivu kwa kutumia vigezo kadhaa. Jambo muhimu la kimjadala katika deni la taifa ni kasi ya ukuaji wake. Kama taifa linakopa na kutumia vizuri fedha katika shughuli za maendeleo sio vibaya. Hata hivyo ni muhimu kuwa na uangalifu mkubwa kuhusu mwenendo wa ukuaji wa deni kwa ujumla, masharti ya kukopa, athari za muda mfupi, wa kati na mrefu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

#### 4.5.1.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uchumi Endelevu

AZAKI Tunahitaji:-

(i) Viongozi watakaosimamia ukuaji wa uchumi, kupanda kutoka tarakimu moja (7%) kwenda tarakimu mbili yaani zaidi ya 10%.

(ii) Uukuaji endelevu wenye manufaa kwa wananchi. Hii ni pamoja na kuhakikisha anapanua wigo wa mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje.

(iii) Serikali itakayoweza kusimamia ukuaji wa viwanda vilivyoanzishwa kwa kuwaraihisishia gharama za uendeshaji na kupanua wingo kwa wawekezaji wapya ili kuwekeza kwa mikataba nafuu na yenye masilahi kwa watanzania.

(iv) Serikali itakayoweka msisitizo katika kilimo na viwanda kwa kutenga bajeti ya kutosha na yenye tija katika sekta hizi.

#### 4.5.2 Dira na Mpango wa Maendeleo yaTaifa na Uchumi wa Tanzania
#### 4.5.2.1 Kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ni mwongozo au mwelekeo wa Tanzania kama taifa linavyotaka kuwa itakapofika mwaka 2025. Lengo kuu ni kuielekeza Tanzania kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Malengo makuu matatu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ni kuwaletea wananchi maisha bora na mazuri; kudumisha uongozi bora na utawala wa sheria; na, kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani.

#### 4.5.2.2 Kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2018-2021

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2018/19 ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/2017 – 2020/2021. Malengo mahsusi ya Mpango huu ni:-

(i) Kuendeleza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kuongeza matumizi ya fursa na majaliwa ya kipekee ya nchi kwa tija.

(ii) Kuimarisha kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, hasa kwa kutanzua changamoto za upatikanaji wa fedha na mitaji, ardhi na maeneo ya uwekezaji, na kuimarisha mipango miji na maendeleo ya makazi.

(iii) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

(iv) Kupanua fursa kuwezesha wananchi wengi kushiriki katika uwekezaji na uendeshaji biashara ili kuongeza uwezo wa nchi na wananchi kupambana na umaskini.

(v) Kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii kwa kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji na kinga kwa jamii na kaya maskini.

(vi) Kuongeza idadi ya rasilimali watu yenye ujuzi na weledi unaohitajika katika uendeshaji wa uchumi wa viwanda na kuimarisha upatikanaji wa teknolojia na ubunifu na hivyo kujenga uwezo wa nchi kushindana kibiashara.

(vii) Kuongeza uzalishaji katika sekta asili (primary production) ili kukidhi mahitaji na usalama wa chakula na upatikanaji wa mazao ghafi kwa uzalishaji viwandani kwa bei itakayowezesha ushindani kimataifa.

#### 4.5.2.3 Madai ya AZAKI kuhusu Dira ya Maendeleo yaTaifa na Uchumi wa Tanzania

AZAKI tunahitaji:-

(i) Viongozi na serikali itakayosimamia na kutekeleza kikamilifu sera zetu zinazopelekea ukuaji wa kiuchumi (FYDP II na III) ipasavyo ili kuwa Taifa la uchumi wa kati.

(ii) Viongozi na serikali itakayoweza kuboresha sera zetu za uchumi mara kwa mara ili kuendana na mazigira yanayohitajika katika kukuza uchumi wa nchi ya Tanzania.

(iii) Viongozi na serikali itakayodhibiti mfumuko wa bei na upatikanaji wa huduma na bidhaa nafuu za kijamii ili kupunguza umasikini.

(iv) Viongozi na serikali itakayosimamia ongezeko la uzalishaji katika sekta zote za uchumi kama vile viwanda, madini, utalii, kilimo na kadhalika ili kuongeza uuzaji wa bidhaa na huduma ndani na nje ya nchi na kupelekea kukuza uchumi jumuishi kwa njia endelevu.

### 4.5.3 Ajira na Ustawi wa Jamii

#### 4.5.3.1 Mantiki ya Kutilia Mkazo Masuala ya Ajira na Ustawi wa Jamii

Taifa linalokua kiuchumi linapimwa kwa njia mbalimbali - ikiwemo kuangalia idadi ya watu walio na ajira au waliokosa ajira. Wananchi wengi wakiwa na ajira au shughuli zozote za kuwaingizia kipato ni dhahiri kwamba wanaongeza idadi ya kuchangia pato la taifa ambalo pia uchangia katika ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Serikali makini na inayotaka uchumi wake ukue vizuri huwa inatengeneza mazigira rafiki, ya kuvutia na wenzeshi kwa kila mwananchi kupata shughuli ya kumuingizia kipato endelevu. Hii ni pamoja na kutoa ajira au kuajiri, kuwezesha biashara na shughuli za kilimo, kurasimisha na kuongeza thamani ya shuguli za kuingiza kipato katika sekta sisizo rasmi, kulinda wawekeza na wafanyabiashara katika kuwajengea mazingira rafiki na wenzeshi ili kukuza biashara zao, kupunguza kodi na milolongo mingine ili kuwezesha biashara nyingi kwa wakati mmoja nk.

#### 4.5.3.2 Tathmini Fupi ya Ilani Iliyopita Kuhusu Ajira na Ustawi wa Jamii

Serikali ya Awamu ya tano imefanya jitihada kubwa katika kuimarisha hali ya wafanya biashara na wawekezaji nchi. Hii ni pamoja na vikao vinavyofanywa mara kwa mara na Mheshimiwa Rais na wafanyabiashara na wawekezaji wa sekta mbalimbali ili kusikiliza na kutatua kero zao. Mafanikio mengine ni pamoja na, kuwa serikali:-

(i) Imeweza kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zinalenga mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) na pia kupunguza baadhi ya kodi zilizokuwa zinakandamiza wafanyabiashara na wawekezaji nchini.
(ii) Inatoa ajira kwa wastani wa 50,000 kwa mwaka katika sekta zake mbali mbali ndani na nje ya nchi.
(iii) Kupitia taasisi zake za kifedha (kama Benki ya Uwekezaji (TIB), Benki ya Kilimo Tanzania, n.k.) inatoa mikopo wezeshi kusaidia kukuza shunguli mbali mbali za kuongeza pato la taifa.

Hata hivyo, kwa kipindi cha nyuma na tulichonacho kuna baadhi ya mapungufu yaliyochangia kutokukua kwa kasi nzuri ya uchumi wa taifa letu ambayo yanaweza kusahihishwa na viongozi watakaoingia madarakani mwaka 2019/20. Mapungufu haya ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kuongezeka kwa tatizo la ukosefu wa ajira hadi 13.4% kwa vijana (15-35). Hii inatakana na serikali kutokubuni njia mbadala za kutengeneza ajira mpya haswa kwa vijana kupitia sekta zake, serikali kutokusimamia kikamilifu stahiki za wafanya kazi wa sekta binafsi na sisizo rasmi ili wapewe mikataba au mikataba yenye unafuu ya ajira, waunganishwe na mifuko ya kijamii, wakatiwe bima za afya nk.

(ii) Serikali kuelekeza hela nyingi sana za kimaendeleo katika miundombinu ukilinganisha na maeneo mengine haswa ya ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja.

#### 4.5.3.3 Tamko la Ilani Kuhusu Ajira na Ustawi wa Jamii

AZAKI tunahitaji:-

(i) Serikali itakayotengeneza ajira mpya na zenye staha kwa wingi kupitia sekta mbali mbali na pia kuimarisha na kusimamia mishahara ya watumishi wa umma na sekta binafsi mtawalia.

(ii) Serikali itakayompunguzia mwananchi kodi na makato mengine yatokanayo na mishahara na huduma zingine za kijamii.

(iii) Serikali itakayosaidia wahitimu haswa vijana kuajiriwa au kujiajiri kwa kutumia mapato ya nchi ya ndani kwa kubuni na kutekeleza miradi mipya (kwa kutoa ruzuku na mikopo) itokanayo na fursa zilizopo nchini katika sekta ya kilimo, viwanda, utalii, ubunifu wa habari na wamawasiliano, n.k.

(iv) Serikali itakayotengeneza ajira mpya kwa wingi kupitia sekta mbali mbali na pia kuhimarisha na kusimamia mishahara ya watumishi wa umma na sekta binafsi mtawalia.

(v) Serikali itakayompunguzia mwananchi kodi na makato mengine yatokanayo na mishahara na huduma zingine za kijamii.

### 4.5.4 Usalama wa Mali

#### 4.5.4.1 Hali ya Sasa kuhusu Usalama wa Mali

Kuna malalamiko ya baadhi ya raia kuhamishwa na kubomolewa nyumba na makazi yao bila kupewa fidia. Aidha, watumishi wa umma kukaa kipindi kirefu bila kupandishiwa mishahara au madaraja. Vilevile, makato ya mishahara haswa kwa wahitimu wanaodaiwa madeni ya mikopo ya elimu ya juu kupanda kwa kiasi kikubwa mno.

#### 4.5.4.2 Tamko la AZAKI Kuhusu Usalama wa Mali

AZAKI tunahitaji:-

(i) Kiongozi atakayesimamia na kulinda mali za raia mmoja mmoja na wawekezaji wote nchini kwa kuzingatia katiba na haki za binadamu.

(ii) Serikali itakayokuwa inatoafidia stahiki kwa kila raia na mali zake pale ambapo sheria inaelekeza kufanya hivyo endapo serikali au wawekezaji wanahitaji kutumia, kuamisha au kubomoa mali zake.

(iii) Kiongozi atakayesimamia na kulinda mali za raia mmoja mmoja na wawekezaji wote nchini kwa kuzingatia katiba na haki za binadamu.

(iv) Serikali itakayokuwa na kutabirika kwa mazingira ya kisera, kisheria na kiudhibiti katika biashara.



Sura ya 5

# ULINZI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA

## 5.1 UTANGULIZI

Nchi ya Tanzania imejaliwa kuwa na mazingira mazuri ya kijiolojia na utajiri mkubwa wa maliasili. Rasilimali hizo ni pamoja na misitu, ardhi, wanayamapori, bahari, maziwa, mito, madini na gesi asilia.

> *Pamoja na kuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali, mchango wake katika pato la taifa na maendeleo ya jamii bado ni mdogo chini na haukidhi matarajio ya wananchi. Mipango dhaifu ya kisera na kitaasisi, ukusanyaji duni wa mapato, ukosefu wa taaluma stahili na teknolojia, ukwepaji wa kodi wa wawekezaji na utoroshwaji mkubwa wa rasilimali hizo hususani madini kwenda masoko katika nchi jirani ni baadhi ya sababu zinazoifanya nchi isinufaike vilivyo na utajiri wa rasilimali hizo.*

Tanzania ina sheria mbalimbali zinazotambua na kusimamia maliasili na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. Sheria hizo kwa ujumla zinatamka kwamba maliasilia za nchi zitamilikiwa na kutumika kwa ajili ya umma wa Tanzania, huku Rais wa JMT akiwa ndiye muangalizi mkuu wa rasilimali hizi kwa niaba ya Watanzania. Ulinzi wa rasilimali na maliasili ni wajibu wa kila raia kwa mujibu wa Ibara 27(1) ya Katiba ya JMT ya 1977.

## 5.2 TATHMINI YA HALI HALISI NA UTEKELEZAJI WA ILANI YA AWALI

Kwa kutambua umuhimu wa rasilimali hizi, serikali ya jmt imechukua hatua mbalimbali kuhakisha inazilinda rasilimali hizi na kwamba umma wa Tanzania unaendelea kuwa wamiliki wa msingi wa rasilimali hizi. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuundwa kwa kamati maalumu na Mheshimiwa Rais wa JMT zikiwemo kamati maalum ya kuchunguza usafirishaji mchanga wa madini ambao hujasafishwa maarufu kwama 'Makinikia' mnamo May 2017 iliyoongozwa na Mwenyekiti Prof. Ossoro; pamoja na kamati maalum ya kuchunguza masuala ya kisheria na kiuchumi inayohusu mchanga huo iliyoongozwa na Prof. Mruma.

(ii) Uwepo wa jitihada zingine zilizofanywa kupitia kamati ya Bunge iliyoundwa na Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(iii) Mabadiliko ya kisera na kisheria pamoja na kuzuia na kudhibiti usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi chini ya the Mining (Mineral Beneficiations) Regulations of 2019; kutangaza mamlaka ya kudumu kimaamuzi juu ya utajiri rasilimali za nchi - Natural Wealth and Resource (Permanent Sovereignty) Act of 2017; sheria ya kupitia upya mikataba na masharti yanahusu rasilimali – Natural Wealth and Resource (Contract Review and Re-Negotiations of the Unconscionable Terms) Act of 2017 na; kujenga ukuta kuzunguka maeneo ya uchimbaji wa Tanzanite Mirerani; na vilevile, kuiwekea uthibiti kisheria chini ya the Mining (Mirerani Controlled Area) Regulations 2019 G.N. 135.

### 5.3 MADAI YA ILANI YA AZAKI

Pamoja na jitihadi hizo za serikali, bado kuna changamoto katika umiliki na ulinzi wa maliasili. Hivyo basi tunapendekeza kwa serikali na viongozi wajao kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuhakikisha kuwa maliasili za nchi yetu ni mali ya umma na kwamba Rais si mmiliki bali ni muangalizi tu.

(ii) Kuhakikisha mwananchi anashiriki kikamilifu katika maamuzi yote ya kimkakati juu ya rasilimali hizi.

(iii) Mipango na matumizi ya rasilimali iwe wenye tija na kuzingatia masilahi na ustawi wa wananchi wote.

(iv) Kuhakikisha kwamba wananchi na wadau wanashiriki kikamilifu katika hatua na michakato yote inayohusu usimamizi, uendelezwaji, ulinzi na umiliki wa rasilimali ikiwemo utungwaji wa sheria na sera.

(v) Serikali na viongozi wajao kuandaa mfumo bora na huru wa utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji (arbitration) na mahakama za biashara (commercial courts). Hii itawapa wawekezaji imani ya kupata maamuzi ya haki na usawa isiyoingiliwa kisiasa ili kuepuka kupeleka malalamiko kwa vyombo vya kisheria nje ya nchi (international investment dispute settlement mechanism).

(vi) Viongozi na serikali kuhakikisha kuwa uvunaji haramu wa maliasili za nchi unadhibitiwa na kutokomezwa kabisa.

### 5.4 UFAFANUZI ZAIDI KUHUSU USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA

#### 5.4.1 Usimamizi wa Rasilimali

Usimamizi wa rasilimali na maliasili za nchi unatakiwa uwe wenye tija kwa taifa. Hivyo serikali intakiwa kuongeza na kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali hizi.

##### 5.4.1.1 Tathmini Fupi ya Hali Halisi

Mwaka 2015 serikali ilitunga sheria ya uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini, mafuta na gasi kwa lengo la kukuza na kuboresha. Uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. Kwa miaka mingi sasa asasi za kiraia nchini zimekuwa zikifanya uchechemuzi kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za nchi.

Lengo likiwa ni kwa wananchi kuweza kupata taarifa kuhusu mikataba na mapato yatokanayo na rasilimali. Kwa miaka ya hivi karibu, AZAKI zinatambua jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali kwa lengo la kukuza na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika sekta ya uziduaji. Jitihada hizo ni kama vile uwepo na upatikanaji wa taarifa ya mwaka kuhusu mapato katika sekta ya uziduaji (TEITI Annual Reconciliation Report); utayari wa serikali kuweka wazi mikataba ya madini; na uwazi wa mapato yatokanayo na madini.

##### 5.4.1.2 Tamko la Ilani Kuhusu Usimamizi wa Rasilimali

Pamoja na jitihada hizi nzuri za serikali bado kuna changamoto ambazo viongozi wajao watatakiwa kuzifanyia kazi kwa karibu zaidi. AZAKI tutataka:-

(i) Serikali ijayo ihakikishe uwazi na uwajibikaji ipanue wigo kwenda kwenye usimamizi wa sekta zote za maliasili na rasilimali za taifa.

(ii) Serikali (kupitia Wizara ya Madini, Wizara ya Nishati) kuweka wazi mikataba ya madini, gesi na rasilimali zingine kwa kuzingatia kwamba, uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ni kitu cha msingi.

(iii) Serikali na viongozi wahakikishe sheria ya madini, mafuta na gesi asilia zinatoa mamlaka ya moja kwa moja kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata taarifa zitakazosaidia kulinda maslahi mapana ya nchi.

(iv) Kuimarisha na kutoa rasilimali za kutosha kwajili ya kamati ya ufuatiliaji wa mapato ya sekta hizi (TEITI).

(v) Bunge lipewe fursa kujadili na kuhakiki mikataba na makubaliano yote yanahusu sekta hizi kwa maslahi wa taifa.

### 5.4.2 Ushiriki wa Raia

Umma wa Tanzania mdio wamiliki wa mali asili zote za nchi, na wao ya kikatiba ya kushiriki katika kutunza na kulinda maliasili zote za Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya ya 27 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo fanyiwa marekebisho.

#### 5.4.2.1 Uwezeshaji Wazawa (Local Content)

Kwa kupitia Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na sheria ya Petroli ya mwaka 2015 pamoja na kanuni zake, kampuni za uchimbaji na uvunaji wa madini na gasi asilia Tanzania zinapaswa kuandaa na kuwasilisha mpango wa uwezeshaji wazawa katika kamati/ tume ya uwezeshaji wazawa. Kati ya masuala mengine, mpango huo utapaswa kuonesha namna kampuni za wananchi (wazawa) zitapata vipaumbele katika zabuni na bidhaa zinazopatikana nchini, upatikanaji wa ajira kwa watanzania na utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo zaidi waajiriwa wazawa. Kwa sasa suala hili kitaifa linaratibiwa na baraza la uwezeshaji wananchi kiuchumi (NEEC) pamoja na wizara husika.

#### 5.4.2.2 Tamko la Ilani Kuhusu Uwezeshaji Wazawa

AZAKI tunataka:-

(i) Serikali na viongozi wajao wapiti upya mpango mkakati wa taifa pamoja na sera ya taifa ya namna wazawa watashiriki katika mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya uziduaji na sekta nyingine za maliasili.

(ii) Serikali na viongozi wajao wahakikishe kuna mifumo na mikakati ya kuwaandaa wananchi ikiwemo kutenga mikakati bora ya bajeti na kitaasiis kwajili ya kuwajengea uwezo kushiriki kikamilifu katika mnyororo mzima wa thamani katika sekta ya uziduaji.

(iii) Kuwa na taarifa ya tathmini kila mwaka kuhusu hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza malengo ya sera na mipango hii.

(iv) Kuunga mkono uendelezaji wa sekta binafsi kwa wazawa kimkakati (indigenisation) kupitia sheria na kuondoa vikwazo vya kibiashara kupitia mfumo bora wa upatikanaji wa mikopo, teknolojia na kuondoa kodi kandamizi.

(v) Kushirikisha wadau katika kupitia mikakati ya maendeleo kwa kulenga uchimbaji mdogo wa madini.

(vi) Kufungamanisha mikakati ya sekta ya madini au/na gesi pamoja na sera ya viwanda, kilimo na ukuzaji mifumo ya elimu, sayansi na utafiti.

(vii) Kulinda na kutetea haki za wafanyakazi ili kupata ujira stahiki, bima za afya, mafunzo bora na mafao bora wanapostaafu.

### 5.4.3 Uwajibikaji wa Makampuni Kwa Jamii
#### 5.4.3.1 Jitihada Zilizofanyika

Chini ya Sheria ya Madini ya 2010, Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya 2017 pamoja na sheria ya Petroli ya mwaka 2015, makampuni yanawajibu wa kushiriki katika utoaji wa huduma za kijamii (corporate social responsibility) katika maeneo ambayo shughuli za uziduaji zinafanyika.

Sheria pia inaelekeza kuwa kila mwaka kampuni hizi zinapaswa kuandaa Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (Annual Corporate Social Responsibilty Plan). Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa kushiriki kujadiliana na kupitishwa kwa kuangalia vipaumbele vya eneo husika.

Pamoja na jitihada hizi, bado jambo hili linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo CSR uchukuliwa na makampuni kama sio jambo la lazima na ni msaada na ukarimu wa makampuni kwa jamii husika.

#### 5.4.3.2 Tamko la Ilani Kuhusu Uwajibikaji wa Makampuni Kwa Jamii

AZAKI tunataka:-

(i) Serikali na viongozi wajao wanapaswa kuhakikisha kuna ufuatiliaji wa karibu namna ambavyo makampuni yana wajibika kwa jamii.

(ii) Maeneo husika kuandaa mikutano ya wadau kila mwaka kujadili na kutathmini mipango ya kijamii na mipango hiyo iwe ya kwa muda wa angalau miaka mitatu mitatu.

(iii) Mipango ya Uwajibikaji wa Makampuni Kwa Jamii iweze kuchapishwa na kusambaziwa wananchi kupitia Wizara husika (madini au nishati) kwajili ya kujadiliwa na wananchi.

(iv) Kutambua mchango wa asasi zisizo za kiserikali katika kuelimisha na kushauri wananchi na hata serikali kuhusu mafanikio na athari katika utekelezaji wa sera na mipango ndani ya sekta hii.

(v) Tathmini ya haki za binadamu na haki ya umiliki ardhi katika maeneo yote yanayoguswa na uwekezaji, ikiwemo elimu kutolewa kwa wanaoathirika kabla na wakati wa utekelezaji wa uwekezaji mkubwa.

(vi) Kuruhusu Tume ya Utawala Bora na Haki za Binadamu, vyama vya wafanyakazi na asasi ziziso za kiserikali kufanya kazi kwa uhuru katika kutathmini na kuhakiki uwekezaji wa madini na mafuta.

### 5.4.4 Usimamizi wa Mapato Maliasili na Rasilimali za Nchi
#### 5.4.4.1 Jitihada na Hali Ilivyo Sasa

Pamoja na uwepo wa rasilimali nyingi katika nchi yetu, ni muhimu zaidi kuhakikisha kuwa uwekezaji unaofanywa na unagusa rasilimali hizo na kwamba, mapato yake kukusanywa na kusimamiwa vizuri kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho. Hii ni kutokana na sababu kuwa, rasilimali hizo kama madini, mafuta na gesi asilia hazidumu milele pindi tu uvunwaji wake unapoanza. Mwaka 2015, ilitungwa sheria ya usimamizi wa mapato yatokanayo na mafuta na gesi asilia (Oil and Gas Revenue Management Act of 2015) kwa ajili ya kuunda mfuko maalumu ya kutunza mapato yanayotokana na sekta hii.

#### 5.4.4.2 Tamko la Ilani Kuhusu Mapato Maliasili na Rasilimali za Nchi

AZAKI tunataka:-

(i) Serikali na viongozi wajao wahakikishe sekta ya madini pia itakuwa na sheria na mfuko wake (Sovereign

Welfare Fund) kama ilivyo sekta ya mafuta na gesi.

(ii) Serikali ihakikishe mfumo wa uwazi utakaosimamia usimamizi na ushiriki wa taasisi za dola kwenye uwekezaji kwenye madini na mafuta.

(iii) Serikali iimarishe sheria na mifumo kuimarisha upatikanaji wa taarifa za uzalishaji na uvunaji wa rasilimali,mapato yatokanayo na uvunaji huo pamoja majina ya wamiliki halisi wa biashara hizo ili kuepuka utoroshaji wa mapato nje ya nchi au/na utakatishaji fedha.

(iv) Usimamizi wa mifuko (Sovereign Welfare Fund) iwekwe chini ya wataalamu na sio wateule wa kisiasa, watakaowajibika kutoa taarifa kwa Bunge kama wawakilishi wa wananchi.

### 5.4.5 Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi

#### 5.4.5.1 Mazingira kama Haki ya Binadamu

Mazingira ni suala lenye umuhimu mkubwa katika maisha na Ustawi binadamu. Hivyo basi tunawajibu mkubwa wa kutunza mazingira yanayotuzunguka kwa mawanda mapana. Ni haki ya kila binadamu kuishi katika mazingira safi na salama kwa mujibu wa kifungu la 4 la Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004.

#### 5.4.5.2 Tathmini ya Hali Halisi Kuhusu Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi

Sambamba na kuzingatia uhifadhi na utunzaji wa mazingira, mabadiliko ya tabia nchi ni muhimu zaidi kuzingatiwa kwani majanga makubwa hususani, kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha joto , kukosa mvua kwa msimu mahususi, vimbunga, kupungua kwa kina cha maji katika bahari na maziwa, kupotea au kuzama kwa baadhi ya visiwa kama Maziwe (Pangani) na kupungua kwa barafu katika mlima Kilimanjaro ni baadhi ya mabadiliko ya tabia nchi yanayo ikumba nchi yetu.

Kwa kutambua kuwa suala la mazingira ni muhimu na mtambuka katika kila sekta, kumekuwa na jitihada mabalimbali zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha kuwa utunzaji wa mazingira na madiliko ya tabia nchi yanazingatiwa mfano; kuwepo kwa sheria mahususi kwa ajili ya usimamizi wa mazingira na Kuhakikisha kuwa katika kila sekta kunakuwa kuna kitengo au idara ya mazingira. Kupiga maufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilikuwa inachafua mazingira kwa kiwango kikubwa.

Hata hivyo kumekuwa kuna shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazofanyika na kuathiri mazingira yetu kama kujenga au kufanya shughuli za binadamu karibuna vyanzo vya maji, ukataji wa miti kiholela, na kutekeleza miradi mikubwa ya kiuchumi bila kuwa na tathmini yakinifu ya athari za uharibifu wa mazingira.

#### 5.4.5.3 Tamko la Ilani Kuhusu Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi

Ni wito wa AZAKI kwa viongozi wajao kuhakikisha mambo yafuatayo yanazingatiwa katika kuhifadhi na kutuza mazingira na mabadiliko ya tabia nchi:-

(i) Kuhakikisha kuwa kuna sera mahususi ya mabadiliko ya tabia nchi.

(ii) Kuhakikisha kuwa miradi yote mikubwa yenye athari za moja kwa moja katika mazingira kabla ya utekelezwaji wake tathmini ya uharibifu wa kimazingira inafanywa na kuzingatiwa (EIA).

(iii) Nchi kuheshimu na kutekeleza mikataba mbalimabali ya kimataifa inayohusu utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

(iv) Kuwa na mikakati madhubuti ya kuendelea kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

(v) Serikali na viongizi wajao waheshimu mamlaka za kisheria kama Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kusimamia utunzaji wa mazingira bila kuhafifisha na kutweza jitihada za taasisi hizo katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

(vi) Kuboresha vituo vya ukusanyaji taarifa za mabadiliko ya tabia ya nchi, uchambuzi wa taarifa na ufikishwaji wa taarifa hizo kwa wananchi.

(vii) Kufanya utafiti na kupata taarifa mahususi kuhusu viashiria vya mabadiliko ya tabia ya nchi, athari zake katika uchumi na Maisha ya watu ili kuweka mikakati ya kukabiliana nayo.

(viii) Kujenga uelewa wa wananchi kuhusu mabadiliko ya tabia ya nachi, viashiria na athari zake na kuwashirikisha wananchi katika kuandaa mbinu za kukabiliana na athari za mabadiriko ya tabia ya nchi.

(ix) Serikali kuweka utaratibu wa kisheria na kisera utaowezesha umakini katika kuingia mikataba ya uwekezaji ambayo inatilia maanani utunzaji wa mazingira na maliasili.



Sura ya 6

# USAWA WA KIJINSIA NA MAKUNDI MAALUM

## 6.1 UTANGULIZI

Dhana ya usawa wa kijinsia inahusu mahusiano yaliyojengeka katika jamii kati ya wanawake na wanaume pamoja na makundi mengine. Vipengele muhimu vinavyotofautisha kwa kina dhana hii ni masuala ya ugawaji wa mamlaka, rasilimali, majukumu na nafasi za maamuzi. Aidha, utofauti huu huonekana zaidi katika ngazi ya kaya na jamii na yamerasimishwa katika mifumo ya sera na bajeti na hata mifumo ya kisiasa, mfano kwenye vyama vya siasa, michakato ya uchaguzi pamoja na uteuzi kwenye nyanja mbalimbali za uongozi.

## 6.2 JITIHADA ZA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA KIJINSIA

Kuna jitihada kadhaa zinafanyika katika kupunguza changamoto za masuala ya kijinsia. Kwa mfano, kuna ongezeko la ushiriki wa wanawake katika ngazi za juu za maamuzi, ubunge na udiwani kwa kuongeza nafasi ya viti maalumu kwa wanawake kutoka asilimia 15 hadi asiliamia 30 (Bungeni) na asilimia 25 had asilimia 30% (Udiwani). Kadhalika, uwepo wa WWU na vijana katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Aidha, serikali imepiga hatua katika uwezeshaji wanawake kutokana na uwepo wa sera zinazoelekeza uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake, vijana na WWU; uwepo wa sera ya elimu bila ada; Mpango wa Taifa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), kumechangia kwa kiasi kikubwa ulinzi wa makundi yote, afya kwa watoto na utoaji wa vitambulisho vya matibabu kwa wazee.

> *Azimio la Umoja wa Afrika kupitia Mkataba Nyongeza wa Maputo uliagiza nchi wanachama kufanya marekebisho ya Katiba ili kuweze- sha kufikia 50/50 usawa wa kijinsia katika Uongozi ifikapo mwaka 2015, wakati Aganda 2063 –"Afrika Tuitakayo." Malengo nama 17 na 5 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, yameelekeza ukondoishaji wa usawa wa kijinsia katika maeneo yote ili kuhakikisha wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu, vijana na makundi yote ya pembezoni yanashiriki kikamilifu katika nyanja.*

## 6.3 TAMKO LA ILANI KUHUSU USAWA WA KIJINSIA

AZAKI tunapendekeza kuwa, serikali itakayoingia madarakani:-

(i) Ifanye marekebisho ya Katiba na sheria za uchaguzi na vyama vya siasa ili kuweka utaratibu utakaowezesha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika ngazi za maamumuzi ili kufikia kiwango cha asilimia hamsini kwa hamsini (50% kwa 50%).

(ii) Kuthibiti mfumo unaoruhusu wenye mali kuhodhi madaraka ya kisiasa ambao unadhohofisha demokrasia shirikishi na kuadhiri ushiriki wa wanawake, wanaume na WWU na vijana wenye hali ya chini kiuchumi katika maamuzi ya uongozi wa taifa katika ngazi zote.

(iii) Kuweka utaratibu wa kisheria na kikatiba utakaotoa mwongozo kuwezesha makundi yote ya jamii kama wanawake, WWU na makundi ya pembezoni wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi kama wapiga kura na kama wagombea uongozi wa nyadhifa mbalimbali.

(iv) Kuhakikisha kinga dhidi ya wanawake mbele ya sheria dhidi ya aina zote za usumbufu, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia pamoja na kurekebisha sheria zote kandamizi kama vile Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sheria ya Kimila ya Mirathi ya Mwaka 1963, Tangazo la Serikali GN 436. Pia kutunga Sheria ya Ukatili Majumbani na kuanzisha Mahakama Maalum ya Familia ili kufikia Malengo ya MTAKUWWA ya 2016/17-2021/22.

(v) Kutunga Sheria mahususi ya kuzuia ukatili wa kijinsia majumbani, wakati wa uchaguzi, na katika jamii kwa ujumla na kuanzisha Mahakama Maalum ya Familia ili kufikia Malengo ya MTAKUWWA ya 2016/17-2021/22.

(vi) Kuendelea kusimamia upatikanaji wa haki za wanawake na kupiga vita mila na desturi zinazowabagua au kudhalilisha wanawake na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Mikataba yote ya Kimataifa inayohusu ustawi wa mwanamke.

(vii) Kupiga marufuku matumizi ya lugha za kashfa, matusi, udhalilishaji na aina yoyote ya ukatili wa kijinsia kwenye chaguzi zote ili makundi yote yaweze kushiriki bila kikwazo.

(viii) Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Jinsia na Wanawake ya mwaka 2000, ili kuweka utaratibu wa kisera wa kuboresha Maisha ya wanawake kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Kuendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuboresha huduma zinazofanywa na wanawake hususan katika maeneo ya nishati, usimamizi wa maliasili, kilimo, mwani, maji, na uzalishaji wa bidhaa mbali mbali ili kufikia uchumi wa kati na nchi ya viwanda.

(ix) Kuhakikisha kwamba halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu.

(x) Kwa kuwa wanawake wengi wanapatikana maeneo ya vijijini, na hujishighulisha na sekta ya kilimo na ufugaji, serikali iongeze uwekezaji katika sekta kilimo na kuwawezesha wanawake kupata miondombinu mahususi kwa ajili ya kilimo cha kisasa ili kukabiliana na mabadiriko ya tabia ya nchi.

## 6.4 HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

### 6.4.1 Ufafanuzi – Hali Halisi ya Makundi Maalumu

Haki za makundi maalum ni haki zote zinazojumuisha haki zote za binadamu kama inavyoainishwa kwenye Azimio la Kimataifa wa Haki za Binadamu (10 Disemba 1948) kwa makundi mbalimbali ya watu wanaotakiwa kupewa uangalizi maalum kwa sababu ya hali ya mazingira magumu wanayokutana nayo katika jamii. Makundi haya ni kama vile watoto, vijana, WWU, wakimbizi, wazee, wanawake, wakulima na wafugaji na makundi mengine madogo madogo katika jamii.

Kutokana na utete wa hali ya makundi haya maalumu, imekuwa ni rahisi kwao kunyanyasika kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, mauaji ya watu wenye ualbino na vikongwe nchini. Ulinzi wa kisheria bado haujawa madhubuti hasa kutokana na udhaifu wa usimamizi wa sheria na pia, kuwepo kwa baadhi ya sheria kandamizi dhidi ya wanawake na watoto. Changamoto nyingine kuu ni pamoja na ukosefu wa hifadhi ya jamii kwa wazee na makundi mengine ya pembezoni.

#### 6.4.2 Watu Wenye Ulemavu
#### 6.4.2.1 Tathmini Fupi Kuhusu Upatikanaji wa Haki za WWU

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu na Mkataba wa Nyongeza (2006) umezitaka nchi wanachama, kati ya mambo meninge, kuhakikisha na kuendeleza upatikanaji kamilifu wa haki zote za binadamu na uhuru wa msingi kwa WWU bila ubaguzi wa namna yoyote ile kwa misingi ya ulemavu. Vilevile mkataba huu umeagiza nchi wanachama wanawahakikishia WWU haki za kisiasa na fursa ya kunufaika na haki hizo kwa misingi ya usawa na watu wengine na zitachukua hatua za nchi wanachama zinakubali.

Aidha, serikali na wadau mbalimbali wamekuwa wakisaidia upatikanaji wa huduma kwa WWU ikiwa ni pamoja na kugawa vifaa saidizi kwa WWU, kukomesha mauaji dhidi ya wenye ualbino na kuwashirikisha kwa kuteua WWU katika nafasi za maamuzi (udiwani, ubunge na uwaziri) na nafasi nyingine za kiutendaji, bado tunahitaji kuongeza idadi yao kwenye nafasi mbalimbali ili sauti zao zisikike katika nyanja zote hasa wakati wa kupanga na kugawa rasilimali za taifa kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji/mtaa hadi taifa.

#### 6.4.2.2.Tamko la Ilani Kuhusu Upatikanaji wa Haki za WWU

AZAKI tunapendekeza yafuatayo:-

(i) WWU kuwekewa mazingira wezeshi na jumuishi ya kushiriki katika mchakato wote wa uchaguzi bila vikwazo.

(ii) Vyama vya siasa na wagombea wengine, waepuke lugha za udhalilishaji na ubaguzi kwa WWU ambazo zinaweza kurudisha nyuma ari yao ya kutaka kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa uongozi.

(iii) Fursa za kiuchumi ziongezwe kwa WWU ikiwemo kuwawezesha katika kupata ajira stahiki.

(iv) Kuweka sera na miongozo ambayo itakondoisha masuala ya WWU.

(v) Kuboresha miundo mbinu na kuweka huduma rafiki kwa WWU hasa katika upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii kama afya na elimu. Kwa mfano kuwe na vitengo rasmi vya ukalimani wa lugha ya alama katika idara za afya, polisi na mahakama

(vi) Watumishi wa afya wapewe mafunzo maalum ya lugha ya alama kwenye kusaidia kuwahudumia watu wenye ulemavu wa usikivu.

#### 6.4.3 Uwezeshaji wa Wanawake
#### 6.4.3.1 Tathmini Fupi Kuhusu Upatikanaji wa Haki za Wanawake

Misingi ya kudai haki za wanawake katika ushiriki wao kwenye nafasi za uongozi, unaongozwa na nyenzo mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Katiba ya Zanzibar inahimiza misingi ya usawa, Katiba ya JMT pia imehimiza haki na usawa kwa wote pamoja na kuheshimu kila mtu na kutokufanya ubaguzi kwa mtu yeyote. Mihimili ya kisera ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jinsia na Wanawake ya 2000 na Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia wa 2005. Dira ya SMZ nayo inaainisha kupunguza mapengo kijinsia, na kuimarisha fursa za ushiriki wa watu wote bila ubaguzi.

Dhana ya uwezeshaji wanawake ni mchakato unawawezesha wanawake na wasichana kutambua mazingira ya ukandamizaji na hali duni waliyo nayo katika jamii. Kinachotizamwa katika dhana hii ni ulinzi wa utu na uhuru wa mwanamke ili aweze kushiriki kikamilifu kwenye nafasi za maamuzi, umiliki wa rasilimali, huduma bora za kijamii na kutokomeza ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

#### 6.4.3.2 Tamko la Ilani Kuhusu Uwezeshaji wa Wanawake

AZAKI tunapendekeza:

(i) Kujenga ujuzi na stadi zao ili kuibua na kuchambua sababu zinazosababisha wanawake na wasichana kuwa na hali duni katika jamii.

(ii) Kubadilisha fikra mgando kwa wanawake wenyewe na kwa jamii nzima na kuanza kujiamini na kujithamini.

(iii) Kuwepo kwa nafasi maalum zinazotolewa kwa wanawake au makundi ya kijamii yaliyoachwa pembezoni na si mikakati ya upendeleo kama mitazamo mingi ya kijamii inavyoonesha. Kwa mfano wanawake kushiriki katika maamuzi kwa kupewa nafasi ya kuchaguliwa katika uongozi kupitia viti maalum vya wanawake bungeni na udiwani.

(iv) Kuongezwa uungwaji mkono wa juhudi za wanawake katika ukulima wa mwani, ukulima wa zao la karafuu, kazi za mikono, vikundi vya vikoba na ushiriki wao katika sekta ya utalii Zanzibar kwa kuweka mfuko maalum wa kuwapatia mikopo endelevu na isiyo na riba kubwa kutoka serikalini kupitia wizara ya uwezeshaji, jinsia, wanawake na watoto.

(v) Kuhamasisha ushiriki wa wanawake wa Zanzibar katika mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2020 kutokana na changamoto zilizojitokeza uchaguzi wa mwaka 2015 na ule wa marejeo wa mwaka 2016.

### 6.4.4 Maendeleo ya Vijana

#### 6.4.4.1 Tathmini Fupi Kuhusu Maendeleo ya Vijana

Vijana ni kundi muhimu sana katika ngazi zote za maendeleo na ujenzi wa taifa. Kwa mujibu wa Takwimu za Idara ya Takwimu ya Taifa (NBS) 2012, idadi ya vijana umri kati ya 15 na 35 inakadiriwa kuwa 35% na idadi hii inachangia nguvu kazi ya taifa kwa zaidi ya 60%. Hii ni ishara kwamba taifa lina mtaji mkubwa wa nguvu kazi ambao unatakiwa kuendeleza na kujengewa mazingira wezeshi.

JMT kwa sasa imepiga hatua katika maeneo mbalimbali ikiwemo kuwapa nafasi za maamuzi vijana kama vile ukuu wa mkoa, wilaya, uwaziri n.k. pia uwezeshaji vijana kiuchumi kwa kutenga 4% za fedha zitokanazo na makusanyo ya halmashauri; kuanzishwa kwa Baraza la Vijana Taifa (Zanzibar); na, nafasi za ajira katika sekta mbalimbali.

#### 6.4.4.2 Tamko la Ilani Kuhusu Maendeleo ya Vijana

Katika kudai ushirikishwaji wa vijana katika shughuli zote za kimaendeleo na uwakilishi katika ngazi za ufanyaji maamuzi, AZAKI tunatoa mapendekezo yafuatayo ambayo ni mtambuka kwa vijana:-

(i) Serikali itakayoingia madarakani ihakikishe baraza la vijana taifa linaanza kufanya kazi na pia liwe na maamuzi yake na lisifungamane na itikadi za vyama vya siasa ili liweze kupigania haki na mahitaji ya vijana wote wa kike na kiume.

(ii) Serikali itakayoingia madarakani ihakikishe inatoa elimu ya kujitegemea, kujiajiri na stadi za maisha kwa vijana ili kupunguza wimbi la vijana wengi wasiokua na ajira mitaani.

(iii) Serikali ikamilishe mchakato wa kupitisha sera mpya za vijana iliyotokana na maboresho ya Sera ya Maendeleo ya Taifa ya Vijana ya 2007 (kwa Tanzania Bara) na kwa Zanzibar, kulingana na maboresho ya sera ya mwaka 2005.

(iv) Kuwekewa mazingira wezeshi na shirikishi yatakayoongeza wigo wa vijana wote kushiriki katika mchakato wa uchaguzi.

(v) Kuongeza fursa za kiuchumi kuwawezesha vijana kujitegemea. Kuweka mfumo maalum wa kipato kitakachokwenda katika maendeleo ya vijana kama vile Tanzania Bara walivyopendekeza asilima 4 ya mapato ya halmashauri au ule mfuko wa maendeleo wa vijana uendeshwe kwa uwazi zaidi na uwajibikaji na uwe chini ya wizara ya vijana.

### 6.4.5 Ulinzi na Ustawi wa Wazee

#### 6.4.5.1 Tathmini Fupi Kuhusu Ulinzi na Ustawi wa Wazee

Magonjwa ya mara kwa mara ya muda mrefu, ni hali ya kawaida kwa wazee walio wengi. Hali hii inahitaji uangalizi na matunzo maalum ya kitaalam. Pamoja na ukweli huo, huduma za afya hazipatikani kwa urahisi kwa wazee walio wengi na mara nyingi ni ghali. Utaratibu wa kutoa huduma bure kwa wazee bado una mapungufu.

> *Katika ilani ya AZAKI ya mwaka 2015 suala la wazee lilipendekezwa kwa kuelekeza kuweka mifumo rasmi itakayochangia kupeleka mbele masuala ya wazee ikiwemo kuzingatia stahiki zao, kuthaminiwa na kulindwa dhidi ya ubaguzi uliopo katika jamii. Ilani za vyama karibia vyote vya siasa ziligusia namna ambavyo serikali itawasaidia wazee kupata matibabu bure na kupatiwa pensheni ya uzeeni. Sera ya wazee ya mwaka 2003, imeeleza mambo mazuri juu ya haki za wazee na kutoa maelekezo mazuri kwa serikali na wadau.*

Mauaji na ukatili kwa wazee/ vikongwe vimepungua kwa kiasi kikubwa; uwepo wa mwongozo wa kuwapatia huduma za afya bure; pia baadhi ya wazee wamenufaika na mfuko wa maendeleo wa jamii (TASAF) hasa vijijini. Pia uwepo wa sera ya wazee ya mwaka 2003.

Pamoja na serikali kutunga sera ya wazee mwaka 2003 hadi sasa bado Muswada wa Sheria ya Wazee haujapelekwa Bungeni, kujadiliwa na kupitishwa. Suala hili linasababisha baadhi ya wazee kuishi maisha ya tabu kwa kukosa huduma stahiki.

6.4.5.2 Tamko la Ilani Kuhusu Ulinzi na Ustawi wa Wazee

AZAKI tunapendekeza:-

(i) Serikali itakayoingia madarakani kuhakikisha inapata takwimu halisi za wazee na kuwaunganisha na mifuko ya hifadhi ya jamii.

(ii) Serikali iweke utaratibu wa kutoa elimu na hamasa kwa jamii, juu ya kulea na kulinda haki za wazee katika ngazi ya kaya ili kupunguza kasi ya kuwa na makambi ya kulea wazee.

(iii) Serikali itakayoingia madarakani ihakikishe sera ya kuchangia gharama za afya inafanyiwa mapitio kwa lengo la kurekebisha vigezo vya utambuzi wa umri wa miaka 60.

(iv) Watumishi wa afya wapewe mafunzo maalum ya namna ya kuwahudumia wazee hasa umuhimu wa kuwapa wazee kipaumbele wanapofika vituo vya afya.

### 6.4.6 Ulinzi na Ustawi wa Watoto

#### 6.4.6.1 Tathmini Fupi Kuhusu Ulinzi na Ustawi wa Watoto

Utafiti uliofanywa juu ya ukatili dhidi ya watoto mwaka 2011 unaonesha kuwa takribani mmoja kati ya wavulana saba amekutana na ukatili wa kingono kabla ya kutimiza miaka 18, na kati yao asilimia 71 wamekutana na ukatili wa kimwili. Hata hivyo, utafiti huo unaonyesha kuwa kwa upande wa watoto wa kike, idadi ipo juu zaidi kwa mmoja kati ya watatu na asilimia 72. Licha ya athari wanazopata watoto au wanawake kimwili na kisaikolojia kutokana na vitendo vya ukatili, vitendo hivyo pia vinaathari kubwa sana katika uchumi. Takwimu zinaonyesha, vitendo vya ukatili vinaugharimu uchumi wa dunia kati ya asilimia 3 hadi 8 ya pato lake na kwa Tanzania, zaidi ya billioni 6.5 za kimarekani, ambayo ni sawa na asilimia 7 ya pato la taifa, hupotea.

Matukio ya ukatili kwa watoto yanakua kwa kasi. Kwa mfano kwa kipindi cha mwaka 2018 pekee zaidi ya visa 6,000 vya ukatili au unyanyasaji dhidi ya watoto ikiwemo ukatili kiongono viliripotiwa (LHRC 2018).

Zipo jitihada ambazo zimefanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa haki za wanawake na watoto katika kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni pamoja na kutungwa na kufanyiwa kazi sera na sheria mbalimbali zinazolenga kuboresha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi.

#### 6.4.6.2 Tamko la Ilani Kuhusu Ulinzi na Ustawi wa Watoto

AZAKI tunapendekeza (kwa uongozi na serikali vitakavyoingia madarakani):-

(i) Kufanyiwa marekebisho kwa sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ili itoe ulinzi thabiti kwa mtoto wa kike na kuongeza umri wa kuolewa kwa wasichana kutoka miaka 14 hadi zaidi 18.

(ii) Kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu (ujenzi wa mabweni, huduma za jamii, n.k) ili kuondoa vitendo vya ubakaji, ndoa na mimba za utotoni kwa wanafunzi wa kike.

(iii) Serikali isimamie utekelezaji wa MTAKUWA kwa kila kitongoji, kijiji na kata.

(iv) Serikali ihakikishe watoto wa kike wanaopata ujauzito kutokana na changamoto za kimazingira wanapatiwa fursa na haki ya kuendelea na masomo.

(v) Serikali isimamie afya na mama na mtoto (MCH) ili kupunguza au kuondoa kabisa vifo vya mama na mtoto.

(vi) Serikali ihakikishe inatoa bima ya afya kwa watoto wote kuanzia umri wa mwaka 0 hadi miaka 18 bure.

(vii) Serikali ianzishe vituo vingine vya mkono kwa mkono (one stop centre) kutoka vine vya sasa[1] vilivyopo na kuwa kila mkoa - ili kutoa huduma za afya, ushauri nasihi na msaada wa kisheria kwa wahanga wa ukatili.

### 6.4.7 Maendeleo ya Wakulima, Wafugaji wa Asili na Waokota Matunda

#### 6.4.7.1 Tathmini Fupi Kuhusu Wakulima, Wafugaji wa Asili na Waokota Matunda

Tanzania inashika nafasi ya pili kwa wingi wa mifugo barani Afrika ikiwa na ng'ombe milioni 25, mbuzi milioni 16.7, kondoo milioni 8, nguruwe milioni 2.4, na kuku milioni 36. Kati ya ng'ombe milioni 25 ng'ombe wa asili ni 98%. Hivyo, ni 2% tu ya ng'ombe wote Tanzania wanaofugwa kwa mfumo wa ufugaji wa kisasa (URT, 2015).

1 Mikoa ya Dar es Salaam (Hospitali ya Amana); Shinyanga (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa); Mwanza (Hospitali ya Sekou Toure); Mkoa wa Mjini Maghrib (Hospitali ya Mnazi Mmoja); na, Iringa (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa)

Tafiti zinaonesha kuwa ufugaji wa asili unachangia 7.4% ya pato la taifa na ongezeko la ukuaji la 2.2% kila mwaka. Ufugaji wa asili umethibitika kiuchumi kuwa na ufanisi mkubwa katika matumizi ya ardhi na uhifadhi wa mazingira ufugaji wa asili unategemewa na idadi kubwa ya watanzania kwa kuendesha maisha yao; iwe kwa chakula, mavazi, na maendeleo kwa mapana yake.

### 6.4.7.2 Tamko la Ilani Kuhusu Wakulima, Wafugaji wa Asili na Waokota Matunda

AZAKI tunapendekeza (kwa serikali itakayo ingia madarakani):-

(i) Serikali kuanzia ngazi ya serikali za mitaa hadi taifa kwa kushirikiana na wadau iwe na mkakati wa pamoja wa kuelimisha umma juu ya umuhimu wa amani baina ya makundi yote katika jamii na kulinda haki ya kila mmoja.

(ii) Serikali iweke mazingira mazuri ya kisera, na ya mgawanyo sawa wa rasilimali yanayoruhusu kila sekta kukua bila kuingiliwa au kuzuiliwa na sekta nyingine.

(iii) Serikali isimamie marakabisho ya Sheria ya ardhi wanyama pori na nyingine ziwatambue wafugaji wa asili na mifugo yao kama watanzania wenye uwezo na haki ya kumiliki ardhi.

(iv) Mifugo itambuliwe rasmi kama rasilimali nyinginezo zinazohitaji kupewa haki katika umilikaji na matumizi ya ardhi.

(v) Serikali iandae sera mahsusi ya ufugaji asili itakayosimamia haki na maendeleo ya sekta hii kwani sera ya mifugo iliyopo haikidhi mahitaji ya ufugaji wa asili

(vi) Serikali kwa kushirikisha wadau ifanye mapitio juu ya sera na sheria zinazogusa masilahi ya wafugaji na wakulima ili kubaini maeneo yanayohitaji maboresho katika utekelezaji kwa ajili ya ukuaji wa mfumo mzima wa uzalishaji mali, ustawi wa amani na mshikamano miongoni mwa makundi yote ya jamii.

(vii) Utekelezaji wake ufuatene na serikali kuunda timu itakayojumuisha wataalamu, viongozi wa siasa na wa serikali, asasi za kiraia, wakulima, wafugaji, vyombo vya habari, taasisi za serikali na wawekezaji itakayo baini vyanzo vya migogoro na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuondokana na migogoro ya ardhi

(viii) Serikali ilinde haki za wanawake wafugaji na wakulima ili wanufaike na rasilimali husika kwa kuboresha mazingira ya fufikia, kumiliki na kunufaika na rasilimali ardhi.



## Sura ya 7

# UPATIKANAJI NA UNAFUU WA HUDUMA ZA MSINGI ZA KIJAMII

### 7.1 UTANGULIZI

Upatikanaji na unafuu wa huduma za jamii ni moja kati ya vichocheo vikuu vya uharakishaji wa maendeleo kwa wananchi na hasa mwananchi mmoja mmoja. Huduma za jamii kama maji, afya na elimu zinasaidia kwa kiasi kikubwa kukua kwa uchumi na ustawi wa wananchi kwa uendelevu.

Kwa mujibu wa Katiba, serikali inapaswa kuweka mazingira wezeshi kuhakikisha hudumaza kijamii zinapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu kwa watu wotena kwa wakati. Kwa miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru hali ya utoaji wa huduma za msingi za kijamii umekuwa ukiboreshwa na serikali imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maji, elimu na afya kwenye maeneo yote nchini.

> *Hata hivyo kulingana na ongezeko kubwa la watanzania, wingi wa shughuli za uzalishaji na mabadiliko ya hali ya hewa, hali na wakati tulionao huduma za jamii bado zinaonekana sio za kuridhisha. Changamoto hii inaonekana kuwa kubwa zaidi tunaposhuhudia utofauti wa huduma hizi kati ya maeneo ya vijijini na mijini, na kaya zenye unafuu wa maisha na kaya maskini n.k. AZAKI tunaamini katika kuweka mazingira wezeshi na ya usawa kwenye upatikanaji wa huduma hizi nchini, wananchi wotewanapaswa kushirikishwa katika mipango na mgawanyo wa rasilimali, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma zinazotengwa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za maji, afya na elimu kuanziangaziza chini hadi ngazi zajuu.*

### 7.2 TATHMINI FUPI KUHUSU UPATIKANAJI NA UNAFUU WA HUDUMA

Katika ushiriki wa AZAKI nchini kwenye kuboresha uduma za jamii moja kwa moja na kupitia utetezi kwa niaba ya wananchi zimebainika sababu za wazi ambazo zimekuwa zinasababisha kwa kiasi kikubwa kudorora kwa ufikiwaji wa huduma bora za jamii. Sababu hizo ni pamoja na:

(i) Utengaji wa bajeti ndogo ya serikali kwa ajili ya huduma za jimii.
(ii) Usimamizi mdogo wa pesa kidogo inayotengwa na hivyo kusababisha upotevu wa pesa za umma.
(iii) Kutoshirikishwa kikamilifu kwa wananchi wakati wa kubuni miradi ya huduma za jamii.
(iv) Uelewa mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa huduma hizo kwenye kuharakisha maendeleo.
(v) Mifumo duni ya ufuatiliaji na tathmini juu ya mahitaji halisi ya wananchi kulingana na mabadiliko hali na wakati.

Mpaka sasa serikali haijafanikiwa kutoa huduma moja wapo kwa kiwango kizuri kulingana na mahitaji halisi ya wananchi. Kwa wakati wote na maeneo yote ya nchi, wananchi wamekuwa wakilalamikia ukosefu wa maji safi na salama; changamoto ya elimu na miundombinu; pamoja na huduma za afya zisizoridhisha.

### 7.3 UFAFANUZI WA ILANI KUHUSU UPATIKANAJI NA UNAFUU WA HUDUMA

#### 7.3.1 Upatikanaji wa Huduma ya Elimu

##### 7.3.1.1 Mafanikio

Kati ya maadui watatu wa taifa waliotajwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa JMT moja wapo ni ujinga. Maadui wengine ni umasikini na maradhi. Watafiti, wataalamu wa masuala ya maendeleo ya jamii na wadau wa elimu wamebainisha wazi elimu ndiyo silaha madhubuti ya kumaliza kwa haraka maadui maradhi na umasikini, hivyo kufanya elimu kuwa ukombozi wa maisha ya mwanadamu kwenye nyanja mbalimbali. Aidha, haki ya elimu ni haki ya msingi ya binadamu na ni haki muhimu kwa maendeleo. Haki hii inahamasisha uhuru na uwezo wa mtu binafsi katika kujiletea maendeleo.

> *Mwaka 2015, AZAKI kupitia Ilani ya Uchaguzi ya AZAKI ilibainisha hali na changamoto za elimu hapa nchini na kutoa tamko juu ya namna bora serikali inayoweza kuimarisha upatikanaji na unafuu wa elimu kwa wote. Kati ya mambo yaliyobainishwa ni pamoja na ukosefu wa miundombinu ya kutosha kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo, ukosefu wa vitabu vya ziada na kiada, vifaa vya kufundishia na mazingira magumu ya kazi na usimamizi mbovu wa sekta ya elimu.*

Kwa kipindi cha utawala wa awamu ya tano AZAKI imebaini namna ambavyo serikali imeendelea kuonyesha jitihada za kuboresha elimu nchini na kuweka mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa wote na hasa kuwezesha watoto kutoka kaya masikini kujiunga na masomo kupitia sera ya elimu bila malipo na ufadhili wa elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Aidha, serikali imeonyesha nia ya kuboresha miundombinu ya elimu kwa kufanya ukarabati mkubwa wa shule kongwe 88 nchi nzima. Mazingira haya wezeshi kwenye sekta ya elimu imepelekea uandikishwaji wa watoto wa shule za msingi kuongezeka kwa asilimia 46.1 kutoka 1,069,823 mwaka 2015 hadi kufikia 1,562,770 mwaka 2016.

##### 7.3.1.2 Changamoto

Pamoja na jitihada hizi za serikali bado sekta ya elimu imeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Uchache wa miundombinu kama vyumba vya madarasa, maabara, maktaba, vyoo na nyumba za walimu.
(ii) Ufinyu wa bajeti ya elimu na kutotolewa kwa fedha zilizokwishapitishwa.
(iii) Ukosefu wa walimu wenye sifa na wakutosha.
(iv) Ukosefu wa vitabu vya ziada na kiada na vifaa vya kufundishia.
(v) Usimamizi mbovu wa sekta ya elimu, kuwepo kwa sera tata ya lugha ya kufundishia na kujifunza na mtaala usioendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknologia na hivyo kufanya kundi kubwa la wahitimu kutoongeza uzalishaji kwa taifa kwa kushindwa kujiajiri au kukidhi viwango vya soko la ajira.

##### 7.3.1.3 Tamko la Ilani ya Kuhusu Elimu

AZAKI tunapendekeza (kwa serikali itakayo ingia madarakani):-

(i) Serikali kufanya utafiti na tathmini ya hali ya ubora wa elimu nchini kulinganisha na hali ya dunia katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kiteknolojia na hivyo kuja na sera na mitaala mpya na kuweka mikakati endelevu ya kuboresha kiwango cha elimu kwa manufaa ya watanzania wote.

(ii) Serikali iboreshe utoaji wa elimu katika shule za umma ili kupunguza utofauti wa ubora wa elimu kwa shule za umma na binafsi, pamoja na shule za mjini na vijijini.

(iii) Kuongeza bajeti ya elimu na kufikia asilimia 20 ya bajeti nzima ya serikali ili kuendana na mahitaji yake ya sasa na pesa inayotengwa inapelekwa kwa asilimia 100.

(iv) Serikali ianze kuongeza na kuboresha miundombinu ya elimu iendane na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na masomo kupitia mpango muhimu wa elimu bila malipo.

(v) Serikali inachukulia kwa umuhimu wake madai ya walimu ya muda mrefu yasiyo ya mishahara na madeni yanayotokana na mishahara, na kuweka mazingira mazuri ya kulipa walimu stahiki zao kwa muda muafaka.

(vi) Serikali kwa msingi wa sera ya elimu iweke mkazo juu ya kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa wote na hivyo kuondoa vikwazo vinavyozuia fursa ya mwanafunzi kuendelea na masomo na hivyo kukamilisha mzunguko na kuhakikisha usawa wa kijinsia katika elimu na mafunzo unazingatiwa.

(vii) Serikali iweke utaratibu wa kufanya utambuzi wa awali wa watoto wenye ulemavu ili kuhakikisha kuwa wanapanga na kuwapatia elimu inayoendana na mahitaji yao.

(viii) Kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanakwenda kwa kupiga vita ajira kwa watoto wenye umri wa kuwa shule.

(ix) Serikali iweke mfumo madhubuti wa kupima kiwango cha umahili wa wanafaunzi katika kila ngazi ya elimu kwa kuzingatia mitaala iliyopo ili kujua kiwango cha ujifunzaji cha wanafunzi.

(x) Serikali iboreshe utolewaji wa elimu ya awali kwa kuandaa walimu wa kutosha, kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia.

(xi) Kuifanya shule kuwa mahali salama na rafiki ili kumwezesha mtoto kupenda shule na kujifunza kwa ufanisi.

(xii) Kuboresha mishahara na maslahi ya walimu na kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa walimu kwa shule za sekondari na msingi.

(xiii) Serikali iangalie upya mgongano wa sheria zinazominya fursa ya mtoto wa kike kupata elimu. Baadhi ya sheria hizo ni pamoja na zinazochangia mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri mdogo.

(xiv) Mfumo imara na rahisi kwa wanafunzi wanaodahiliwa vyuo vikuu kupatika udhamini wa masomo yao bila ya masharti magumu. Pia, kuweka pia mfumo ambao ni rafiki wa wanafunzi kama vile kushusha vigezo vya ufadhili kulingana na ufaulu wa wanafunzi katika kiwango cha kitaifa au kuondoa vigezo vya mikopo kwa yeyote mwenye sifa za kujiunga na elimu ya juu.

(xv) Mfumo wa udahili wa vyuo vikuu (TCU) uwe na utaratibu wa kubadilisha viwango vya udahili kwa baadhi ya kozi ili kuwezesha fursa zaidi kwa wanfunzi kujiunga na elimu ya juu.

### 7.3.2 Upatikanaji na Unafuu wa Huduma za Afya

#### 7.3.2.1 Jitihada za Kuboresha Huduma za Afya

Tokea uhuru serikali ya Tanzania imekuwa ikifanya jitihada za kuboresha huduma za afya kwa kutumia rasilimali za ndani na kutoka kwa wahisani. Kwa hatua hiyo, imefanikiwa kujenga vituo vya afya na zahanati sambamba na ununuzi wa dawa na vifaa tiba na hatua mbalimbali za kuendeleza na kuboresha huduma za afya nchini.

Jitihada nyingine zimekuwa ni kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa inayoelekeza nchi wanachama kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa kutenga bajeti ya ndani. Mfano, Tanzania ni miongoni

mwa nchi zilizosaini makubaliano ya Abuja ya Kutenga 15% ya jumla ya bajeti yake kwenda sekta ya afya; na imekuwa ikitekeleza sera na mikakati mbalimbali mfano Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya (HSSP 1V). Hizi zote ni jitihada za serikali kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi kwa kuongeza vituo vya afya, idadi ya watumishi na kuboresha miundo mbinu kwenye ngazi ya halmashauri, mkoa na taifa.

### 7.3.2.2 Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Afya kwa Sasa

Katika Ilani ya Uchaguzi ya AZAKI Tanzania 2015 ilipendekeza mambo kadhaa kuzingatiwa ikiwa ni pamoja na kuongeza bajeti ya afya inayoendana na mahitaji wa wananchi. Hii ilitokana na ukweli kwamba serikali imekuwa ikitenga bajeti ya afya ndogo na haikidhi mahitaji ya wizara na hivyo bajeti ya afya kutegemea fedha ya wahisani ambayo mara nyingi huchelewa kufika au kutoingia kabisa nchini kutokana na masharti ambayo yanapelekea kuathiri utolewaji wa huduma za afya.

Katika mazingira hayo, upatikanaji na unafuu wa huduma za afya nchini imekuwa ni changamoto. Zahanati na vituo vya afya vilivyoko kwa wananchi vinakosa dawa za kutosha na vifaa tiba, uchache wa watumishi wa kada mbalimbali, uchakavu wa miundombinu na wafanyakazi kukosa motisha. Hali hii kiujumla inasababisha kudorora kwa huduma muhimu ya afya ambayo ni haki ya binadamu na waathirika wakubwa ni watoto, wazee na mama wajawazito ambao wamepatiwa msamaha lakini hawapati dawa kwenye vituo vya afya.

Hata hivyo serikali iliyopo madarakani imejitahidi kwa kiasi kikubwa sana katika kuboreha huduma za afya nchini. Kwa mfano katika kipindi cha miaka mine ya serikali ya awamu ya tano, tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta ya afya. Mpaka kufikia Julai 17, mwaka 2018, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu ilitamka kua iliishajenga vituo vya afya 108 na ililenga kumalizia vingine 68 katika mwaka wa fedha wa 2018/2019. Pia serikali imefanya maendeleo makubwa katika kuboresha upatikanaji wa madawa, vifaa tiba na wataalamu wa afya katika hospitali nyingi nchini.

### 7.3.2.3 Tamko la Ilani Kuhusu Huduma za Afya

AZAKI tunapendekeza (kwa serikali itakayo ingia madarakani):-

(i) Serikali itenge fedha za kutosha kwenye bajeti kwaajiliyasektaya afya ili kuwezesha upatikanaji na unafuu wa huduma za afya; bajeti iendane na Makubaliano ya Abuja ya kutenga 15% ya bajeti nzima ya serikali ya mwaka husika.

(ii) Serikali ianzishe Bima ya Afya ya lazima na iliyoboreshwa kwa wote ambayo itasaidia kupunguza pengo la fedha na kurahisisha matibabu kwa wananchi.[2]

(iii) Serikali itekeleze sera ya msamaha wa matibabu kwa ufanisi kwenye makundi yaliyopewa kipaumbele yaani watoto chini ya umri wa miaka mitano, wazee, mama wajawazito na wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, tofauti na sasa ambapo pamoja na kuwepo kwa msamaha huo bado kuna malalamiko makubwa ya kukosekana dawa kwenye hospitali Kuu, Vituo vya Afya na Zahanati.

(iv) Serikali itoe ajira za kutosha kwa watumishi wa afya kwa kada mbalimbali kulingana na mahitaji halisi na hasa maeneo ya vijijini; na madaktari bingwa kwenye hospitali za mikoa zote kama ya watumishi idara ya Afya inavyoelekeza (Mfano: Watumishi 15 kwenye ngazi ya zahanati n.k).

2 Hii iendane sambamba na ufatiliaji wa utoaji wa huduma za afya kwa wenye bima bila usumbufu kwani kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa watumiaji wa bima ya afya kuwekwa kama wapewa huduma wa daraja la pili baada ya wale wanaofanya malipo ya moja kwa moja.

(v) Serikali inachukulia kwa umakini bajeti ya Wizara ya Afya kwa kutenga kiasi kinachokidhi mahitaji ya watanzania na hasa masikini, na fedha inayotengwa ifikishwe kwenye wizara hiyo kwa 100% ili kufanikisha utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali kwa ukamilifu.

(vi) Serikali inaonyesha utashi wa kutosha kwenye kushughulikia tatizo sugu la uhaba na uchakavu wa miundombinu ya msingi kwenye hospitali zote za umma na hususani zilizoko vijijini.[3]

(vii) Viongozi watakaohakikisha WWU wa ngozi (albinism) wanapata vifaa vya kujikinga na magonjwa na mionzi kama vile mafuta maalum ya ngozi na miwani ya jua.

(viii) Serikali inasimamia kikamilifu matumizi sahihi ya bajeti ya Afya na hasa ngazi ya halmashauri itumike kwa matumizi yaliyokusudiwa; kamati za usimamizi wa vituo vya afya zijengewe uwezo wa kusimamia uwazi na uwajibikaji kwenye wa idara ya afya.

(ix) Serikali itoe kipaumbele kwa utoaji wa huduma rafiki kwa vijana kwa kuongeza vituo vya utoaji huduma hizo pamoja na vitendea kazi.[4]

### 7.3.3 Upatikanaji na Unafuu wa Huduma za Maji Safi na Salama

#### 7.3.3.1 Ufafanuzi Kuhusu Maji Safi na Salama

Upatikanaji na unafuu wa maji safi, na salama kwa wote ni sehemu na hitaji muhimu la ulimwengu tunayotaka kuishi. Kuna maji safi ya kutosha duniani ili kufikia hitaji hili. Lakini kwa sababu ya uchumi au miundombinu mibaya, kila mwaka mamilioni ya watu, wengi wao wakiwa watoto, hufa kutokana na magonjwa yanayohusiana na ukosefu wa maji ya kutosha.

Mazingira yenye ukosefu wa maji au maji yasiyokuwa na ubora huathiri vibaya usalama wa chakula, uchaguzi wa maisha na fursa za elimu kwa familia masikini nchini Tanzania.

#### 7.3.3.2 Jitihada za Upatikanaji wa Huduma za Maji

Tangu uhuru, serikali ya Tanzania imekuwa ikijitahidi kuboresha huduma za jamii zinazohusishwa na wananchi wengi kama huduma za maji; kutokana na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na bajeti tegemezi, rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma ngazi ya serikali kuu na serikali za mitaa, ndoto hii bado haijafikiwa.

Serikali ya sasa kupitia kampeni na mkakati wake unaojulikana kama "mtue mama ndoo kichwani" imeonyesha kuweka tahadhari ya pekee juu ya tatizo la maji nchini Tanzania. Kampeni hii inasisitiza na kuonyesha jinsi wanawake wanavyokabiliwa na changamoto zitokanazo na ukosefu wa huduma za maji katika maeneo na hivyo kurudisha nyuma juhudi za wanawake kuchangia maendeleo ya kitaifa na ukombozi wao kiuchumi.

Katika kusimamia mkakati huo serikali ya awamu ya tano kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo AZAKI Tanzania tumebaini utashi wa kuendelea kuongeza bajeti ya ndani kwenye sekta ya maji kwa kiasi kikubwa, kwa mfano mwaka 2017/2018 ilitengwa Bilioni 648.01 na mwaka 2018/2019 ilitengwa bilioni 727.35 sawa na ongezeko la bilioni 79.[5]

3 Mfano ukosefu wa nyumba za watumishi, umeme, maji ya uhakika, mashimo ya kutupia kondo la nyuma la uzazi, vichomea taka na matundo ya vyoo ya kutosha.

4 Hii itasaidia kujenga taifa lenye vijana wenye afya bora na wenye kuleta maendeleo kwa kasi hasa kwa kuzingatia hitaji la uchumi wa viwanda.

5 Kadhalika, serikali imeendelea kufanya maboresho ya kisera, kisheria na kimfumo kwenye wizara ya maji na tayari imepitishwa sheria mpya namba 5 ya mwaka 2019 ya huduma za maji na usafi wa mazingira. Aidha, zimeonekana juhudi za wazi za kusimamia kwa ukaribu na kufufua miradi ya maji vijijini na mijini na Mamlaka za maji kuongeza uwajibikaji, usimamizi wa karibu na ukarabati wa miundombinu ya maji ili kuokoa upotevu wa maji.

### 7.3.3.3 Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Maji kwa Sasa

Suala la umuhimu wa maji kwa wananchi wa Tanzania halina mjadala. Ni wazi kwamba sehemu zote zilizofikiwa na miundo mbinu ya maji safi na nafuu wananchi wa maeneo hayo wameweza kuboresha ustawi wao katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na magojwa ya milipuko. Kwa kuzingatia umuhimu huo Mwaka 2015 AZAKI Tanzania kupitia Ilani ya Uchaguzi, kwa niaba ya wananchi, tulibainisha namna ambavyo serikali inapaswa kutatua tatizo sugu la ukosefu wa maji safi na ya kutosha maeneo ya mijini na vijijini.

Pamoja na jitihada za awamu hii kupitia Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) katika kusimamia miradi ya maji, kufufua miradi iliyotelekezwa kwa miaka mingi, kuongeza bajeti na kuboresha muundo na mfumo wa usimamizi wa wizara, bado kiwango cha upatikanaji na unafuu wa huduma za maji ni duni sana.

Wananchi wameendelea kutembea umbali mrefu kutafuta maji, wengine kuamka usiku wa manane kuchota maji na hivyo kupoteza muda mwingi kutafuta huduma hii muhimu. Aidha, kwenye maeneo yaliyofikiwa na miundo mbinu ya maji bado kuna usimamizi mbaya kiasi cha kushindwa kufanya ukarabati wa miundombinu na kupelekea upotevu wa maji bila sababu ya msingi.

Aidha, serikali imeshindwa kuchukua hatua ya kuvuna maji ya mvua inavyotakiwa kupitia mabwawa na matenki maeneo ya vijijini kwenye majengo ya kutolewa huduma kama shuleni, hospitalini na maeneo mengine ya umma yanayohitaji maji kwa wingi. Kwa sababu ya Umuhimu wa maji kwenye kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu AZAKI tunasema Maji ni Uchumi, Ustawi na Afya. Hivyo, serikali inawajibu wa kuweka mikakati madhubuti ya kimfumo na kibajeti kumaliza tatizo la maji kwa wananchi wa Tanzania.

### 7.3.3.4 Tamko la Ilani Kuhusu Huduma za MAJI

Kwa kuwa tunajua umuhimu wa maji kwenye maisha ya wananchi wetu AZAKI kwa niaba ya wananchi tunahitaji:

(i) Kuona serikali inatenga bajeti ya kutosha kwa kutumia pesa za ndani kujenga miundombinu maeneo ya vijijini yaliyosahaulika kwa muda mrefu na meneo mengine ya utolewaji wa huduma za afya na elimu.

(ii) Serikali kuweka mazingira ya upatikanaji wa huduma hii kwa unafuu zaidi tofauti na iliyo sasa. Maji yasiwe bidhaa bali huduma muhimu kwa wananchi wote maeneo yote.

(iii) Serikali iendelee kuona umuhimu na kulipa kipaumbele suala la utunzaji wa mazingira na udhibiti wa vyanzo vyote asili vya maji.

(iv) Tunahitaji kuona serikali inaongeza udhibiti kwenye upotevu wa pesa za umma zinazoelekezwa kwenye wizara ya maji, kuanzia serikali kuu na serikali za mitaa kwani utengaji wa bajeti kubwa hauwezi kuzaa matunda kama udhibiti na uwajibikaji wa watendaji wa serikali hautasimami kikamilifu.

(v) Kuona serikali inashirikiana na sekta binafsi kuboresha huduma za maji nchini.

(vi) Serikali kupitia serikali za mitaa, iweke kipaumbele kwenye kujengea uwezo wananchi kulinda na kuendeleza miundombinu ya maji inayotekelezwa kwa pesa za umma au wahisani, na kulinda vyanzo vyote vya maji vilivyopo.



Sura ya 8

# AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO WA TAIFA

## 8.1 UTANGULIZI

Tokea muungano kuasisiwa mwaka 1964, JMT inatambulika kuwa ni kisiwa cha amani na utulivu katika bara zima la Afrika. Jamhuri hii ya Tanzania inaendelea kuwa na nafasi ya juu katika suala la amani duniani na hata kushika nafasi ya kwanza katika nchi za Afrika mashariki (Global Peace Index) 2017 na 2018. Nchi hii imefanikiwa kutokomeza matukio ya ujambazi wa kutumia silaha katika maeneo mbali mbali. Kutokana na utulivu huu, JMT imekuwa ni kimbilio na kivutio cha wageni wengi ikiwa ni pamoja na wahitaji kama vile wakimbizi kutoka nchi za jirani.

Ili kuendelea kusifika kuwa nchi ya amani inahitaji mikakati na mbinu jumuishi katika misingi ya mshikamano kutatua changamoto kwenye suala la amani, usalama, umoja na mshikamano wa taifa. Hivyo, ili kuwa na taifa imara lenye uchumi usioyumba tunawataka viongozi kuwekeza nguvu zaidi kwenye kuimarisha na kulinda amani, usalama, umoja na mshikamano ili kujenga taifa lenye upendo na kuheshimiana.

## 8.2 MWENENDO WA AMANI, USALAMA NA UMOJA WA KITAIFA

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zenye misingi ya amani, usalama, umoja na mshikamano wa taifa, nchi ambayo imeaminiwa na umoja wa mataifa katika ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali zenye migogoro. Kubwa zaidi la kujivunia na namna serikali imeweza kudhibiti matendo ya wizi na ujambazi wa kutumia silaha; utekaji wa magari; na, uvunjaji wa maduka pamoja na mabenki matukio ambayo yametokomezwa kwa ustadi mkubwa wa vyombo vya dola kwa ushirikiano na wananchi.

Pamoja na hayo serikali kwa kushirikiana na AZAKI imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutatua migogoro ya rasilimani kama ya migogoro ya wakulima na wafugaji katika mikoa mbalimbali nchini. Ni jambo la kijivunia kama taifa kuwa na uwezo kutatua migogoro ya ndani kwa njia ya mazungumzo hakika ni hatua na sifa kwa taifa.

Hatahivyo, hivyo, hivi karibuni yamejitokeza matukio mbalimbali ya uvunjifu wa amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa. Matukio ambayo yamegusa wabunge wa vyama vyote, wananchi, waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu, wanasiasa, wanamuziki wakitekwa, kupigwa na kuumizwa, na hata kuuawa. Matukio haya yameathiri amani kwa kiasi kikubwa sana kama inavyofafanuliwa zaidi hapa chini.

Migogoro ya wakulima na wafugaji imeendelea kuripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, migogoro ya kisiasa, ubaguzi, chuki na mgawanyiko baina ya viongozi wa kidini wenyewe kwa wenyewe, viongozi wa kidini na serikali, pamoja makundi ya waharifu kuibuka kama yale ya eneo la Kibiti mkoani

Pwani, pamoja na migogoro ya kijamii kama ukosefu wa ajira kwa vijana nchini. Lakini pia limeibuka wimbi la jeshi la polisi kutumia nguvu kubwa na mabavu katika kushugulikia wanachama wa vyama vya siasa na hasa wa vyama vya upinzani. Uminywaji wa demekrasia katika chaguzi ndogo mwaka 2018, kuendelea kuzuia mikutano ya vyama vya siasa wakirukuhusu vyama vingine kufanya siasa jambo ambalo linaonesha upendeleo katika vyama.

> *Hata hivyo kulingana na taarifa hizo za Wizara na taarifa zingine, ikiwemo taarifa zilizokusanywa kutoka vyombo vya habari, kuanzia mwaka 2016 mpaka mwezi Julai 2019 jumla ya matukio 86 ya utekaji yaliripotiwa. Kati ya waliotekwa watoto ni 23 na watu wazima ni 63. Kati ya hao 86 wengine wamerudi, wengine wamekutwa wamekufa na wengine hawajulikani walipo hadi sasa akiwemo mwandishi wa habari za kiuchunguzi, Azory Gwanda.*

## 8.3 UFAFANUZI ZAIDI KUHUSU AMANI, USALAMA NA UMOJA

### 8.3.1 Amani Katika Taifa

Amani ni hitaji kubwa katika maisha ya binadamu na taifa lolote duniani. Binadamu hawezi kupata maendeleo ya kweli ambayo pasipo amani. Na amani haipatikani pasipo haki. Utulivu uliopo Tanzania ni kielelezo cha kinachotambulika kuwa ni kisiwa cha amani, hii inatokana na uvumilivu mkubwa wa watanzania ambao bado wamebeba upendo, utu na kuheshimiana.

Hivyo ni vyema amani ikatunzwa, ikalindwa na kudumishwa kwa maendeleo ya taifa hili. Iko haja kuchukuwa hatuwa madhubuti kuondoa woga na hofu waliyonayo watanzania kwamba hawana uhuru wa kutoa maoni.

Wanahitajika viongozi wanaothamini na kujenga maridhiano kwa kukubali kuzungumza na kuelewana kwa maslahi ya nchi. Kwa mfano:-

(i) Kazi kubwa iliyofanyika Zanzibar baina ya Rais wa Zanzibar wakati huo Mheshimiwa Amani Abeid Karume kutoka CCM na Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad kutoka CUF kwa kukaa pamoja na kuacha tofauti zao ambazo zilichukua miongo kadhaa ya kuendesha siasa za chuki na uhasama.[6]

(ii) Juhudi za Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa mchakato wa Katiba mpya alifanikiwa kujenga maridhiano na vyama vya upinzani ili kuhakikisha umoja wa kitaifa unalidwa kwa misingi ya haki na usawa.

Kunahitajika kiongozi atakayeweza kulinda na kutetea haki za watanzania wote bila ya kujali rangi, dini wala ukabila au itikadi za vyama vya siasa. Kiongozi ambaye pia anayeweza kushughulikia kero za muungano na usawa katika kumaliza yale yote yanayolalamikiwa pande zote mbili za Muungano. Hatua hiyo itaongeza upendo na Mshikamano baina ya wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar kwani msingi mkuu wa Muungano ni mashirikiano na umoja wa nchi hizo.

### 8.3.2 Usalama Katika Taifa

Tanzania ni moja ya nchi zinazotambulika kuwa na usalama wa hali ya juu Afrika na duniani kwa ujumla. Pamoja na heshima hiyo tuliyonayo hali imeingia dosali kwani katika siku za karibuni, kumekuwa na masuala kadhaa ya watetezi wa haki za binadamu, waandishi wa habari, wafanyabiashara, wanasiasa na wasanii kutekwa, kuteswa na hata kuuawa, pasipo hatua madhubuti kuchukuliwa dhidi ya ulinzi na usalama wao.

6 Maridhiano yao kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar ambayo ilimaliza hasama kati ya vyama viwili vikuu na wafuasi wao.

Mara kadhaa kumeripotiwa taarifa za watu kutekwa au kupotea katika mazingira ya kutatanisha, ambayo yamekuwa yakihatarisha hali ya usalama na kuzua taharuki miongoni mwa wananchi. Katika taarifa iliyotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhe Kangi Lugola, mnamo tarehe 14 mwezi Oktoba mwaka 2018 jumla ya matukio 75 ya utekaji yaliripotiwa tangu mwaka 2016.

Vilevile, kumejitokeza matukio ya kutisha zaidi pale ambapo hadi vituo vya polisi navyo vinakuwa ni wahanga wa hali hii kwa kuchomwa moto na baadhi ya askali kudaiwa kuuawa na watu waovu maeneo ya Kibiti, Pwani na kwingineko. Haya ni baadhi tu ya matukio na viashiria vya kuteteleka kwa usalama.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, ni jukumu la jeshi la polisi kulinda amani. Jeshi hili linaweza kutimiza vyema jukumu hili kwa kushirikiana na majeshi mengine na raia wote. Hivyo, ni lazima kwa jeshi hili kuendelea kufanya kazi kwa weledi na hasa kujiepusha na upendeleo wowote ule hasa zinazotokana na misukumo ya itikadi za kisiasa.

### 8.3.3 Tamko la Ilani Kuhusu Amani, Usalama, Umoja na Mshikamano

Ili kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa kisiwa cha amani, AZAKI tunawataka viongozi wote kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:-

(i) Wawajibike kuwajibisha vyombo vya dola kulinda ipasavyo na bila upendeleo raia wote na mali zao.

(ii) Kuundwe chombo jumuishi cha maridhiano ya kitaifa ambacho kitatambuliwa rasmi kwa mujibu wa katiba kama kile cha Afrika ya Kusini na serikali iweke utaratibu wa kuwa na vikao vya maridhiano kujadiliana suala la amani, usalama, umoja na mshikamano wa taifa kila inapotokea stafahamu miongoni mwa viongozi na jamii.

(iii) Kuundwe chombo cha kusimamia weledi wa jeshi la polisi nchini ili lifanye kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi kulinda watu, mali na amani nchini.

(iv) Kuhuisha sera na sheria zinazokinzana katika kulinda na kudumisha amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa.

(v) Katiba iwe na Ibara inayoweka na kusisitiza ulinzi, amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa.

(vi) Viongozi walazimike kuchukua hatua za makusudi ili kulinda haki za AZAKI, watetezi wa haki za binadamu, waandishi wa habari, wafanyakazi wa afya, wanaharakati wa kisiasa na watu wote kwa mujibu wa katiba ya Tanzania.

(vii) Vyombo vya ulinzi na usalama Tanzania vihakikishe kuwa kila raia anaishi kwa uhuru, usalama na amani nchini.

(viii) Mbinu za kutatua migogoro ya ndani zirejewe upya kuona wapi tumekosea ili kuziimarisha na kuendelea kufanikisha kutatua na kumaliza migogoro yote kwa njia ya mazungumzo na maridhiano.



## Sura ya 9

# TANZANIA NA DIPLOMASIA YA KIKANDA NA KIMATAIFA

### 9.1 UTANGULIZI

Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania imekuwepo na kurekebishwa kwa miaka mingi. Sera kama hiyo duniani kote hutekelezwa kupitia diplomasia. Kushamiri au kuyumba kwa lolote katika hayo mawili huweza kufifisha mahusiano ya nchi na washirikika wa nje (jumuiya au mashirika ya kimataifa). Wataalamu wa diplomasia husema kuwa diplomasia kwa taifa ni kama ulivyo ubongo kwa binadamu. Haiwezekani kukipuuza chochote katika hivyo - kwa sababu hiyo, diplomasia hubeba kila eneo la sera za kidunia.

### 9.2 SERA MPYA YA MAMBO YA NJE YA TANZANIA

Sera mpya yaTanzania ya Mambo ya Nje ilichapishwa kwa mara kwanza mwaka 2001 na kuhuishwa mwaka 2015. Sera hii mpya inatambua kuwa msisitizo mkubwa wa mahusiano ya Tanzania kimataifa kwa miaka yote kabla ya sasa ulikuwa ni diplomasia ya kisiasa. Katika eneo hili, sera inakiri kuwa kumekuwepo mafanikio makubwa sana. Sera mpya pia inabainisha kuwa Sera ya zamani ya mambo ya nje iliegemea mno siasa na kusahau malengo ya kiuchumi. Kwa kutambua hilo, sera mpya ya mambo ya nje inalenga kutekeleza diplomasia ya uchumi.

> *Kimkakati, sera mpya inalenga kutekelezwa kwa namna mbili. Kwanza, kupitia njia ya mahusiano ya kimaendeleo ambapo Tanzania itakuwa na kuendeleza mahusiano yake na nchi moja moja na mashirika ya kimataifa katika kusukuma gurudumu la maendeleo mbele. Pili, kupitia mahusiano ya Tanzania na nchi za kusini (South – South Cooperation), Tanzania inajipanga kutumia jina lake zuri na uzoefu mkubwa ilioonesha katika nyanja za kisiasa kuimarisha mahusiano ya kiuchumi kati yake na nchi za uchumi wa kati na masikini duniani. Hii ni pamoja na kuendeleza na kuimarisha mahusiano yake na nchi ya China ambayo wa sasa imepiga hatua kubwa kimaendeleo.*

Sera mpya ya mambo ya nje inabainisha misingi muhimu kama vile:-

(i) Kulinda uhuru na mipaka ya Tanzania pasipo hiyana.
(ii) Ulinzi wa haki za raia, haki za binadamu, usawa na demokrasia.
(iii) Ujenzi wa ujirani mwema.
(iv) Kuendeleza na kutetea umoja wa Afrika.
(v) Kuendeleza na kuimarisha mahusiano mema na wahisani na wafadhili.
(vi) Kuunga mkono uendelezaji wa sera ya kutofungamana na upande wowote wa kisiasa duniani.
(vii) Kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa katika kutafuta maendeleo ya kiuchumi, amani na usalama duniani kote.

Kikanda, Tanzania ni mwanachama mwanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); Jumuiya ya Soko la Pamoja Kusini mwa Afrika (COMESA); na, Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu, kwa uchache. Kutokana na mchango wake wa kidiplomasia siku na miaka iliyopita, jumuiya ya kimataifa inaichukulia na kuitegemea Tanzania kuendelea kutoa mchango katika maendeleo na mijadala ya masuala mbalimbali yanayotokea katika ujirani wetu. Hata bila mafanikio makubwa sana, Rais wa zamani wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin Mkapa wa Tanzania ameweza kusaidia sana mazungumzo ya amani na hali ya baadaye ya Burundi na ukanda wa maziwa makuu. Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi pia amekuwa tegemeo kuwa kuongoza tafakari ya hali ya baadaye ya Sudan, kupitia mchakato wa Kitaifa ujulikanao kama National Dialogue.

Aidha, hivi karibuni zaidi, aliyekuwa Rais mwingine wa JMT Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete naye amekuwa tumaini kubwa katika kujaribu kuraghbisha mazungumzo ya amani nchini Sudan ya Kusini kati ya mahasimu wakuu, Rais Salva Kiir na Riek Machar. Nje ya Sudan kusini, Rais Kikwete amefanywa kuwa kiongozi wa michakato kadhaa barani Afrika ikiwemo kama mkuu wa waangalizi wa uchaguzi wa Umoja wa Afrika katika nchi mbalimbali barani. Haya yote yanatokana na mchango mkubwa ambayo Tanzania imetoa miaka kwa miaka mingi.

## 9.3 MUELEKEO WA KUNUFAIKA KUPITIA DIPLOMASIA YA UCHUMI

Kwa mujibu wa dira ya Maendeleo ya Taifa, Tanzania itafikia uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo mwaka 2025. Ingawa lengo hili ni zuri na kupongezwa, kumekuwa na kukosekana kwa uelewa wa pamoja juu ya namna ya kufikia lengo hilo zuri lakini kubwa na zito.

Kumekuwa na hoja kuwa utahitajika mfumo wa kuwianisha dhana ya uchumi wa viwanda kwa upande mmoja, na diplomasia ya uchumi (ambayo inahusu uzalishaji na uuzaji) na demokrasia ya kisiasa (ambayo ni pamoja na usafirishaji bidhaa na mahusiano mengine ya kimaamuzi kuhusu kinachozalishwa nchini). Pasipo urari wa mambo hayo, ndoto ya uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025 inaweza kuwa ndoto mfu.

> *AZAKI tunataka kuwepo kwa mjadala wa kitaifa kuhusu mwelekeo wa diplomasia na mahusiano ya kimataifa na kikanda Tanzania. Hii itahusisha na kufikia makubaliano juu ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika kudumisha uchumi wa viwanda nchini na mahusiano yake kimataifa na kikanda.*

Pasipo maelewano ndani kwa ndani, ipo hatari ya kupata wazalishaji watakaohamasika kuzalisha pasipo fikra ya wapi watauza ikizingatiwa kuwa kuwapoka wazalishaji au wauzaji wa mazao asili wa miaka mingi kunaweza kudhoofisha soko la bidhaa za Tanzania duniani. Hii imekaribia kutokea kwenye soko la Korosho, Tanzanite na dhahabu. Suala kama la Tanzania kutaka kurejewa kwa miakaba yake ya madini na makampuni ya uwekezaji ni ishara ya udhaifu mkubwa wa wataalamu waliosaini mikataba hiyo na linatikisa diplomasia ya Tanzania kiuchuni.

## 9.4 UWAKILISHI WA NCHI KATIKA MIKUTANO YA KIKANDA NA KIMATAIFA

Sambamba na diplomasia ya Kisiasa, limeibuka ombwe katika uwakilishi wa Tanzania kwenye vikao na michakato mbalimbali ya kikanda na kidunia. Kwa mfano, mchakato wa tathmini ya hali ya Haki za Binadamu Kidunia (UPR) umeshuhudia Tanzania ikisuasua katika miaka ya hivi karibuni katika kutoa taarifa husika.

Aidha,Tanzania imepeleka wawakilishi wa nyadhifa za chini kama mabalozi au mawaziri katika vikao vikubwa kama Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, vikao vya kikanda kama SADC na vinginevyo. Ingawa uwakilishi si jambo baya kabisa, ngazi ya mwakilishi anayeongoza jopo la serikali kwenye mkutano au mchakato fulani wa kimataifa huonesha umuhimu ambao nchi husika inaupa mkutano au mchakato husika.

AZAKI tungependa kuona kuwa Rais atakayechaguliwa katika uchaguzi wa mwaka 2020 aweze kutoa kipaumbele kikubwa kwa diplomasia na mahusiano ya kimataifa. Aidha, Bunge la Tanzania liondoe suala la Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia kutoka kwenye fungu na Kamati ya Ulinzi, Usalama na Mambo ya Nje ili kuliweka huru suala mambo ya nje kwa watanzania wote kuweza kuchangia hoja na maoni.

## 9.5 UTEKELEZAJI WA MAKUBALIANO NA MIKATABA YA KIMATAIFA

Ingawa msingi wa kimataifa wa mamlaka kamili ya nchi (territorial sovereignty) inaruhusu nchi yoyote ikiwemo Tanzania kuweza kufanya maamuzi yoyote ya ndani, mahusiano bora ya kimataifa yanazitaka nchi husika kufanya hivyo kwa kuzingatia na kuheshimu sheria, mikataba na matamko mbalimbali ya kimataifa.

Ukiukaji wa sheria za kimataifa hususani katika eneo la mikataba ya uwekezakaji umewahi na unaendelea kuigharimu Tanzania mabilioni ya pesa za kigeni hadi suluhu ya mambo hayo ipatikane. Mfano wa miaka ya karibuni ulikuwa ni kushitakiwa kwa Tanzania katika chombo chenye hadhi ya mahakama ya uwekezaji wa kimataifa kiitwacho ICSID. Ingawa Tanzania ilishinda keshi hiyo kwa msaada wa marafiki wa mahakama (amicus) kutoka Tanzania na nchi nyinginezo, gharama iliyotumika kujitetea ilikuwa kubwa sana.

Aidha, endapo wawekezaje wa City Water Services wangeshinda, Tanzania ingeweza kulipa gharama kubwa za mabilioni ya fedha za kigeni kama fidia. Hivi karibuni zaidi, kushikiliwa kwa baadhi ya ndege za Shirika la ndege la Tanzania huko Canada kulileta sokomoko hadi mazungumzo yalipofanyika kuhusu deni la Tanzania kwa wawekezaji wa Stabag. Hivi karibuni pia, mkasa kama huo wa kushikiliwa kwa ndege ya Tanzania umetokea nchini Afrika ya Kusini.
Mwenendo huu si mzuri kwa diplomasia ya nchi.

Kwa ujumla, diplomasia inaweza kuwa nyezo muhimu ya kuwezesha watanzania kushiriki katika uchumi wa dunia.

## 9.6 TAMKO LA ILANI KUHUSU DIPLOMASIA

AZAKI tunataka:-

(i) Viongozi watakaochaguliwa mwaka 2020 kuheshimu makubaliano, mikataba na maazimio mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

(ii) Baraza jipya la mawaziri kuanzia 2020 kuagiza Wizara ya Mambo ya Nje kuongeza juhudi za utafutaji fursa mbalimbali zilizoko duniani na barani Afrika na kuwatafuta watanzania walio na sifa za kumudu fursa hizo lengo likiwa kuwawezesha watanzania kuchukua fursa hizo.[7] Hii itaongeza uwakilishi wa Tanzania katika taasisi na vyombo vya kimataifa.

(iii) Utekelezaji wa Azimio la Malabo ambalo linazitaka nchi wanachama wa umoja wa Afrika (AU) kutenga bajeti inayofikia kiwango cha asilimia 20% ambayo haijafikiwa na Tanzania.

(iv) Utekelezaji wa Azimio la Abuja ambalo linataka Nchi za Afrika bajeti ya sekta ya Afya isipungue asilimia 15% ya bajeti ya Taifa.

(v) Serikali ya Tanzania iipe tasnia ya mahusiano ya kimataifa na diplomasia heshima na uzito inayostahili badala ya kuibeza na kuibagaza.

(vi) Kuwe na juhudi za makusudi kwa Serikali ya Tanzania kushirikiana na AZAKI kurejesha hadhi na heshima ya Tanzania kimataifa.

(vii) Serikali ya Tanzania isaini na kuifanyanyia kazi mikataba muhimu ya kimataifa ambayo inajenga mifumo imara ya kidemkrasia, uwazi na uwajibikaji kama vile mkataba wa Maputo na mkataba wa Uchaguzi, Demokrasia na Uendeshaji.

7 Nchi kama Nigeria, Ghana, Kenya na Rwanda zimeamua kuhamasisha wananchi wake kuzijua na kuzikamata fursa hizo, ziwe ni ajira, uwekezaji na hata internships.



## Sura ya 10

# UHURU WA KUJIELEZA, KUJUMUIKA NA KUKUTANA

### 10.1 UTANGULIZI

Katika taifa lenye misingi ya kidemokrasia na haki za binadamu ni muhimu kuzingatia haki za msingi za kujieleza, kujumuika na kukutana. Ni katika haki hizi wadau mbalimbali wakiwemo wadau kutoka kwenye AZAKI, vyombo vya habari, watetezi wa haki za binadamu, vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla wanaweza kujumuika. Kujumuika huwezesha watu kupata fursa ya kushauriana na kutoa maoni mfano kuhusu maendeleo ya kitaifa. Ili taifa lolote ile liweze kusimamia misingi ya haki za binadamu na utawala bora, ni lazima haki hizi zitamalaki.

Ilani ya AZAKI ya mwaka 2015 ilibainisha matakwa ya wananchi kuhusu haki ya kujieleza, kujumuika na kukutana ambayo ililenga hasa kuboresha mazingira ya AZAKI ziweze kufanya kazi kwa uhuru. Isistizwe tena kuwa, AZAKI zimekuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa. Aidha, AZAKI zimekuwa mstari wa mbele kutetea haki na maslahi ya watanzania wote.

> *Hata hivyo, mchango wa AZAKI haujaweza kutambulika sana na pia, uwepo wa AZAKI haujapewa kipaumbele kama wadau muhimu wa maendeleo katika Taifa hili. Uhuru wa AZAKI kufanya kazi zao umekuwa pia ukipata vikwazo vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa sheria kandamizi; vizuizi vya kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo; changamoto za ulinzi wa haki za binadamu, utawala bora na uwajibikaji kiujumla.*

### 10.2 UHURU WA KUTETEA, KUDAI NA KULINDA HAKI ZA BINADAMU

Uhuru wa kutetea, kudai na kulinda haki za binadamu ulielezwa kwa kifupi katika Ilani ya Uchaguzi ya AZAKI ya mwaka 2015. Ilani iliwataka viongozi walioingia madarakani kusimamia misingi itakayowawezesha watetezi wa haki za binadamu/ AZAKI kufanya kazi ya kutetea na kulinda haki pasipo na vikwazo.

Msingi wa uwepo wa uhuru wa kutetea, kudai na kulinda haki za binadamu unatoka katika Katiba ya JMT ya mwaka 1977 pamoja na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu la 1998. Kati ya Ibara muhimu zinazotoa uhuru wa kutetea na kulinda haki za binadamu kwenye Katiba ni Ibara ya 26(2). Ibara hiyo inasema kila mtu ana wajibu ya kulinda Katiba ya nchi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa kisheria. Hata hivyo, hadi sasa hakuna sheria iliyotungwa kwa ajili ya kuwalinda watetezi wa haki za binadamu Tanzania.

#### 10.2.1 Hali ilivyo kwa sasa kuhusu Uhuru wa Azaki

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita zimekuwepo jitihada za kupitisha sheria na miongozo mbalimbali kuhusu usiamizi na utendaji wa AZAKI na hata vyama vya siasa. Lengo limetajwa kuwa ni kuboresha utendaji kazi wao na vilevile, kuratibu uwepo wao. Lakini sheria na miongozo hiyo imekuja na vifungu vinavyominya kwa kiasi kikubwa uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukutana.

Utungwaji wa sheria na miongozo hiyo (ilitajwa katika sura nyingine za Ilani hii) umedhorotesha kwa kiasi kikubwa jitihada za AZAKI katika kuchangia maendeleo ya nchi hasa kutokuwa huru kufanya shughuli zao mfano za kitafiti kwa hofu ya sheria ngumu kama vile ya takwimu.

Jitihada za AZAKI kujikwamua kutoka katika hali ya sasa ya uwepo wa sheria kandamizi kwa shughuli zao bado hazijazaa matunda na hata baada ya kutumia njia ya Mahakama kudai kubatilishwa kwa baadhi ya vifungu vya sheria kandamizi.

### 10.2.2 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kudai Haki, Kutetea na Kulinda Haki za Binadamu

Ili kuhakikisha maendeleo ya nchi yetu katika nyanja zote za maisha ya binadamu, ni lazima haki zao za msingi ziheshimiwe kwani ni wajibu wa kikatiba na sio takwa na mtu binafasi au taasisi fulani. Hivyo ni lazima AZAKI na watetezi wa haki za binadamu kwa ujumla wapewe uhuru wa kudai haki, kutetea na kulinda haki za binadamu. Ili haki hizo ziweze kupatikana yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa katika mchakato wa kuwapata viongozi hao (watakaochaguliwa):-

(i) Viongozi wazingatie umuhimu wa kutambua na kulinda uhuru wa kudai kaki, kutetea na kulinda haki za binadamu.
(ii) Viongozi wawe mstari wa mbele kwenye kuwa na ujasiri wa kudai haki, kutetea na kulinda haki za binadamu kwa vitendo.
(iii) Wawe tayari kufanyia marekebisho au kuondoa kabisa sheria mbalimbali zinazokandamiza uhuru wa kudai haki, kutetea na kulinda haki za binadamu.
(iv) Wawe na ujasiri wa kukemea baadhi ya viongozi wanaotumia nyadhifa zao kukandamiza na kuzuia utekelezaji wa kazi za AZAKI na watetezi wa haki za binadamu katika maeneo yao bila kusukumwa na itikadi Fulani.
(v) Viongozi watakaoshirikisha AZAKI na watetezi wa haki za binadamu katika mipango mbali mbali ya maendeleo na kuthamini michango yao kwa ustawi wa jamii na taifa.

## 10.3 UHURU WA KUTOA MAONI NA KUSHAURI

### 10.3.1 Hali ya Uhuru wa Kutoa Maoni na Kushauri

Katiba za JMT na Zanzibar zote kwa pamoja zinatoa uhuru kwa kila mtu wa kushauri na kutoa maoni kwa mambo yeyote ambayo mtu ana maslahi nayo na yenye maslahi kwa taifa pia.

Hali ilivyo kwa sasa inaonyesha kuwa, uhuru wa kukosoa, kutoa ushauri na maoni juu ya mambo yenye maslahi kwa taifaa umeshuka kwa kiasi kikubwa. Watu walio mstari wa mbele katika kukosoa na kuishauri serikali wamekua wakipata changamoto nyingi. Miongoni mwao wapo wanao kamatwa, kuwekwa mahabusu kwa muda mrefu bila kupata dhamana na kufuguliwa mashtaka yasiyokuwa na dhamana kama vile uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha haramu.

> *Aidha, kama ilivyosemwa hapo awali, zipo baadhi ya sheria ambazo kwa namna moja au nyingine zinaweka miongozo kuhusu namna ambayo wananchi wanaweza kutoa maoni yao kuhusu masuala muhimu yenye maslahi kwa taifa. Baadhi ya sheria hizo zinaminya uhuru wa wanahabari na vyombo vya habari kwa ujumla. Kupitia sheria zilizopitishwa ndani ya miaka mitano iliyopita, zikiwemo Sheria ya Habari ya mwaka 2016; Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015; na, Sheria ya Takwimu, uhuru wa kutafiti, kukusanya na kutoa taarifa umebinywa sana.*

Vilevile, kumekua na vikwazo vingi katika utekelezaji haki za kupata taarifa na kutoa maoni. Vyombo vya habari kwa sasa vinafanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kutokuwa na uhuru wa kutosha. Kwa mfano, baadhi ya vyombo vya habari vimepewa adhabu kali ikiwemo kusimamishwa kwa muda, kufunguwa, kutozwa faini na wakati mwingine waandishi habari kufunguliwa mashitaka ya kijinai.

Hatari nyingine walizokumbana nazo wanahabari ni pamoja na vitisho, kupigwa, kutekwa na kukamatwa bila sababu za msingi. Katika mwaka 2018 pekee yaliriporiwa matukio 19 ya matukio ya vitisho, utekwaji, kupigwa na wakati mwingine kufunguliwa mashtaka ya kupikwa.

### 10.3.2 Jitihada Zilizochukuliwa Kumaliza Tatizo Hili

Pamoja na kwamba waandishi wa habari, AZAKI na wadau mbalimbali wamekua mstari wa mbele kuomba marekebisho ya vifungu mbalimbali vya sheria vinavyoathiri haki hizi muhimu, bado viongozi hawajaonyesha utayari wa kufanya marekebisho muhimu ya sharia hizi.

Pia, baadhi ya viongozi wamekua wanarudi nyuma katika suala hili la marekebisho ya sheria za habari. Aidha pia baadhi ya watoa maamuzi wanahisi suala la marekebisho ya sheria (za habari au nyenginezo) zinawahusu zaidi serikali na hivyo AZAKI huwa na nafasi ndogo; na, huwekewa vikwaazo katika kutoa maoni yao. Bila shaka, jitihada kubwa zaidi zinahitajika ili kuboresha sheria zilizopo katika hali ambayo hakuna utashi wa kisiasa kufanya hivyo kwa haraka.

### 10.3.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kutoa Maoni Mbalimbali

Ili kuhakikisha maendeleo ya nchi yetu katika nyanja zote za maisha ya binadamu, ni lazima haki zao za msingi ziheshimiwe kwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Viongozi watakaochaguliwa wazingatie umuhimu wa kutambua na kulinda uhuru wa kutoa maoni, kushauri na kadhalika juu mambo yenye maslahi kitaifa.

(ii) Wawe tayari kufanyia marekebisho au kuondoa kabisa sheria mbalimbali zinazobinya uhuru wa kukosoa, kutoa ushauri na maoni juu mambo yenye maslahi kitaifa.

(iii) Kukemea baadhi ya viongozi wanaotumia nyadhifa zao kukandamiza na kuzuia wananchi katika kutoa maoni yao na kukosoa juu ya mambo yenye maslahi kwa taifa letu.

(iv) Viongozi watakaoshirikisha AZAKI, watetezi wa haki za binadamu na makundi yote ya wananchi katika mipango mbali mbali ya maendeleo na kuthamini michango na mawazo yao katika kujenga nchi yetu.

(v) Viongozi watakaokua tayari kutetea uhuru wa habari na kukemea baadhi ya viongozi wanaotumia nyadhifa zao kukandamiza na kuzuia wananchi katika kutoa maoni yao, na kukosoa juu ya mambo yenye maslahi kwa taifa.

(vi) Suala la uhuru wa uhariri (editorial independence) halina budi kupewa kipaumble katika vyombo vya habari vyote viwe vya serikali au binafsi. Aidha kuzinagatia kwa vitendo maadili ya taaluma ya habari na kufanya kazi kwa weledi na umahiri.

(vii) Umuhimu wa kuvumiliana unatakiwa iwe agenda ya juu katika kukosoa.[8]

(viii) Kauli za chuki ambazo zinahatarisha amani na umoja wa wananchi hazina budi kuachwa hususan na viongozi wa kisiasa katika majukwaa yao ya kampeni na mikutano ya hadhara.9

8 Viongozi wanatakiwa wakosoe kwa lengo la kujenga jamii iliyo bora. Hivyo uvumilivu wa kisisasa unahitajia kwa hali ya juu na kukosoana bila ya kugombana. Haki ya watu kutaa mawazo iheshimiwa na kuthaminiwa.

9 Ni muhimu kwa viongozi kijikita katika kueleza sera, dhimana wajibu kuliko kuanza kueleza masuala ya matusi na kauli za chuki ambazo

### 10.4 UHURU WA KUJUMUIKA NA KUFANYA SHUGHULI ZA KIRAIA NA KISIASA

#### 10.4.1 Hali ya Uhuru wa Kujumuika na Kufanya Shughuli za Kiraia na Kisiasa

Kwa mujibu wa sheria za kimataifa, kikanda na Katiba ya JMT, serikali inapaswa kuheshimu haki na uhuru wa wananchi kuweza kujumuika na kufanya shughuli zao za kiraia na kisiasa.

Sera ya Uchaguzi ya AZAKI ya mwaka 2015 ilieleza juu ya Tanzania Tunayoitaka kuhusu haki za binadamu ikiwemo haki ya kujumuika na kufanya shughuli za kiraia na kisiasa. Sera iliwataka viongozi waliokua wakiingia katika uchaguzi kwa wakati huo kuhakikisha wanawapa nafasi wananchi kuweza kukusanyika na kufanya kazi zao za kiraia na kisiasa kwa mujibu wa Katiba ya JMT.

Hata hivyo kupitia sheria mbalimbali, kumekua na uminyaji wa haki hii ya kujumuika. Kwa mfano sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi inatumika vibaya kuwanyima wananchi haki yao ya kujumuika. Pia sheria zingine zinazoongoza mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya siasa zimeongeza changamoto nyingi katika utekelezaji wa shughuli za kiraia na kisiasa.

> *Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002 ikisomwa kwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2005 na 2019 imeweka mazingira magumu ya kufanya shughuli za kiraia. Kwa mfano Kifungu cha 4 cha sheria hiyo kinampa mamlaka Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) kuagiza vyombo vya usalama kuingilia utendaji wa AZISE muda wowote. Hii ni mamlaka kubwa aliyopewa msajili ambayo inaweza kuleta madhara makubwa katika utendaji wa AZISE husika.*

Aidha, zipo pia Kanuni za Sheria ya MAshirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa na marekebisho yake yam waka 2018. Kanuni hizi zimeongeza ugumu katika utendaji kazi wa AZISE. Kwa mfano kifungu cha 13 kimeweka masharti magumu ya utoaji wa taarifa. Kifungu hicho kinazitaka AZISE kutoa ripoti kuhusu kiasi cha fedha kilichokusanywana kuziweka katika magazeti na vyombo vya habari mara mbili kw amwaka. Matakwa haya pamoja na mengine mengi yameendelea kukandamiza uhuru wa kufanya shughuli za AZISE nchini.

Kuhusu haki za kisiasa, hivi karibuni serikali na Bunge la JMT walipitisha mabadiliko ya sheria ya Vyama vya Siasa mwaka 2019. Kati ya masuala mengine, mabadiliko hayo yameongeza vipengele vingi vianavyokandamiza haki za kisiasa. Kwa mfano kifungu cha 5B cha sheria hiyo kinampa nguvu, Msajili wa Vyama vya Siasa kuomba na kupewa taarifa yeyote ile ya chama chochote cha siasa. Afisa yeyote wa chama cha siasa ambaye ataenda kinyume na matakwa ya kipengele hicho, atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia atapigwa faini ya kuanzia shilingi milioni moja mpaka milioni kumi au kifungo kisichopungua miezi 6 na kisichozidi miezi 12. Pia vipo vifungu vinavyompa mamlaka makubwa Msajili huyo ikiwa pia ni pamoja na kumpa kinga dhidi ya mashtaka.

Pia kumekua na matamko ya mara kwa mara ya viongozi wa serikali yanayozuia wananchi kujumuika. Moja ya matamko hayo ni maagizo ya Mkuu wa Nchi kupiga marufuku mikutano ya vyama vya siasa alihali chama kimoja kikionekana kufanya mikutano hiyo pahala mbalimbali hapa nchini.

#### 10.4.2 Jitihada Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto Hizo

Pamoja na kwamba AZAKI, vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla wamekua mstari wa mbele kuomba marekebisho ya vifungu mbalimbali vya sheria vinavyoathiri haki hizi muhimu, bado viongozi (mamlaka husika) hawajaonyesha utayari wa kufanya marekebisho muhimu ya sheria hizi.

---

zinahatarisha usalama wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Pia, baadhi ya viongozi wamekua wakiendelea kutoa matamko yanayoashiria uminywaji wa haki hii ya kujumuika.

### 10.4.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kujumuika

Ili kuhakikisha utekelezaji na usimamizi mzuri wa haki ya kujumuika nchini ni muhimu mambo yafuatayo yazingatiwe ipasavyo:-

(i) Tunataka viongozi watakaochaguliwa wajiepushe kutoa kauli na kufanya vitendo vinavyoweza kukandamiza haki za wananchi kuweza kujumuika na kufanya shughuli zao za kiraia na kisiasa kwa maslahi mapana ya taifa.
(ii) Viongozi wawe tayari kufanyia marekebisho au kuondoa kabisa sheria mbalimbali zinazokandamiza uhuru wa Kujumuika na kufanya shughuli za kiraia na kisiasa.
(iii) Viongozi wawe na uwezo wa kulinda, kutetea na kukemea waziwazi vitendo vya vya baadhi ya mamlaka za serikali na vyombo vya usalama kuzuia haki ya wananchi kujumuika.

## 10.5 UHURU WA KUFANYA TAFITI NA KUTOA TAARIFA MBADALA

### 10.5.1 Hali ya Uhuru wa Kufanya Tafiti na Kutoa Taarifa Mbadala

AZAKI na wadau mbalimbali wamekua wakifanya kazi nzuri katika kufanya tafiti na kutoa taarifa ambazo husaidia kwa kiasi kikubwa katika nyanja mbalimbali za maisha na maendeleo ya watanzania wote. Zipo tafiti mbalimbali zinazofanywa katika sekta ya elimu, afya, uchumi, sheria, haki za binadamu, uatwara bora na maeneo mbalimbali ya kijamii ambayo kwa ujumla wake zina lengo moja la kutafuta masuluhisho yatakayosaidia katika maendeleo ya taifa.

Tafiti na kutoa taarifa ni kiungo muhimu katika utekelezaji wa haki ya kupata taarifa. Msingi wa tafiti hizi ni haki za kupata taarifa na kutoa maoni ambayo inatambuliwa kikatiba chini ya Ibara ya 18 ya Katiba JMT ya 1977. Kwa mujibu wa Ibara hiyo 'kila mtu ana haki ya kupata taarifa zinazohusu maisha yake na zile zinazohusu jamii.'

Tafiti na utoaji wa taatifa zimekua zikiongozwa na sheria nyingi kulingana na aina ya tafiti husika. Baadhi ya sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Tume ya Sayanzi na Teknolojia ya 1979 na kanuni zake; Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015; na, Sheria ya Habari ya 2016. Sheria hizi na zinginezo kwa ujumla wake zina baadhi ya vifungu vinavyominya uhuru wa kufanya tafiti na kutoa taarifa kama ilivyotamkwa katika sehemu nyingine za Ilani hii.

### 10.5.2 Jitihada Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto Hii

Zipo hatua chache zilizochukuliwa na serikali ya awamu ya tano katika kuleta mabadiliko ya kweli katika sheria hizi ili kuhakikisha uhuru wa kufanya tafiti na kutoa taarifa. Kwa mfano June 2019 serikali amebadilisha vifungu vichache katika sheria ya Takwimu. Kuna dhana kuwa, mabadiliko hayo yalitokana na msukumo wa Benki ya Dunia. Kiujumla, bado viongozi hawajaonyesha utayari wa kufanya marekebisho muhimu ya sheria hizi.

### 10.5.3 Tamko la Ilani Kuhusu Uhuru wa Kufanya Tafiti na Kutoa Taarifa Mbadala

AZAKI tunataka viongozi watakaochaguliwa:-

(i) Wawe na utayari wa kuboresha mazingira ya ufanyaji wa tafiti, ikiwa ni pamoja na kufanya mabadiliko ya sheria zote zinazoleta ukakasi katika ufanyaji wa tafiti na utoaji wa taarifa.

(ii) Watambue kuwa kufanya tafiti na kutoa matokeo ya tafiti hizo kwa mujibu wa katiba yetu sio dhambi, kwani tafiti hizo hulenga kurekebisha au kuchangia katika maendeleo ya taifa.

### 10.6 MASUALA MENGINE KIUJUMLA

AZAKI tunataka viongozi watakaochaguliwa:-

(i) Wazingatie umuhimu wa kutambua na kulinda nafasi ya AZAKI na watetezi wa haki za binadamu kama wabia muhimu wa maendeleo na utawala bora wenye kuzingatia sheria katika taifa.

(ii) Wawe tayari kufanyia marekebisho au kuondoa kabisa sheria mbalimbali zinazokandamiza uhuru wa AZAKI, watetezi wa haki za biandamu na vyama vya siasa hapa nchini.

(iii) Kukemea baadhi ya viongozi wanaotumia nyadhifa zao kukandamiza na kuzuia utekelezaji wa kazi za AZAKI katika maeneo yao.

(iv) Watakaoshirikisha AZAKI katika mipango mbali mbali ya maendeleo na kuthamini michango ya AZAKI kwa ustawi wa jamii na taifa.

(v) Watakaotoa uwakilishi wa AZAKI katika vyombo vya maamuzi kama Bunge bila kupitia chama chochote cha siasa.[10]

(vi) Heshimu misingi ya demokrasia na hivyo kuruhusu vyama vya siasa kujumuika na kufanya kazi zao kwa uhuru na kwa mujibu wa Katiba ya JMT na ile ya Zanzibar.

10 Mfano Rais kutumia madaraka yake ya uteuzi wa wabunge kumteua mwakilishi wa AZAKI asiyefungamana na chama chochote.

Sura ya 11

# UWEKEZAJI NA ULINZI WA MATUMIZI YA TEHAMA

## 11.1 UTANGULIZI

Tanzania ni sehemu ya udunia ambao sasa unatambulika kuwa ni kijiji (global village). Hivyo, masuala mengi ya haki za binadamu na hata Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanatokea kwingineko duniani yanaathiri hali halisi ya nchi hii.

> *Jitihada mbalimbali zimefanyika kuhakikisha ukuaji wa TEHAMA nchini. Hizo ni pamoja na uwepo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (National ICT Broadband Backbone). Mkongo huo umesaidia kushuka kwa gharama za intaneti kutoka shilingi 36,000 hadi shilingi 9, 000 kwa 'Gb' kufikia mwaka 2013. Aidha, mkongo wa taifa:-*

*(i) Umesaidia kuharakisha usambazaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara.*

*(ii) Umewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano na uwezo wa kusafirisha masafa.*

*(iii) Imesaidia kushusha gharama za maunganisho ya mawasiliano ya simu za mkononi kutoka kampuni moja kwenda nyingine (interconnection fees) ambapo sasa gharama imepungua kutoka TZS 115 hadi shilingi 34.92 kwa dakika.*

*(iv) Umesaidia kuongeza ushirikiano wa kikanda kati ya nchi za Afrika Mashariki na kati ambapo nchi za Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi, Uganda, na Kenya ambapo hali hiyo imeongeza fursa za kibiashara na kukuza uchumi wa nchi.*

Karne hii ya 21 ni ya sayansi na teknologia ambayo, imegubikwa na matumizi ya TEHAMA. Matumizi hayo ni fursa na changamoto pia kwa wakati mmoja. Hivyo, ni muhimu sana kuyaakisi katika Ilani hii.

Kwa upande wa Zanzibar serikali imeweka Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Miradi na Rasilimali za TEHAMA Serikalini (GIP) na kusisitiza taasisi za umma kuweka taarifa za miradi yao ya Tehama iliyopo kwenye mipango, miradi inayoendelea na iliyokamilika kwenye Mikataba ya kikanda inayolenga kuendeleza na kukuza sayansi na teknolojia kama vile (2063-the Africa We Want), SDGs na Dira ya Taifa 2025.

## 11.2 BAADHI YA FAIDA YA TEHAMA KWA JAMII

Kwa upande mwingine TEHAMA imezalisha mitandao ya kijamii ambayo inatoa fursa ya watu kuweza kujadiliana kuhusu masuala ya siasa, uchumi, afya, biashara na mambo kadha wa kadha ya kijamii. Fursa hiyo inaruhusu mawasiliano baina ya mtu au watu kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Faida ya matumizi ya mitandao ya kijamii inadhihirika si tu kwa wafanyabiashara na vijana bali pia katika Wizara na taasisi za serikali, AZISE na makampuni mbalimbali nchini ambapo wahusika wanatumia mitandao ya kijamii kuimarisha, kurahisha na kuwezesha mawasiliano kwa kuwa na kurasa na mitandao husika.

Aidha ukuaji na maendeleo katika TEHAMA kumesaidia kwa kiasi kikubwa katika suala zima za kufanya miamala ya fedha. Kwa sasa, watu hawalazimiki kutembea na kiasi kikubwa cha fedha taslimu. Badala yake wamekuwa wakitunza fedha katika simu zao za mkononi. Mfumo huu umesaidia kuokoa muda kwa wahusika na hivyo kupata nafasi ya kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

Kwa mujimu wa takwimu za toka TCRA za mwaka 2018, Tanzania ina watumiaji wa mtandao milioni 23. Wengi wao wakiwa vijana hasa wanaoishi maeneo ya mijini.

### 11.3 TAMKO LA ILANI KUHUSU TEHAMA KIUJUMLA

AZAKI tunataka kuwa, serikali na uongozi utakaoingia madarakani izingatie:

(i) Kuweka kipaumbele kwenye eneo la TEHAMA. Serikali ingalie kwa umakini mkubwa jinsi gani inaweza kuzitumia kwa tija, fursa katika eneo hili na kujenga mifumo ya uzalishaji na kuhamasisha uwekezaji kwa watu wote wanaogundua teknolojia mbalimbali.

(ii) Kuweka mfumo mzuri utakaosaidia kupungua kwa gharama za miamala kwa njia ya simu.

(iii) Kuwekeza katika kutafuta takwimu kwa kutumia TEHAMA.

(iv) Kubuni mazingira maalum ya biashara na viwanda kwa kutumia TEHAMA.

(v) Majukwaa ya TEHAMA yanaweza kutumika kama fursa kwa kushirikishana ujuzi na kujifunza mambo mbalimbali kama vile kufanya biashara, kilimo, uvuvi, useremala ikiwa ni pamoja na kujifunza masuala mbali mbali kutoka katika kila kona ya dunia.

(vi) Ihakikishe inaajiri zaidi watu mwenye ujuzi na uwezo wa kiufundi kwa kupelekwa, kusimamia na kudumisha vifaa TEHAMA, programu na mifumo stahiki, ili iweze kufanya kazi vizuri kwa watumiaji.

(vii) Ihakikishe inatunga sheria maalum ya ulinzi wa taarifa za watumiaji wa TEHAMA nchini.

### 11.4 UHURU NA ULINZI WA MATUMIZI YA TEHAMA

#### 11.4.1 Hali Ilivyo Sasa

Kama ilivyobainishwa hapo juu, TEHAMA ni muhimu sana hasa katika ustawi wa taifa na maendeleo ni watu. Hivyo basi, kunahitajika ulinzi wa taarifa za mtu binafsi bila kulazimishwa kutoa kwa nguvu au kuibiwa. Lazima uwepo utaratibu wa kupata taarifa binafsi kwa kufuata sheria (due process). Uhuru wa kuelezea, kuandika habari na matukio yoyote kwa kuzingatia taratibu na sheria bila kuogofya kuangalia nyuma ya bega ni muhimu kwa utawala bora na ustawi wa watu katika ubunifu.

Kwa sasa, uhuru wa matumizi ya TEHAMA umekua ni mdogo,hasa kwa kufungiwa kwa baadhi ya vyombo vya habari. Aidha, ulinzi wa wabunifu katika TEHAMA umekua ni mdogo sana hadi kupelekea baadhi ya watu kua na woga wa kusema kile walichokibuni ili taifa linufaike, huku pia wakihofia kukamatwa.

#### 11.4.2 Tamko la Ilani Kuhusu Ulinzi na Matumizi ya TEHAMA

AZAKI tunataka, serikali itakayoingia madarakani:-

(i) Isimamie na kuhakikisha uhuru wa matumizi ya TEHAMA bila vikwazo.

(ii) Ilinde usiri wa mawasiliano na taarifa za watumiaji wa mtandao na mitandao ya kijamii na kuwapa watu uhuru wa kutumia mitandao ya kijamii na teknolojia bila kuogopa kuwa mawasiliano au taarifa zao zinaweza kudukuliwa au kwenda kwenye mikono isiyo sahihi.

(iii) Ihakikishe ulinzi zaidi wa ubunifu kwa watu wote wanaobuni vitu mbali mbali, kuwapa nafasi na kuwawezesha ili wafanye mambo makubwa zaidi.

(iv) Serikali ifufue muswada wa sheria ya ulinzi wa usiri na taarifa binafsi (wa 2014) na kutunga use sheria ili kuhakikisha ulinzi wa usiri na taarifa za watumiaji wa TEHAMA nchini.

(v) Itoe elimu juu ya matumizi mazuri ya TEHAMA ili kuepusha migongano baina ya serikali na wananchi.

(vi) Iweke utaratibu utakaozuia watoto kutumia vibaya mitandao ya kijamii na watoto kutotumiwa vibaya na mitandao hiyo ya kijamii kiujumla.

(vii) Ihakikishe inaongeza matumizi ya TEHAMA katika kupunguza msongamano maeneo mbalimbali ya huduma kwa wananchi kama vile Mahakama (kuzifanya kutunza kumbukumbu na mienendo ya kesi kwa njia ya TEHAMA).

(viii) Kuwekeza zaidi katika TEHAMA kwenye masuala ya ulinzi na usalama. TEHAMA inaweza kutumika katika kuweka vifaa maalum vya ulinzi katika mahoteli, kumbi za mikutano, benki na maeneo yote yenye msongamano.

## 11.5 UPATIKANAJI NA UNAFUU WA GHARAMA ZA MATUMIZI YA TEHAMA

### 11.5.1 Hali Ilivyo kwa Sasa Kuhusu Unafuu wa Gharama

Wakati matumizi ya simu za mkononi kufanikisha huduma za fedha zikiipa Tanzania sifa nje ya mipaka yake, yapo baadhi ya maeneo hayana mtandao huo wa mawasiliano – hasa maeneo ya vijijini.

Hata hivyo, hali inaendelea kuwa nzuri kwani asilimia 94 ya wananchi wote nchini wanapata huduma za mawasiliano na serikali imetoa ruzuku kwa kampuni za simu nchini kujenga minara na kufikisha huduma hizo maeneo ambayo hayajaunganishwa.

Hadi sasa, serikali imetoa TZS 95 bilioni kufikisha mawasiliano vijijini na tayari kata 451 zimepata mawasiliano kupitia ruzuku ya serikali. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umetoa zabuni ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata 75 zenye vijiji 154, ambapo kata nane zenye vijiji 15 zimekamilika na mpaka Juni 2019, 67 zilizobaki zitakuwa zimekamilika. Hii ni hatua nzuri sana ya kuendelezwa zaidi.

### 11.5.2 Tamko la Ilani Kuhusu Unafuu wa Gharama

AZAKI tunataka, serikali itakayoingia madarakani:-

(i) Ihakikishe inaendelea kuchukua hatua za kutekeleza mpango wa kuimarisha upatikanaji wa huduma za mtandao (intaneti) kwa bei nafuu kuliko hivi sasa.

(ii) Isimamie kwa ukaribu usambazaji wa mitambo (minara) ya kutoa huduma za mitandao ya simu ifike katika maeneo yote Tanzania.

(iii) Sheria na bei za kuweka mitambo hio iwe na nafuu kuwawezesha wawekezaji kuwekeza zaidi nchini.

(iv) Pia iweke mipango imara ya kushusha bei vya vifaa vya teknolojia ili kuwawezesha wananchi wa vipato vyote kumudu gharama.



# Sura ya 12

# WITO KWA WADAU KIUJUMLA

## 12.1 UTANGULIZI

Kwakuwa uchaguzi ni mchakato unaohusisha na kugusa kila mtu na kila mdau, ni vyema basi kila mdau akahusika kwa kutimiza wajibu wake ipasavyo. Sehemu zilizopita za Ilani hii zimegusia kwa kwa undani masuala ambayo serikali kwa kupitia vyombo vyake vya dola na uchaguzi wanapaswa kuzingatia.

Aidha, viongozi watarajiwa wameakisiwa kwa undani kwenye Nyanja mbalimbali ambazo AZAKI imebaini ni vipaumbele kwa sasa. Sehemu hii ya mwisho ya Ilani inabainisha masuala mengine ya ziada kwa kuwalenga zaidi wadau wengine ambao kwa sehemu kubwa hawakuguswa katika maelezo ya awali. Pia, kuna hitimisho la Ilani.

## 12.2 WITO KWA WADAU MBALIMBALI

### 12.2.1 Kwa Wananchi

- Wananchi ndiyo wadau muhimu katika uchaguzi wa SM wa 2019 na uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika 2020. Hivyo wanapaswa kushiriki kikamilifu katika mikutano yote ya kampeni na kusikiliza sera za wagombea wote wa vyama vya siasa ili wakati wa kupiga kura wafanye maamuzi sahihi.
- Viongozi wabovu huwekwa madarakani na raia ambao huwa hawajitokezi kupiga kura. Hivyo tunawahimiza wananchi wote wajitokeze kwa wingi kujiandikisha kwenye daftari la wapiga kura na siku ya kupiga kura ili kutimiza wajibuwao.
- Aidha wananchi wasikubali kwa hali yoyote kurubuniwa na wanasiasa na kupoteza haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka. Baada ya serikali kuapishwa wananchi wawe tayari kushiriki hatua zote za michakato ya maendeleo badala ya kuwaachia wanasiasa kuamua na kutekeleza wenyewe.
- Nilazima kufuatilia kwa karibu ili kuweza kuwawajibisha viongozi na watendaji wote ambao hawatimizi majukumu na ahadi zao wakati wote.
- Kujiepusha kushiriki kwenye vitendo vyovyote vya vurugu au kutumika kisiasa kwa lengo la kumnufaisha mgombea Fulani.
- Kushiriki kikamilifu katika kufuatilia ilani za vyama vya siasa, kusikiliza ahadi za wagombea ili wakati wa kupiga kura waweze kufanya maamuzi sahihi wakati wa kupiga kura.

### 12.2.2 Kwa Vyama vya Siasa

- Vyama vya siasa vinapaswa kuendesha kampeni za kistaarabu zina-zoheshimu misingi ya sheria na siasa za ushindani ambazo zinatambua kuwa kuna kushinda na kushindwa. Kusiwepo na kampeni za vitisho, matusi na ubaguzi wa aina yoyote na badala yake kuwepo kampeni za kistaarabu zinazoheshimu na zinazozingatia maadili ambayo vyama vyote vya siasa vimesaini.

- Vyama vya siasa vijumuishe matakwa haya ya AZAKI na wananchi katika Ilani zao za uchaguzi.
- Vyama vihakikishe vinasambaza ilani zao za uchaguzi kwa wingi kwa wananchi. Pia, chama kitakachoshinda kiunde serikali na kuipa jukumu la kutekeleza ahadi zote zilizoandikwa kwenye ilani ya chama chao.
- Vyama vya siasa vinapaswa kuzingatia usawa wa kijinsia katika michakato yao ya ndani ya kupitisha wagombea watakaogombea kwenye chaguzi za serikali za Mitaa na uchaguzi Mkuu katika nafasi zote.
- Vyama vya siasa vitoe pia nafasi kwa watu wenye ulemavu waweze kujitokeza kupata nafasi ya kuombea.

**12.2.3 Kwa Wagombea**

- Tunawasihi wagombea wajikite kwenye ajenda za wananchi sambamba na ilani za vyama vyao na kuacha kuwahadaa wananchi kwa ahadi ambazo wanajua hawataweza kuzitimiza.
- Aidha, tunawataka wagombea waache tabia ya kutumia pesa kuwahonga wananchi na njia nyingine zisizostahili kwa lengo la kujipatia madaraka.
- Kujiepusha kutoa kauli zenye kujenga chuki (hate speeches), vitisho dhidi ya wagombea wengine ikiwemo taarifa za uongo
- Wagombea wanapaswa kuheshimu sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi ili kuepusha vurugu dhidi ya wafuasi wa vyama vyao.
- Kuheshimu matokeo ya uchaguzi mara baada ya kutangazwa na iwapo hawaridhiki basi wafuate taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria katika kupinga matokeo, kamwe wasitumie njia zitakazosababisha kuhatarisha amani.

**12.2.4 Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi (Tume za Uchaguzi (NEC na ZEC) na TAMISEMI**

- Tume za uchaguzi na TAMISEMI vifanye kazi kwa uhuru, kufuata sheria, kusimamia kanuni walizokubaliana na vyama vya siasa na kujiepusha kwa namna yoyote kukipendelea chama chochote wakati wote wa mchakato wauchaguzi.
- Vyombo hivyo vinapaswa kuhakikisha kuwa vinawapa mafunzo ya uhakika maofisa na wasaidizi wa uchaguzi na kuchunguza mienendo yao kabla hawajawakabidhi vituo vya kazi ili kuepusha makosa yaliojitokeza wakati wa kuandikisha wapiga kura.
- Vyombo vya kusimamia uchaguzi vinapaswa kufanya maandalizi mapema, pia kusambaza vitendea kazi vinavyotakiwa kwa wakati ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza siku ya upigaji kura.
- Pia vihakikishe kuwa watu wote wenye sifa na wanaostahili kupiga kura ambao hawakuandikishwa kupiga kura kwa sababu mbalimbali ikiwemo wanafunzi, wanaandikishwa katika daftari la kudumu la kupiga kura na wanapiga kura.
- Kuteuwa wasimamizi huru katika kila jimbo na si Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji, Wilaya na Manispaa kama ilivyoagizwa na Mahakama.
- Uboreshaji na uandikishaji wapiga kura ufanyike mapema na kutoa muda Zaidi kwa wapiga kura wenye sifa ili waweze kupata nafasi ya kujiandikisha na kupiga kura.

- Vyombo hivyo vishirikiane na AZAKI na wadau wengine katika kutoa elimu ya Uraia na Upigaji kura kwa wananchi ili kuongeza uelewa.
- Kuendesha kwa uwazi uchaguzi na kutangaza matokeo kwa mgombea aliyeshinda tu na si kinyume chake.
- Kutangaza mapema maeneo ya upigaji kura (vituo) ili vitambulike na wapiga kura kuepusha usumbufu.

### 12.2.5 Vyombo vya Ulinzi na Usalama

- Vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi zake kwa uweledi na tahadhari ya kutowatia hofu wapiga kura na wananchi wote kijumla. Vyombo vya ulinzi visitumie vitisho, nguvu, na silaha za kivita wakati wa mikutano ya kampeni na siku ya kupiga kura.
- Vyombo vya usalama havipaswi kwa namna yoyote kuegemea upande wowote wa chama cha siasa bali vitende haki kwa vyama vyote na wananchi wote wakiwemo wagombea mmoja mmoja na wala visikubali kuyumbishwa na mamlaka yoyote nje ya sheria inayovipa mamlaka kutekeleza wajibu wao.
- Tunalishauri Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Polisi kutojihusisha na mchakato wa uchaguzi kuanzia kipindi cha maandalizi ya uchaguzi, chakampeni, upigaji kura na baada ya upigaji kura na matokeo kutangazwa.
- Vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kufanya kazi kwa weledi katika kuzuia vurugu zozote zinazojitokeza kipindi cha uchaguzi na kampeni.

### 12.2.6 Wadau wa Kimataifa

- Wadau wa kimataifa waendelee kuzisaidia serikali zetu kitaalamu na kifedha ili ziweze kufanikisha mchakato wa uchaguzi huru na wa haki.
- Wadau wa kimataifa waendelee kufanya kazi kwa karibu na AZAKI ili kufanikisha utoaji wa elimu ya uraia na mpiga kura kwa wananchi. Wadau wa kimataifa wajiepushe kuingilia masuala ya ndani ya vyama vya siasa.

### 12.2.7 Watumishi wa Umma

- Watumishi wa umma wanaogombea nyadhifa mbalimbali za kisiasa wasiruhusiwe kutumia rasilimali au mali za umma wakati wa michakato yote ndani ya vyama vya siasa na hata wakati wa uchaguzi mkuu.
- Watumishi wa umma wawe huru wakati wa mchakato wauchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za Mitaa, pia watumie haki yao ya kikatiba kuwachagua viongozi wanaowataka bila ya kupokea shinikizo na vitisho kutoka kwa mtu yeyote ndani na nje ya serikali.
- Watumishi wa umma hawapaswi kuonyesha hadharani mapenzi au mahaba yao au upendeleo kwa chama chochote cha siasa.
- Pia kutojihusisha na kampeni zozote kwa kutumia nafasi zao kama watumishi wa umma

### 12.2.8 Vyombo vya Habari

- Vyombo vya habari na waandishi wa habari wafuate na kuzingatia maadili ya taaluma yao kwa kuhakikisha taarifa wanazozitoa kwa umma hazipendelei chama au mgombea yoyote bali zilenge kuchambua sera za vyama na tija yake kwa wananchi.
- Aidha, vyombo vya habari vya umma vinavyoendeshwa kwa kodi za wananchi vihakikishe kwamba vinawapatia fursa sawa wagombea na vyama vyote vya siasa.

- Watumishi wa umma wawe huru wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu na pia watumie haki yao ya kikatiba kuwachagua viongozi wanaowataka bila ya kupokea shinikizo na vitisho kutoka kwa mtu yeyote ndani na nje ya serikali.
- Vyombo ya habari vinapaswa kuelimisha, kuhamasisha juu ya ushiriki wa wananchi kujitokeza kupiga kura, kushiriki kampeni na hatua zote za mchakato wa uchaguzi wa serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

- Pia vyombo vya habari vinawajibu wa kuonya, kukosoa na kukemea vitendo vyote vya ukiukwaji wa sharia za uchaguzi au vitendo vya vurugu kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi.
- Vyombo vya habari vihakikishe vinatoa taarifa za kweli katika kuwapasha habari wananchi kuripoti taarifa za uchaguzi kwa wagombea na vyama vya.

### 12.2.9 Viongozi wa Dini

- Viongozi wa dini wanapaswa kuhubiri amani kwa wafuasi wao na kujiepusha na kutamka kauli zenye muelekeo wa kupendelea mgombea au chama fulani kwenye maeneo yao ya ibada, majukwaani na hadharani.
- Hata hivyo, wanaweza kutoa ushauri au elimu ya uraia kwa waumini wao na taifa pasipo kuegemea itikadi yoyote.
- Vile vile viongozi wa dini wanapaswa kuonya na kukemea na kupaza sauti dhidi ya aina zozote za vitendo vya ukiukwaji wa sheria kwa waumini au wasimamizi wa uchaguzi, pia kukemea vitendo vyote vitakavyosababisha vurugu.

### 12.2.10 Asasi za Kiraia (AZAKI)

- Asasi za kiraia zinapaswa kusimamia kikamilifu hatua zote za mchakato wa maandalizi ya uchaguzi ikiwemo katika uboreshaji wa daftari la wapigakura, kampeni, kutoa elimu ya upigaji kura na kuwahamasisha wananchi kushiriki.
- Pia AZAKI zitakuwa na wajibu wa kufanya uangalizi wa uchaguzi ili kuangalia mchakato mzima wa uchaguzi na kutoa maono na mapendekezo kwa mamlaka zinazohusika ili kuondoa madhaifu yaliyobainika.
- Kutoegemea upande wowote katika zoezi la uangalizi wa uchaguzi, pia kuhakikisha kwamba wanatoa taarifa kwa kuzingatia weledi na ukweli.
- Kukemea vitendo vya vurugu, uvunjifu wa amani na kuhimiza wananchi, wagombea na viongozi wa vyama vya siasa kuzingatia sheria, maadili na kanuni za uchaguzi.
- Katika kufanya shughuli zote wakati wa uchaguzi AZAKI zinapaswa kujiepusha na kuegemea au kufungamana na upande wowote wa vyama vya siasa.

### 12.2.11 Serikali ya JMT na SMZ

- Serikali hizi zihakikishe mazingira yote wezeshi ya kufanikisha uchaguzi kwa kutoa rasilimali fedha na vifaa kwa vyombo vyenye dhamana ya kusimamia uchaguzi ili kuhakikisha mchakato wa uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za Mitaa upande wa Bara na Visiwani unafanyika kama ilivyopangwa.
- Serikali zote hizi na vyombo vyake vihakikishe vinasimamia uchaguzi wa serikali za Mitaa na uchaguzi mkuu kwa kutoa uwanja sawa kwa vyama vyote kufanya kampeni ili kueneza sera na ilani za wagombea na vyama vyao.
- Kusimamia maadili kwa watumishi wa umma kutojihusisha na siasa au kutumia rasilimali za umma kunufaisha chama Fulani au upendeleo

### 12.2.12 Msajili wa Vyama Vya Siasa:

- Msajili wa Vyama vya Siasa na ofisi yake wanapaswa kutekeleza wajibu wao wa kusimamia utekelezaji wa sheria bila upendeleo au kuegemea chama chochote cha siasa.
- Kutoa miongozo, maelekezo na ushauri kwa vyama vyote ili vitekeleze wajibu wao nyakati za uchaguzi, kampeni na uteuzi wa wagombea nk.




# SURA YA 13

# HITIMISHO

Sisi AZAKI tukiwa ni sehemu ya wananchi na wapiga kura, tunatoa Ilani hii iwe ni dira na mwongozo kwa wananchi, wagombea, tume za uchaguzi, vyombo vya ulinzi na usalama, vyama vya siasa na wadau wengine hapa nchini.

Ni imani yetu kuwa ilani hii itatumika katika kuhakikisha tunakuwa na mchakato wa uchaguzi ambao ni huru, wa haki na usiokuwa na matumizi ya nguvu, rushwa, hongo na matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma.

Aidha, tunayo imani pia kuwa, wagombea, vyombo vya habari, viongozi wa dini na wadau wengine wataepuka lugha za chuki na kibaguzi na uchochezi wa aina yoyote. Kwa kufanya hivyo, Tanzania itaweza kupata viongozi wanao heshimu utu, haki za binadamu na kuwajibika kwa wananchi ambao ndiyo msingi kwa wananchi wanao watumikia kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi.



**TANZANIA HUMAN RIGHT DEFENDERS COALITION (THRDC)**
Mikocheni B, Eyasi Road, P.o.box 105926, Dar Es Salaam, Tanzania
**+255 769 642208/+255657 043191**
**thrddefenders@gmail.com**
**www.facebook.com/TanzaniaHumanRightsDefendersCoalition**
**www.thrd.or.tz**